Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Nane - Tarehe 22 Aprili, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Udhibiti Shehena kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2003 *(The Annual Report and Accounts of the Tanzania Central Freight Bureau, for the Year Ended 30th June, 2003).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 103

**Kupima Maeneo ya *Oysterbay* - Dodoma**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa wakazi wa maeneo ya *Oysterbay*, Maili Mbili na Chang'ombe Mjini Dodoma tarehe 6 Agosti, 2001 waliomba kupimiwa na kuhalalishiwa makazi yao na kukubalika; na kwa kuwa katika swali langu la tarehe 9 Aprili, 2002 nikiomba upimaji wa maeneo, wananchi walipewa matumaini makubwa ya ahadi ya kupimiwa maeneo hayo, kazi ambayo ingefanywa na *CDA* na zoezi kukamilika kabla ya Bunge la Bajeti la Juni, 2002:-

(a) Je, maagizo ya Serikali yanaweza kuachwa au kupuuzwa na watendaji wake na kama hivyo ndivyo ni hatua gani zimechukuliwa?

(b) Je, Serikali inasubiri watendaji wake waanze upimaji wakati wa Uchaguzi Mkuu wa 2005 wakielewa kabisa kuwa kuna athari zitakazotokana na zoezi zima kwa baadhi ya wakazi hao na ni kwa nini zoezi hilo lisifanyike sasa?

(c) Je, ni lini zoezi hilo litaanza ikiwa wakazi wako tayari na wanasubiri kwa hamu utekelezaji wa maagizo ya Serikali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIR MKUU ( MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, nilipojibu swali lake Na. 1447 tarehe 9 Aprili, 2002, niliarifu kwamba, Serikali ilishakubali ombi la wananchi wa eneo la Ukanda wa *Oysterbay*, Chang'ombe, Maili Mbili hadi Mnadani, kuhalalishwa na kuingizwa kwenye mpango kamambe wa Mji huu wa Dodoma. Aidha, niliagiza yafanywe maandalizi kujua gharama na utaratibu wa wananchi watakavyochangia kufanikisha zoezi hilo. Kazi imefanyika vizuri kwa kuwashirikisha Viongozi wa Kata na Mitaa wa maeneo husika. Jumla ya shilingi milioni 11 zimetumika kwa mafunzo, ramani, picha za anga na tathmini zote zinazohusika. Hata hivyo, kiasi cha zaidi ya shilingi milioni 175 zinazotakiwa kuwezesha zoezi hili mpaka hatua ya kukamilika upimaji wa viwanja vitakavyohalalishwa, zimebainika kuwa ni nyingi kuzidi uwezo wa wananchi wengi wanaoishi eneo la mradi na Serikali inaendelea kutafuta fedha ikiwa ni pamoja na kutoka kwa Wahisani walioonyesha nia kama *DANIDA* na *UNDP* ili kuikamilisha azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya machache, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ahadi za Serikali kuhusu kuhalalishiwa na kupimiwa viwanja maeneo ya Mailimbili, Chang'ombe na *Oysterbay,* yametekelezwa na matayarisho yote ya namna zoezi litakavyofanywa kwa kushirikisha walengwa na upembuzi wa gharama zitakazohitajika, kutoka kwa walengwa na nje ya walengwa, tayari zimebainishwa, tatizo kwa sasa, ni uwezo wa kutekeleza zoezi hili.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Mamlaka husika zinaendelea na utekelezaji wa masuala yasiyohitaji fedha nyingi na ni mategemeo ya Serikali kuwa zoezi hili litakamilika mapema jinsi uwezo wa utekelezaji utakavyopatikana.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zoezi hili linatekelezwa kwa kuwashirikisha wananchi ikiwa ni pamoja na kuchangia gharama, tunawaomba viongozi wote pamoja na Mheshimiwa Mbunge wa Dodoma Mjini na Mheshimiwa Nyawazwa, waendelee kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi kuchangia gharama ili tuweze

kukamilisha utekelezaji wa awamu muhimu ya zoezi la uhalalishaji ambayo ni upangaji muafaka wa viwanja na upimaji wa viwanja husika.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini naomba niulize kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa *CDA* walikwenda Dar es Salaam kujifunza jinsi ya upimaji wa maeneo ya Manzese na Temeke kwa ajili ya ardhi. Je, wakazi wa maeneo tajwa kwenye swali langu la msingi wamefaidika vipi na mafunzo hayo?

Pili, kwa kuwa wakazi wa eneo hilo wanaelewa fika kwamba Serikali haina uwezo wa kufikia kiwango hicho na wao wako tayari katika kuchangia gharama hizo, je, ni lini sasa Serikali itaanza kukusanya fedha kwa wakazi wote wanaoishi na wao wako tayari?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, eneo hili la *Oysterbay* lina wakazi 6,000 na nyumba ambazo zinahitaji kuhalalishwa ni kiasi cha nyumba 6,000. Nimesema hapa kwamba, *CDA* imeshatumia shillingi 11,000 milioni, kati ya hizo fedha shilingi 6 milioni zimetumika kununua ramani kutoka kwa Idara ya Sensa, ambayo ilitumia ndege katika kupima eneo lile na ramani tunazo.

Ni kweli wana-*CDA* walikwenda Hananasif Dar es Salaam, kujifunza jinsi utekelezaji wa wa mpango wa aina hii ulivyotekelezwa kwa mafanikio makubwa. Waliporudi wamewashirikisha wananchi kuhamasisha katika eneo lile na kuunda vikundi ili utekelezaji ufanane sana na Hananasif. Zoezi la uhamasishaji lilishirikisha Viongozi wote akiwemo Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na Mkuu wa Wilaya Dodoma Mjini. Kwa hiyo, wananchi wamenufaika sana na hivi sasa wanafahamu umuhimu wa upimaji lakini namna ya hatua zitakavyokuwa za upimaji katika eneo hilo.

Lakini la pili, nafurahi sana kusikia kutoka kwa Mheshimiwa Esther Nyawazwa kwamba, wananchi wako tayari kuchangia. Tulishaainisha gharama kwamba kama mwananchi atachangia shilingi 30,000, *CDA* iko tayari kupima mpaka hatua ya kutoa hati. Kama wananchi wako tayari kuchanga, mimi niko tayari kuanzisha zoezi hilo la uchangishaji kuanzia kesho. *(Makofi)*

Na. 104

**Bendera ya Bunge Katika Ofisi Zake na Kwenye Majimbo**

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni Bunge la Tanzania limeanza kupeperusha bendera yake kwenye Ofisi ya Makao Makuu ya Bunge Dodoma, kwenye Ofisi Ndogo za Bunge za Dar es Salaam na Zanzibar na kwenye Ofisi za Wabunge Majimboni na kadhalika na kwa

kuwa kiutawala nchi imegawanyika katika nguzo tatu yaani Bunge, Mahakama na Serikali:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya bendera kama kitambulisho kwa nguzo ya Mahakama wakati nguzo nyingine yaani Serikali na Bunge tayari zina bendera zao?

(b) Je, kwa nini Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano hapeperushi bendera mezani kwake ndani ya Bunge wakati baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanapeperusha bendera zao katika Ofisi zao Majimboni?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mbunge wa Matemwe, kama ifuatavyo:-

(a) Mahakama kama mojawapo ya mihimili ya dola, hutumia bendera na nembo ya dola. Utaratibu huu pia hutumika katika mfumo wa sheria unaotumika katika nchi zote za Jumia ya Madola. Kwa vile kazi kubwa ya Mahakama ni kutekeleza majukumu ya dola, kutokana na mazoea, Mahakama katika nchi nyingi, hutumia nembo ya bendera ya dola tu. Pamoja na utaratibu huo, Serikali inaona kwamba, suala la Mahakama kuwa na bendera ya kuitambulisha ambayo itakuwa ikitumika sambamba na bendera ya Taifa linazungumzika. Hata hivyo, si kweli kwamba, Serikali kama mhimili mmojawapo wa dola ina bendera yake. Serikali hutumia bendera na nembo ya Taifa ambavyo ni vielelezo vya dola ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, vielelezo ambavyo vimekuwa vikitumiwa pia na Bunge na Mahakama.

(b) Kielelezo cha Mamlaka ya Spika anapokuwa anatekeleza shughuli za Bunge Bungeni, hutambulishwa na Siwa, yaani Rungu la dhahabu lililopo mbele yetu hapa Mezani na ndiyo maana Rungu hilo huingizwa na kutolewa Bungeni kwa heshima zote. Matumizi na upeperushaji wa bendera ya Bunge unasimamiwa na Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge ya Mwaka 1988 kama ilivyorekebishwa, pamoja na Kanuni za Bunge. Kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Bunge, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kama ilivyo kwa Waheshimiwa Wabunge, anaruhusiwa kupeperusha bendera ya Bunge katika meza anayofanyia kazi ofisini kwake, ndiyo maana kwa kutambua ukweli kwamba, siwa ndicho kielelezo halisi cha Mamlaka ya Spika anapokuwa anatekeleza shughuli za Bunge humu Bungeni, Sheria na Kanuni za Bunge zipo kimya kuhusu stahili ya Spika kupeperusha bendera ya Bunge katika meza yake humu Bungeni. *(Makofi)*

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mwanasheria Mkuu kwa majibu yake mazuri. Lakini pamoja na majibu yake mazuri, nina suala moja dogo la nyongeza.

Wakati Wabunge tukiwa katika maeneo yetu au hata nje ya Jiji la Dar es Salaam, Zanzibar na Dodoma, tunakuwa tunapeperusha bendera kama kanuni ilivyokuwa

inaelekeza. Kuna madhara yoyote yale kupeperusha bendera kwenye magari ya Bunge tunayotumia kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma na kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nimemweleza vizuri kuhusu Waheshimiwa Wabunge wanapokuja kwenye shughuli za Bunge kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma na kuondoka Dodoma kwenda majumbani. Kama wanakuja kwa usafiri wa mabasi ama pawepo na mlingoti unaopepea. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, upeperushaji na matumizi ya bendera umeainishwa katika Sheria na Kanuni za Bunge. Matumizi ya bendera ya Bunge kwenye *public transport* kama hayo mabasi si miongoni mwa vyombo ambavyo vinaruhusiwa kwa Waheshimiwa Wabunge kutumia. *(Makofi)*

Na. 105

**Upatikanaji wa Huduma za Afya Vijijini**

**MHE. KHALID S. SURU** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna baadhi ya Kata na Vijiji vikubwa ambavyo viko mbali na Huduma ya Afya; yaani Hospitali, Kituo cha Afya au Zahanati ya Serikali au hata Shirika Lisilo la Kiserikali na kwamba wananchi hao wanapata shida na kero kubwa ya kutembea mwendo mrefu wa zaidi ya km. 8 - 25 kufuata huduma hizo; na kwa kuwa wananchi wenyewe wapo tayari kushirikiana na Serikali/*TASAF* au Shirika lolote lisilo la Kiserikali *(NGOs)* katika kujenga Kituo cha Afya/Zahanati lakini Serikali inakwamisha kwa kisingizio cha sera na upungufu wa watumishi; na kwa kufanya hivyo Serikali inakuwa imekwamisha juhudi zake za kisera za kutoa huduma nzuri za afya kwa wote:-

(a) Je, Serikali inawaambia nini wananchi waliokubaliana mathalan *TASAF* kwa mujibu wa uamuzi wao wa kujenga majengo hayo na kukamilika na kuweka watu binafsi kwa lengo la kusogeza huduma hiyo karibu na wananchi kwa vile uwezo wa Serikali peke yake hautoshi kwa wakati huu?

(b) Kwa kuwa sasa ni wakati muafaka kwa Serikali kuhakikisha kuwa kila Kijiji kinakuwa na Zahanati yake kwa kushirikisha Mashirika yasiyo na Kiserikali *(NGOs)* na watu binafsi; je, kwa nini Serikali inashindwa kuanzisha mikakati ya kutufikisha mahali ambapo wananchi watafaidika na ukaribu wa huduma za Afya?

(c) Je, ni lini Vituo vya Afya na Zahanati zisizo na umeme na simu zitapatiwa huduma hiyo hata kama ni simu za upepo *(Radio Calls)* ili kurahisisha matibabu na mawasiliano?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalid Suru, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni Sera ya Serikali hivi sasa kubinafsisha baadhi ya shughuli zake na kushirikisha wananchi na sekta binafsi katika kupanga na kutoa huduma mbalimbali hapa nchini ili kuipunguzia gharama za uendeshaji au uwekezaji. Hivyo, ni dhahiri kuwa watu binafsi wanaruhusiwa kufungua na kuendesha huduma za Afya karibu na wananchi hata kwa kutumia majengo yaliyojengwa chini ya makubaliano ya wananchi na Asasi mbalimbali kama vile *TASAF,* Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* na Wadau wengine ili mradi waendeshaji vituo hivyo wanazingatia sheria, taratibu na kanuni zilizowekwa na Serikali. Kwa hiyo, napenda kuchukua fursa hii, kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini, kwa kuwa tayari kushirikiana na *TASAF* au Shirika lolote lisilo la Kiserikali katika kujenga majengo ya Zahanati/Vituo vya Afya na kuyakabidhi kwa watu binafsi, kuendesha vituo hivyo kwa lengo la kusogeza huduma kwa wananchi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inayo mikakati thabiti ya kuhakikisha kwamba, wananchi wanakuwa karibu na huduma za afya. Utaratibu wa kuwa na Zahanati au Kituo cha Afya upo wazi kwa mujibu wa sera ya afya. Kama nilivyojibu swali Na. 92 la Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufindi, tarehe 11 Februari, 2004, Zahanati moja inatakiwa kuhudumia watu wapatao 10,000 na kituo kimoja cha Afya kinakadiriwa kutoa huduma kwa watu wapatao 50,000 au wakazi wa Tarafa moja. Kwa hiyo, dhana ya kila Kijiji kuwa na Zahanati yake au Kituo cha Afya kwa kuzingatia Bajeti ya Serikali, kwa mazingira ya sasa haiwezekani. Lakini kwa kutumia Asasi au *NGOs* nyingine, kushirikiana na Halmashauri zinazohusika, wanaweza kabisa wakaendesha Zahanati au Vituo vya Afya katika maeneo yao.

(c) Mheshimiwa Spika, Zahanati na Vituo vya Afya visivyo na umeme au simu vitapatiwa huduma ya simu za upepo *(Radio Calls)* kufuatana na uwezo wa fedha wa Serikali na jinsi kila Wilaya ilivyojipangia kutokana na Programu ya Mfuko wa pamoja wa Afya *(Health Basket Fund).* Katika Wilaya ya Kondoa kati ya Zahanati 40 za Serikali, Zahanati 15 zina simu za upepo *(Radio Calls),* Vituo vya Afya 3 kati ya vituo 4 pamoja na Hospitali ya Wilaya vina huduma ya simu za upepo *(Radio Calls)*. Aidha, Wilaya inao mpango wa kuongeza simu za upepo *(Radio Calls)* katika vituo vyake vya huduma kupitia mpango wa Bajeti wa Mfuko wa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa umeme kwenye Vituo vya Afya na Zahanati, Halmashauri ya Wilaya haikuweza kuweka mpango huo katika mipango na bajeti yake ya mwaka kutokana na ufinyu wa bajeti. Hata hivyo, kwa kutumia fursa ya umeme wa *grid* ya Taifa, upitao karibu na baadhi ya Vituo vya Afya na Zahanati na kwa kutumia fursa ya teknolojia zingine sahihi za kupata umeme, Halmashauri ya Wilaya kwa

kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo, ipo tayari kufikiria uwezekano wa baadhi ya Vituo vya Afya na Zahanati kupatiwa huduma ya umeme. Pamoja na juhudi hizi za Serikali, napenda kutoa wito kwa wananchi wa Kondoa kuwa na mikakati thabiti ya kulinda mali zilizokwisha tolewa zisiibiwe wala kuharibiwa ovyo ovyo.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Lakini pia namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Kwa kuwa suala la huduma ya afya ni muhimu sana kwa wananchi wote na kwamba afya nzuri kwa kweli ndiyo inachangia kiuchumi, kijamii na kisiasa. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba ni vyema tukaanzisha mpango wa dharura unaofanana na ule wa MMEM ili kuwezesha kufikisha utaratibu wa afya kwa wote Vijijini?

Pili, kwa kuwa wananchi wetu wengi ni maskini na kwa sababu hiyo hawaendi kwenye matibabu kama inavyotakiwa na kwa sababu hiyo basi vifo huwa vinaongezeka. Je, Serikali haina utaratibu wowote wa kuweza kupunguza hizi gharama au kuondoa hizi gharama ili wananchi wengi zaidi watibiwe ili kuokoa vifo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza ambalo *actually* inaiomba Serikali itazame uwezekano wa kuwa na mpango kamambe kama tulionao hivi sasa wa MMEM ili kuweza kukidhi mahitaji makubwa katika sekta hii ya afya, ni wazo zuri nafikiri Serikali haina ugomvi na rai yake. Lakini nilitaka vile vile ajue na kutambua kwamba juhudi ambazo Serikali inafanya hivi sasa kupitia mpango wa *Basket Funding,* hautofautiani sana na mpango anaoufikiria yaani wa MMEM. Karibu juhudi ni zile zile na kwa kweli misingi yake ni ile ile.

Lakini pili, kuhusu hali ya umaskini wa wananchi hapa Tanzania, kutokuwa na uwezo wa kuweza kupata matibabu, mambo haya kwa ujumla ni ya kisera na mimi nina hakika Mheshimiwa Khalid Suru anaona juhudi za Serikali zinavyofanyika katika kujaribu kupunguza gharama za matibabu katika maeneo mbalimbali. Kwa upande wa Vijijini yeye anafahamu vizuri sana. Sehemu kubwa basi matibabu yako chini sana ili kuwezeshwa watu wengi kuweza kupata fursa hiyo. Sasa tunahamasisha mpango wa Afya ya Jamii ili huduma hizo ziweze kuwa nafuu zaidi, unapolipia shilingi 10,000 kwa mwaka basi zinatosheleza kukidhi mahitaji yako yote.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kutokana na maelezo yake, Mheshimiwa Naibu Waziri, anaelewa kwamba *Basket Funding* kusema kweli ni fedha ndogo sana. Kwa maana hiyo basi, Zahanati zilizokubaliwa zibadilishwe kuwa Kituo cha Afya kwa mfano, Mbwera ambayo mpaka sasa hivi tangu mwaka 1994 haijakamilika, je, Mheshimiwa Naibu Waziri yeye mwenyewe ameshuhudia na kulishughulikia suala hilo kwa muda mrefu, anasemaje sasa?

Kusema kweli inaliza kwa sababu kuna visiwa 18 ambavyo watu wanakufa kila siku sasa ina maana mpaka Mbunge wao nilie hapa Bungeni maana yake nini?

Namwomba Naibu Waziri ajibu sasa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nadhani nia yake alitaka kufikisha ujumbe kwamba, Kituo cha Afya cha Mwera, hakijakamilika, lakini amepandia kwenye swali hili.

Mimi naomba nimhakikishie kwamba, Mheshimiwa Prof. Juma Mikidadi, hili suala tutalimaliza kwa sababu unazijua juhudi tunazofanya pale kujaribu kumaliza mgogoro huo wa muda mrefu.

Na. 106

**Kuwaondoa Madiwani Kwenye Bodi za Tenda**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilikuwa na nia njema ya kuwaondoa Waheshimiwa Madiwani katika Bodi za Tenda; na kwa kuwa Serikali inasema kuwa kumekuwa na mafanikio toka suala hilo lianze kutekelezwa:-

(a) Je, kwa nini bado yapo malalamiko ya tenda hizo kutolewa kwa upendeleo katika Halmashauri mbalimbali?

(b) Kwa kuwa ni kanuni ya Serikali kwamba ukiwa Mjumbe wa Bodi na ukawa na mradi unaomba kazi katika Halmashauri hiyo hiyo unapaswa kutangaza kujiondoa katika kikao ili uamuzi wako usiathiri maamuzi ya Bodi, je, ni mara ngapi jambo kama hilo limetokea kwa Mjumbe wa Bodi kujitoa kwa sababu ya kuomba kazi ndani ya Bodi au Halmashauri?

(c) Kwa kuwa wanaohusika kuzivunja kanuni hizo hujificha sana kwa kutumia majina ya watoto wao au waume zao au hata marafiki zao; na kwa kuwa Serikali haijafanya uchunguzi wa kina kuhusu utata huo; je, Serikali haioni kuwa upendeleo na rushwa inaendelea katika kazi ya utoaji wa tenda hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utoaji wa zabuni katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa hutolewa kulingana na Kanuni za Manunuzi zilizotolewa mwaka 2003 *(The Local Government Procurement of Goods and Works Regulations, 2003).* Ofisi yangu hadi sasa haijapokea malalamiko yoyote ya zabuni kutolewa kwa upendeleo katika Halmashauri yoyote nchini, kinyume chake taarifa tulizopata zinaonyesha maendeleo mazuri ya utoaji wa tenda na baadhi ya taarifa hizo tumezipata kutoka kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliopo hapa.

(b) Mheshimiwa Spika, si rahisi kusema ni Wajumbe wangapi walijitoa katika vikao vya zabuni ili uamuzi wao usiathiri maamuzi ya Bodi. Kanuni za Zabuni za Halmashauri zilizotolewa kwenye Notisi za Serikali *(GN No. 279* na *281)* za mwaka 2000, haziruhusu Mjumbe wa Bodi ya Zabuni, kushiriki katika kutoa maamuzi kwenye zabuni ambayo ana maslahi yake binafsi. Hivyo, mara zote suala la namna hiyo linapojitokeza, Mjumbe hulazimika kutoka nje ya kikao ili kutoathiri maamuzi ya Kikao cha Bodi. Pia kanuni hizo zinaelezea wazi taratibu zote zinazotakiwa kufuatwa katika utoaji wa zabuni. Hivyo, Serikali inaendelea kusisitiza kila Halmashauri izingatie kanuni zilizotolewa katika utoaji wa zabuni.

(c) Mheshimiwa Spika, hadi sasa Serikali haijabaini mtumishi yeyote aliyevunja kanuni hizi kwa kujificha akitumia majina ya watoto wake, mume au mke wake au marafiki. Ni wazi kama vitendo hivyo vitatokea na vitabainika wazi wazi, basi jambo hilo litashughulikiwa mapema iwezekanavyo. Kwa hiyo, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla, kutoa taarifa Ofisini kwangu au kwenye vyombo vya kutoa haki kama vile *PCB,* pale wanapoona taratibu na kanuni za utoaji zabuni zimekiukwa. Serikali haitasita kuchukua hatua kali dhidi ya mtumishi yeyote atakayebainika kukiuka maadili ya utumishi wa umma.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuweza kuuliza walau swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, Wizara yake haijapokea malalamiko yoyote, wakati Waheshimiwa Wabunge wengi sana wanafahamu jinsi wafanyakazi wa Serikali za Mitaa, ambao wamebadilisha majina au wametumia majina ya watoto wao au kuweka majina ya marafiki zao na wanaendelea kupata zabuni hizi pia wengine kama Wajumbe wakihudhuria katika vikao hivi vya Bodi. Wizara itakuwa tayari kupeleka wataalamu ili waende katika kila Halmashauri waweze kupeleleza kujua ni jinsi gani watu wameanza kujinufaisha na mtindo huu na kujipatia fedha kwa kutumia ofisi zao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kufahamu juu ya hali hiyo iliyoelezwa na Mheshimiwa Mwananzila ni jambo moja. Lakini kwa kweli kutoyafikisha mawazo haya au malalamiko haya katika vyombo vinavyohusika nadhani ndiyo kikwazo kikubwa katika kufanikisha maamuzi mazuri ya Serikali.

Mimi naomba tu kama kweli Waheshimiwa Wabunge, mnazo taarifa za hakika kuhusiana na uvunjaji wa maadili haya, mimi nasema karibuni sana TAMISEMI, tunaweza kabisa tukapambana nao kuhakikisha kwamba mambo haya yanakomeshwa. Wote mnajua shughuli za namna hii ni za siri siri kwa hiyo inataka kidogo umakini katika kujaribu kufikia maamuzi fulani fulani. Lakini ofisi inaendelea na tunao utaratibu wa kupita na sisi kuangalia uendeshaji wa shughuli. Kwa hiyo, nina hakika tukishirikiana tunaweza kabisa tukafikia mahali pazuri.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa taratibu za fedha za Halmashauri zinataka mikataba yote iwekwe sahihi na Mwenyekiti wa Halmashauri husika; na kwa kuwa hivi sasa Madiwani si Wajumbe wa Kamati za Tenda; Serikali inasemaje pale Wenyeviti wanapokuwa hawakushirikishwa katika hatua za awali za kutoa tenda halafu kuja kutakiwa kuweka sahihi kwenye mikataba? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Mwenyekiti wa Halmashauri kuweka sahihi yake katika hati acha mkataba wowote, ni utaratibu wa kisheria kuonyesha kwamba, hiyo ni *document* halali ambayo ni mali ya Halmashauri. Kwa hiyo, utaratibu huu hauhusu mikataba hii ya zabuni tu. Ni utaratibu ambao unatawala hati zote ambazo zinatakiwa kuwa *authenticated.*

Sasa kwa sababu huyu Mwenyekiti au Diwani hashiriki katika tenda, basi jambo hilo haliwezi kupata uhalali huo, mimi nasema si kweli. Si kweli kabisa lakini nataka niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba, tulifikia uamuzi huu baada ya kuonekana kwamba, utaratibu uliokuwepo wa Madiwani kufanya maamuzi na Madiwani hao hao kukaa na kutekeleza maamuzi yao ulionekana una matatizo makubwa. Kwa hiyo, ndiyo maana tutakubaliana na tukabadili sheria, Diwani hasa afanye kazi ya ku-*cross check* juu ya utendaji wa wataalamu katika Halmashauri yake. Mimi nadhani dhana hii ni sahihi na kinachohitajika kwa kweli ni ushirikiano tu kati yetu na wadau wengine wote. *(Makofi)*

Na. 107

**Kuzagaa Ovyo kwa Vifaa vya Plastiki**

**MHE. ALHAJI AHAMADI HASSAN MPEME** aliuliza: -

Kwa kuwa matumizi ya vifaa vya plastiki kama vile mifuko ya rambo, chupa za maji ya kunywa na vyombo mbalimbali vinazidi kuongezeka hapa nchini; na kwa kuwa baada ya matumizi ya vifaa hivyo hutupwa ovyo na kuachwa vikizagaa zagaa katika maeneo mengi na hatimaye kusababisha uchafuzi mkubwa wa mazingira ambao unachangia kuleta magonjwa mbalimbali kama ugonjwa wa matumbo, malaria, kipindupindu na kadhalika: -

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kubadilisha matumizi ya vifaa hivyo na kutafuta vifaa mbadala?

(b) Kwa kuwa vifaa hivyo sasa vinazagaa ovyo katika maeneo mengi ya nchi yetu, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba vifaa hivyo vinaondoshwa katika maeneo yote ya nchi yetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Hassan Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo: -

Kwanza, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, utupaji holela wa mifuko, chupa za plastiki na bidhaa nyinginezo za plastiki, umesababisha kuzagaa ovyo kwa taka za plastiki ambazo husababisha uchafuzi wa mazingira na pia athari kwa mifugo na afya ya binadamu.

Tatizo la kuzagaa ovyo kwa taka za plastiki linatokana na usimamizi hafifu wa taka hizo. Katika nchi zilizoendelea ambapo bidhaa za plastiki hutumika kwa wingi sana kuliko katika nchi zinazoendelea, hakuna tatizo la kuzagaa kwa taka za aina hiyo. Hii inatokana na mipango madhubuti ya kurejeleza taka hizo. Hili neno kurejeleza naambiwa Kiingereza chake ni *to recycle.*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Hassan Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Kwa kutambua kero ya uchafuzi wa mifuko ya plastiki, Serikali imeongeza kodi kwenye mifuko ya plastiki kwa madhumuni ya kupunguza utumiaji wa mifuko hiyo na kuinua uingizaji, utengenezaji na matumizi ya mifuko mbadala. Matarajio ni kwamba, watumiaji wakuu na wananchi kwa ujumla, wataanza kuona gharama kutumia mifuko ya plastiki na hivyo kutumia vifaa mbadala.

Ili kukabiliana na tatizo la uchafuzi wa mazingira unaotokana na taka za plastiki, Serikali imechukua hatua kadhaa ambazo ni pamoja na hizi zifuatazo: -

(i) Kuhamasisha viwanda vinavyotengeneza bidhaa za plastiki vijihusishe zaidi na kurejeleza taka za aina hiyo. Tayari katika Jiji la Dar es Salaam, baadhi ya viwanda vimeanza kurejeleza taka za plastiki, viwanda hivyo ni *Simba Plastics, Patel Plastics, Cotex, Poly Sacks* na *Centac Plastic;*

(ii) Kukamilisha ujenzi wa kituo cha taka rejea *(recyclable)* katika Jiji la Dar es Salaam kwa msaada wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda *(UNIDO),* ambapo taka aina ya plastiki huchambuliwa na kutayarishwa kuwa malighafi

ya viwanda vingine. Tayari kituo kimeshafanyiwa majaribio na wafanyakazi wameshapatiwa mafunzo. Kwa sasa taratibu zinakamilishwa za kukiwezesha kituo hicho kujiendesha kibiashara. Kituo kina uwezo wa kurejeleza kiasi cha kilogramu 100 za taka za plastiki kwa sasa; na

(iii) Kushirikisha Asasi na vikundi mbalimbali visivyo vya Kiserikali *(NGOs* na *CBOs)* katika maonyesho ya bidhaa mbalimbali zilizotengenezwa kwa kutumia plastiki rejea kama vile madawati ya shule, meza na mabomba ya kupitishia waya za umeme. Lengo hasa ni kukuza weledi na kujenga hamasa kwa jamii kuhusu jukumu na nafasi ya umma katika kukabiliana na tatizo la kuzagaa kwa taka za plastiki.

Mheshimiwa Spika, mwisho, pamoja na hatua nilizozitaja, Serikali inahimiza wananchi kuwa na mazoea ya kutenganisha na kukusanya taka za plastiki kila mmoja mahali alipo ili kupata malighafi ya kutosha na safi kwa ajili ya kutumiwa na viwanda vinavyodurufu plastiki.

**MHE. ALHAJI AHAMADI HASSAN MPEME:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba vifaa hivi sasa vimeongezewa kodi ili kupunguza matumizi yake na kwa kuwa uzagaaji umekuwa mkubwa kiasi ambacho Halmashauri zetu zinashindwa kumudu kukusanya taka hizo. Je, hicho kiasi cha kodi kilichoongezwa, Serikali inaonaje ikatenga fedha hizo ili kuzipa uwezo Halmashauri zetu kuweza kumudu kupambana na kukusanya taka hizo? *(Makofi)*

(b) Kutokana na swali la msingi nililozungumzia kwamba linasababisha magonjwa kadhaa, kwa binadamu pamoja na wanyama, sasa nina hisia kwamba, athari hiyo inaweza kupatikana katika ardhi kutokana na kiwango cha taka kinavyoenea kwa kasi kubwa. Je, Serikali ipo tayari sasa kufanya utafiti kuangalia kwamba ardhi yetu inaweza ikaathirika kiasi gani kutokana na kuzagaa kwa taka hizo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kimsingi linahusu nyongeza ya kodi katika hii mifuko ya plastiki kwamba, fedha inayopatikana sehemu/kiasi ipelekwe kwenye Halmashauri ili iweze kupambana na tatizo la taka za plastiki zinazozagaa ovyo.

Mheshimiwa Spika, ningependa niseme kwamba, wazo hili ni jema kwa sababu Serikali inapotoza kodi lengo ni kuinufaisha jamii. Kwa hiyo, kama mapato yatakuwa ya kutosha na ikaonekana tatizo hili kama tunavyofahamu ni kubwa, ninaamini kimsingi haliko tatizo la kuweka au kutoa sehemu ya fedha zinazopatikana kusaidia Halmashauri zetu kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa niongezee kwamba, tunaotupa taka ni baadhi yetu, miongoni mwetu wanajamii. Sasa, pengine ni vizuri tukaanza kujenga

utamaduni wa kutochafua maeneo tunamoishi kwa kutupa taka ovyo ili tusizitwishe mzigo Halmashauri zetu.

La pili kuhusu hii mifuko kwamba, Serikali ifanye utaratibu na ichunguze kama ina athari kwa ardhi. Kwanza, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Alhaji Mpeme kwamba, mifuko hii ya plastiki pale inapotupwa wala huhitaji kufanya uchunguzi, pengine ni kuarifiwa tu kwamba ardhi inaathirika vipi. Ardhi inahitaji hewa na maji ili iweze kustawisha kitu chochote kwa maana ya *bacteria* waweze kustawi. Sasa mifuko ya plastiki pale inapokuwa imetuama au imekaa, hewa na maji haviingii na maana yake ni kwamba, *bacteria* ardhini wanakufa na ardhi ile kiukweli kweli inakuwa ni jangwa haiwezi kustawisha kitu. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais ndiyo yenye kusimamia na kushughulikia uondoshaji wa umaskini nchini na hivi karibuni vijana walijikusanya pamoja katika Mkoa wa Dar es Salaam na kuanzisha mradi wa kutengeneza mikoba na vikapu vizuri ambavyo matumizi yake ni bora zaidi kuliko mifuko ya plastiki. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba upigaji marufuku wa uingizaji wa mifuko ya rambo nchini ndiyo *solution* ya matatizo haya yote? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, wazo hili la kupiga marufuku mifuko ya plastiki si mara ya kwanza kusikika katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema kwamba, mifuko hii ya plastiki iko ya aina unaweza ukasema mbalimbali. Iko ile ambayo ni myembamba sana na haiwezi kurejelezwa *(non-recyclable).* Sasa hii ni kweli kabisa kwamba, wakati umefika tuipige marufuku. Lakini hii mingine ambayo tumesema na jana wakati najiandaa kuja hapa, nilipita barabara ya Sam Nujoma, nilikuta kikundi nadhani ni kama hivyo vikundi anavyovisema Mheshimiwa Mbunge, wanakusanya hizi chupa za plastiki na nina hakika ni katika utaratibu tuliousema katika jibu la msingi kwamba, baadhi ya plastiki hizi zikirejelezwa zinakuwa ni malighafi kwa mali nyingine.

Kwa hiyo, mifuko ambayo haiwezi kurejelezwa ni muhimu kwa kweli ikapigwa marufuku kwa sababu haina manufaa yoyote, inaharibu ardhi yetu.

Na. 108

**Usafiri wa Daladala**

**MHE. ASHA ALI NGEDE** aliuliza:-

Kwa kuwa Wananchi walio wengi waishio Dar es Salaam kama ilivyo kwa Mikoa mingine hapa nchini, hutumia usafiri wa mabasi maarufu kwa jina la daladala na kwa kuwa wasafiri watumiao usafiri wa aina hiyo kama ilivyo desturi hutoa nauli, lakini kitu ambacho siyo cha kawaida wahusika hawatoi tiketi kwa abiria na kama wakitoa tiketi basi tiketi hizo huwa hazina tarehe: -

(a) Je, Serikali inalifahamu jambo hilo na kwamba sheria inasemaje hasa kwa kuwa gari likipata ajali Wananchi watumiao magari hayo wamekuwa wakipata bughudha za kila aina na uwezekano wa kuwadhibiti wahusika haupo; je, kwa nini Serikali haitekelezi ile azma yake ya kuruhusu magari makubwa yatumike kwa Dar es Salaam badala ya haya ya sasa na utaratibu huo utatekelezwa lini?

(b) Kwa kuwa moja kati ya bughudha wanazopata abiria ni pamoja na ile hali ya magari ya daladala kujaza abiria kinyume cha taratibu na sheria zilizowekwa, je, ule utaratibu wa kutokusimamisha abiria *(Level Sitting)* ambao ulisimamiwa na Kamanda Alfred Tibaigana umefikia wapi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Ngede, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, kifungu cha 28 cha Sheria ya Leseni za Usafirishaji ya Mwaka 1973 *(Transport Licensing Act. No. 1 of 1973)* kinaagiza kwamba, kila mmiliki wa basi sharti atoe tiketi kwa abiria kwa nauli aliyotoa na pia kwa mujibu wa sheria hiyo, abiria anayo haki ya kudai tiketi anapolipa nauli. Kupata tiketi ni haki ya msingi ya abiria ambayo ni kielelezo cha mkataba kati ya abiria na mmiliki wa basi. Nawataka wenye mabasi wote wahakikishe kwamba, watumishi wao wanaitekeleza kwa ukamilifu sheria hii.

Aidha, natoa wito kwa Wananchi wasisite kutoa taarifa Polisi, kila wanapotozwa nauli bila ya kupewa tiketi ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi ya wamiliki wakorofi wa mabasi na/au watumishi wao (madreva na makondakta). Aidha, kuhusu matumizi ya magari makubwa ya abiria Jijini Dar es Salaam badala ya daladala katika njia kuu, Serikali kupitia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, inaendelea na maandalizi ya mradi wa mabasi makubwa yaendayo haraka *(Bus Rapid Transit - BRT).* Mradi huu unatazamiwa kuanza kwa majaribio mwishoni mwa mwaka 2005. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa abiria wa daladala wanapata bughudha kutokana na mabasi hayo kujaza abiria kupita kiasi. Hali hii ni kinyume cha sheria. Sheria ya leseni inataka kila gari la abiria kujaza abiria kulingana na leseni yake. Kwa hiyo, agizo alilotoa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dar es Salaam, kuhusu daladala kutosimamisha abiria *(Level Sitting),* linazingatia mahitaji ya sheria. Agizo hilo bado lipo na linapaswa kuheshimiwa. Zoezi la kutekeleza sheria hiyo ni la kudumu. Madreva na makondakta wa daladala wanaozidisha abiria, wanaendelea kukamatwa na kushtakiwa. Hata hivyo, ushirikiano wa abiria kusaidia Polisi katika eneo hili bado ni

mdogo sana. Serikali inategemea kupungua kwa kiasi kikubwa tatizo la abiria kujazwa kupita kiasi kwenye mabasi ya daladala mara utakapoanza utaratibu wa kutumia mabasi makubwa katika Jiji la Dar es Salaam *(Bus Rapid Transit).* Chini ya utaratibu huo, mabasi ya daladala yatawachukua abiria kwenye maeneo wanakoishi hadi katika vituo vya mabasi makubwa, ambayo ndiyo pekee yataruhusiwa kubeba abiria hadi maeneo ya katikati ya Jiji.

**MHE. ASHA ALI NGEDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Wananchi wengi wa Mkoa wa Dar es Salaam hutumia usafiri wa daladala hasa wale wenye kipato cha chini na pia hupata kero inayofanywa na madreva wa daladala na makondakta wao kwa kukatisha *route*, kwa mfano, basi linalokwenda Tandika - Posta linaishia Keko au Temeke - Muhimbili linaishia Shule ya Uhuru na kufanya walipe nauli mara mbili na kupoteza muda mwingi katika vituo na hufanyika nyakati za asubuhi wakati Wananchi hawa wanakwenda kufanya shughuli za ujenzi wa Taifa na wanafunzi kwenda shuleni: -

(a) Je, Waziri anaweza kutueleza ni sheria ipi inawapa uwezo wa kukatisha *routes* hizo?

(b) Ni sababu gani kubwa inayomfanya mwanafunzi asipovaa sare za shule hata akionyesha kitambulisho alipe nauli ya mtu mzima yaani Sh.150/=, kwani pengine anaenda hospitali kwa matibabu au anaenda *tuition* au anaenda *library* kijisomea? Ahsante.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, hakuna sheria hata moja inayoruhusu madreva wa daladala kukatiza *route* zao walizopangiwa na hii ndiyo maana kama wote tunavyosikia na tunavyoona, juhudi za Mamlaka ya Leseni ya Mkoa wa Dar es Salaam, hasa Mwenyekiti wake, anavyolifuatilia sana suala hili la madaladala kukatiza *routes* zao na kuwachukulia hatua.

Kuhusu mwanafunzi asiyevaa sare au wanafunzi wasiovaa sare kwamba wao wanalazimika kulipa nauli ya mtu mzima, sababu ya kwanza ni kwamba, ile nusu nauli imekusudiwa kwa mwanafunzi kumrahisishia kwenda shule na kurejea nyumbani akitoka shule. Sababu ya pili ni kwamba, kama hayuko kwenye sare si rahisi dreva au kondakta kujua kama kweli huyu ni mwanafunzi au ni kijana tu anajaribu kupata nusu nauli.

**MHE. MWAKA ABRAHMAN RAMADHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Naomba Mheshimiwa Waziri anifahamishe ya kuwa kuna sheria gani inayowapa haki Askari kutolipa nauli wanapopanda daladala wakati ukizingatia kwamba wanafunzi pia wanalipa nauli katika daladala? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, hakuna sheria ambayo inawaruhusu Polisi kupanda mabasi ya abiria bila ya kulipa nauli na ndiyo maana utaratibu huu huwa unafanywa kwa maelewano na pale ambapo maelewano yanapokuwa hayapo, mara nyingine hutolewa maelekezo kwamba, Askari Polisi walipe

nauli. Lakini hii mara nyingine hata madreva wenyewe kwa kurahisisha kazi zao na wao wanaona ni busara kuwasafirisha Polisi bila kulipa nauli.

Na. 109

**Gharama za Ujenzi wa Kibanda cha Mapokezi**
**Ofisi ya Uhamiaji Zanzibar**

**MHE. RAMADHANI NYONJE PANDU** aliuliza: -

Kwa kuwa ujenzi wa kibanda cha mapokezi ya wageni *(Reception)* kilichojengwa mbele ya Ofisi Kuu ya Idara ya Uhamiaji Zanzibar pamoja na ukarabati wa Ofisi ya Uhamiaji ya Mwanakwerekwe vimefanywa kwa lengo la kuondoa kero, usumbufu na msongamano wa wageni uliokuwepo kabla na kurahisisha huduma nzuri kwa wageni. Kwa kuzingatia uzuri wa majengo hayo, je, Serikali inaweza kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba ni kiasi gani cha fedha kilichotumika kwa ujenzi wa kibanda hicho cha mapokezi ya wageni pamoja na gharama zilizotumika kwenye ukarabati wa Ofisi hiyo ya Idara Kuu ya Uhamiaji ya Mwanakwerekwe?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Uhamiaji duniani pote ni kioo kinachoonyesha sura ya nchi husika kwa wageni kutoka nchi za nje. Hivyo, ni azma ya Serikali kuboresha Ofisi za Idara ya Uhamiaji nchini kote ili ziweze kuonyesha sura nzuri ya nchi yetu, kutoa huduma nzuri na kuondoa kero kwa wateja wa ndani na nje ya nchi. Azma hii ya Serikali inafanyika kwa awamu kwa kadri Serikali inavyopata fedha.

Katika kutekeleza azma hiyo huko Zanzibar, Serikali imejenga kibanda cha mapokezi ya wageni mbele ya Ofisi Kuu ya Idara ya Uhamiaji. Ujenzi huo ambao ulijumuisha pia ukarabati wa duka la Uhamiaji na kuweka sakafu ya vigae katika eneo la uwanja wa mbele wa ofisi uligharimu Sh.13,650,000/=. Aidha, Ofisi ya Uhamiaji ya Mwanakwerekwe imefanyiwa ukarabati mkubwa, imefanyiwa upanuzi na kujengewa uzio. Shughuli zote hizi zimefanywa kwa gharama ya Sh.35,250,000/=.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kuwa, Ofisi za Uhamiaji ni kioo cha wageni ili kuvutia au kuona hali halisi ya nchi. Je, kioo hiki ni kujiangalia tu bila ya usafiri au vifaa vingine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hakusikia, hebu rudia swali lako.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nauliza hivi. Mheshimiwa Waziri alisema kuwa, Ofisi za Uhamiaji ni kioo cha wageni, lakini matatizo

makubwa ya ofisi zetu ni kwamba zinakabiliwa na uhaba wa vifaa na usafiri. Je, katika suala hili haoni kuwa lizingatiwe zaidi ili hicho kioo kiwe kinapendeza zaidi? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba, vifaa pamoja na usafiri ni miongoni mwa mambo yanayopamba hizo huduma na sura na hicho kioo ambacho tunakitaka kiwe kwa Idara zetu za Uhamiaji.

Nadhani Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, atakubaliana nami kwamba, kabla hatujafanya matengenezo ya hicho kibanda hali haikuwa nzuri, lakini baada ya kuona vile tumefanya hayo matengenezo na hii inakwenda na hizo huduma nyingine. Magari yetu kwa sasa hivi bado kweli si mazuri, lakini utaratibu wa kutafuta mazuri zaidi unaendelea.

Na. 110

**Barabara ya Tunduma - Sumbawanga**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza: -

Kwa kuwa pamoja na juhudi kubwa ya Serikali kuanza ujenzi wa madaraja yote muhimu kutoka Tunduma hadi Sumbawanga ikiwa ni hatua ya awali ya kuiwekea lami barabara hiyo: -

(a) Je, kwa nini Serikali isingeanza kuweka lami eneo ambalo halina hata daraja moja kuanzia Tunduma hadi Luasho?

(b) Kwa kuwa madaraja yalitakiwa kuwa yamekamilika kufikia mwishoni mwa Desemba, 2003, lakini haikuwezekana, je, kuchelewa huko hakutaathiri ratiba ya kuanza kuiwekea lami barabara hiyo?

(c) Kwa kuwa barabara hiyo sasa inatumika na magari mengi na makubwa yenye uzito wa zaidi ya tani 40 hadi 50, je, isingekuwa busara kuanza kuweka mizani ili isiharibike haraka?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Jimbo la Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya barabara unafuata taratibu za msingi ambazo ni upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na hatimaye ujenzi. Hatua ya upembuzi yakinifu imekamilika na kutumwa Benki ya Dunia tangu Machi, 2004. Kwa vile upembuzi yakinifu umefanyika wakati madaraja mapya yanajengwa, hivyo umezingatia punguzo la gharama za mradi zitakazohitajika kujenga lami hapo baadaye. Mara Benki ya Dunia itakapopitisha ripoti ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina utafuata katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 na kufuatiwa na ujenzi kwa kiwango cha

lami. Taratibu hizo nilizozitaja hapo juu, haziwezi kukiukwa chini ya masharti ya mikopo au misaada kukoka kwa wafadhili, hivyo Serikali haiwezi kuanza kujenga kwa kiwango cha lami kati ya Tunduma na Luasho kabla usanifu haujakamilika.

(b) Mheshimiwa Spika, mradi wa madaraja ambao ulitakiwa kukamilika Desemba, 2003 umechelewa kwa muda wa miezi mitatu na hatimaye umekamilika Machi, 2004.

Kama nilivyokwishaeleza kupitia jibu la sehemu (a) hapo juu, ucheleweshaji huu wa madaraja hautaathiri ratiba ya kuanza kuiwekea lami barabara hiyo.

(c) Mheshimiwa Spika, ili kulinda uwekezaji wa madaraja mapya yaliyojengwa na mradi ujao wa ujenzi kwa kiwango cha lami, mzani mpya utajengwa sambamba na utekelezaji wa mradi wa barabara ya lami.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini pia nataka nitumie nafasi hii kuishukuru Serikali yetu kwa kujenga madaraja kama ilivyokuwa imeahidi katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

(a) Je, Waziri atakubaliana nami kuwa kwa heshima ya Wananchi wa Mkoa wa Rukwa ingekuwa ni wakati muafaka kumwomba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa akaja rasmi katika Mkoa wetu wa Rukwa ili kuzindua haya madaraja ambayo imekuwa ni moja ya ahadi zake?

(b) Je, waziri anakumbuka kwamba Benki ya Dunia imekwishatamka na imekwishatoa vigezo kwamba Shilingi bilioni 35 zimetengwa kwa ajili ya kuwekwa lami kutoka Tunduma mpaka Sumbawanga na kwamba fedha hizo ni sehemu ya Shilingi bilioni 180 zilizotengwa katika barabara za Tanzania na kwamba fedha hizi zinatakiwa zitumike haraka iwezekanavyo ili zisije zikachacha na kuhamishiwa katika miradi mingine? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza, linapitia tu kwangu, mimi sina mamlaka ya kumwomba Mheshimiwa Rais aje huko rasmi. Hili nitamwomba Mkuu wa Mkoa wa Rukwa. Mkuu wa Mkoa wa Rukwa yeye atamwomba rasmi Mheshimiwa Rais afike kule.

Pili, ninafahamu kwamba, hizo fedha zimetengwa, lakini zimetengwa pamoja na masharti haya ambayo nimeyatamka hapa kwamba ni lazima watoe *no objection* kwa usanifu ndiyo watoe pesa hizo kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami na tayari tumekwishawapelekea upembuzi yakinifu kwa hiyo na wao wanajua kwamba kuna pesa zao ambazo wamekwishaziahidi huku, ninaamini watatoa hiyo *no objection* haraka ili tutumie hizo pesa.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imetusaidia sana kujenga madaraja mazuri hadi kufika Kijiji cha Mpuwi na yamebakia madaraja machache kutoka katika Kijiji cha Mpuwi hadi kufika Sumbawanga. Je, Serikali inaweza ikatufahamisha ina mpango gani hasa wa kuhakikisha kwamba yale madaraja mengine nayo yanajengwa kabla lami haijaanza kujengwa kufika Sumbawanga?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba, madaraja yale 11 yameishia Kijiji cha Mpuwi na yapo madaraja mengine mbele, lakini vile vile katika ombi la kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami, tumeongeza na madaraja hayo kama tutakubalika. Tukikubalika tutajenga madaraja hayo na tutajenga na lami moja kwa moja.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa barabara ya kutoka Tunduma mpaka Sumbawanga ni barabara moja na wakati ule mazungumzo yalikuwa kwamba ijengwe kwa awamu na kwa kuwa bei kila wakati zinaongezeka: -

(a) Je, Wizara haioni kwamba ingekuwa ni jambo zuri utekelezaji wa barabara hii yote ukawa ni wa awamu moja?

(c) Kwa nini ujengaji wa barabara ya lami uanzie Tunduma kwenda Sumbawanga badala ya kutoka Sumbawanga kwenda Tunduma?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa kwamba, barabara ya kutoka Tunduma mpaka Sumbawanga ni ndefu na ingestahili kujengwa kwa awamu na ilipangwa ijengwe kwa awamu. Lakini waliokuwa wanatoa pesa za kujenga kwa awamu tukianzia kilomita 50 za mwanzo kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga ni *Kuwait Fund.* Sasa, hao hao *Kuwait Fund* wameamua tuombe pesa za barabara nzima ili waamue kutuletea pesa za barabara nzima.

Kuhusu kwamba barabara hii ijengwe kuanzia Sumbawanga badala ya kuanza Tunduma, *Kuwait Fund* wana sababu zao za msingi wanasema pale ambapo lami ipo ni vizuri kuiunganisha ukianzia hapo badala ya kubeba mitambo kwenda kuanzia mwisho ukaja huku. Kwa hiyo, wao wameamua kwamba wataanzia Tunduma.

Na. 111

**Upembuzi Yakinifu kwa Barabara ya Mtwara - *Mbamba Bay***

**MHE. ABDULA S. LUTAVI** aliuliza: -

Kwa kuwa wakati wa kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka 2003/2004, Serikali ililieleza Bunge kwamba suala la barabara ya Mtwara -

*Mbamba Bay* lingojee upembuzi yakinifu uliokuwa ukiendelea ili kubaini kama barabara hiyo ingekihusisha kipande cha barabara cha Mtwara - Tandahimba - Newala - Masasi; na kwa kuwa katika Mkutano wa Bunge wa 14 Serikali ililiarifu Bunge kwamba upembuzi yakinifu uliokuwa ukifanywa umekamilika; je, kwa mujibu wa matokeo hayo, barabara husika sasa itapita wapi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdula Suleiman Lutavi, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, upembuzi yakinifu uliokuwa ukifanywa kwenye barabara hii umekamilika kama nilivyosema katika Mkutano wa Bunge wa 14. Aidha, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, upembuzi yakinifu umetoa matokeo kwamba, barabara itapitia kwenye mwelekeo wa sasa wa barabara ya kutoka Mtwara - Mingoyo - Nanganga - Masasi ambayo ni sehemu yenye lami na Masasi - Tunduru - Songea hadi *Mbamba Bay.*

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdula Suleiman Lutavi, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, matokeo hayo ya upembezi yakinifu yalizingatia barabara iliyolengwa kufanyiwa upembuzi yakinifu ni ile ya Mtwara - Mingoyo - Masasi - Tunduru - Songea hadi *Mbamba Bay,* sehemu ya Mtwara - Mingoyo - Nanganga - Masasi (km. 205) tayari ina lami hivyo itahitaji matengenezo yenye gharama nafuu kuliko kujenga barabara mpya kati ya Mtwara - Tandahimba - Newala - Masasi (km. 211) na sehemu ya mchepuo wa barabara *(diversion)* ya kufuata tuta la reli kuanzia Nyangao - Mahiwa (Mtama) - Nanganga yenye urefu wa km. 23 nayo ilionekana ni ya gharama kubwa kuijenga kuliko kuinua tuta na kuweka makalvati makubwa kwenye sehemu ya Chipite.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara *(TANROAD)* Mkoa wa Mtwara, inaendelea kuifanyia matengenezo barabara ya Mtwara - Tandahimba - Newala hadi Masasi (km. 211), ili iendelee kupitika hadi hapo tutakapopata uwezo wa kifedha wa kujenga kwa kiwango cha lami.

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu haya ya Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi binafsi nimekata tamaa. Lakini ningelipenda niulize maswali mafupi mawili kama ifuatavyo:-

Moja ni kwamba, kwa vile swali hili linalojibiwa leo, linatokana na maelezo ya awali ya Wizara hii kwamba, tusubiri matokeo ya upembuzi yakinifu. Sasa swali langu ni kwamba, hivi ni kweli mtaalam ambaye tulimpa kazi hii ya kufanya upembuzi yakinifu alipewa na maelekezo hayo ya kusema akaangalie uwezekano wa barabara hii kupita kwenye barabara ile ya Tandahimba, Newala, kufika Masasi? Kama alipewa hivi vigezo hivi tukumbushie pale, lakini nataka kujua tu kwamba ni kweli aliambiwa hivyo?

Lakini pili, naomba kuuliza kwamba, sasa kama hali ni hii, Serikali hii inawaambia nini Wananchi wa maeneo ambayo barabara hii mnayoitaja inapita, maeneo ya Mtwara Vijijini, Tandahimba na Newala ambao kwa muda mrefu sasa dhana nzima hii ya *Corridor* na ujenzi wa barabara ilikuwa imeshawajengea matumaini kuwa ndiyo fursa pekee ya barabara hii tunayoitaja kupata kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Lutavi, kwa jinsi alivyofuatilia kwa karibu sana juu ya upembuzi yakinifu wa barabara hii. Lakini ni bahati mbaya kwamba, matumaini yake hayakufanana na maamuzi ya mtaalam ambaye alifanya upembezi yakinifu. Ningemwomba Mheshimiwa Mbunge, asikate tamaa katika kufuatilia suala hili. Ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, maelekezo aliyopewa mtaalam ni maelezo ya uhuru kabisa, kwamba atuambie sisi Wizara ya Ujenzi, pamoja na *Kuwait Bank* barabara hii ingefaa ipite wapi kufika *Mbamba Bay* na yeye amefanya kazi yake kwa kuiridhisha *Kuwait Fund* ili waweze kutoa fedha kwa uhakika bila maswali mengi na ndiyo maana tuna imani kwamba, sasa tutafanya upembuzi yakinifu kwa sababu *Kuwait Fund* wameipokea taarifa hii kwa furaha kwamba imepunguza gharama. *(Makofi)*

Swali lingine limeulizwa kuwa Serikali inawaambia nini wananchi? Serikali imeshawaambia hapa kwamba, *Kuwait Fund* waligharamia mtalaam kufanya upembezi yakinifu na wamekwishafanya, sasa nimetamka hapa mwisho, Serikali kupitia Wakala wa Barabara *(TANROAD)* Mkoa wa Mtwara, inaendelea kuifanyia matengenezo barabara ya Mtwara, Tandahimba, Newala hadi Masasi km, 211 ili iendelee kupitika na mpaka hapo tutakapopata uwezo wa kifedha tutaijenga kwa lami. Hilo ndiyo tamko la Serikali. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri kuhusu utengenezaji barabara kwa lami kwa sehemu ya Mtwara, Mingoyo, Mtama, Masasi, ningependa kumwuliza swali kama ifuatavyo: Kwa kuwa mpango huu utakuwa ni wa muda mrefu na hivi sasa kwa bahati mbaya, sehemu hiyo aliyoitaja kati ya Nyangao na Nanganga katika eneo la Chipite vimeharibiwa sana na mvua na kufanya pasipitike. Sasa je, Wizara inawaeleza nini wananchi wa maeneo yale kuhusu utengenezaji kwa muda mfupi wa eneo hili la Chipite ili liweze kupitika kabla ya uchaguzi wa mwaka 2005? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru amekubali kwamba, mpango huu ni wa muda mrefu, lakini kabla hatujatoa *tender* kwa ujenzi wa barabara hii, wajibu wa kutengeneza barabara hii bado uko mikononi mwa Wizara ya Ujenzi na kwa mantiki hiyo, uko mikononi wa *TANROAD.* Sehemu ya Nyangao, Chipite ambayo imeharibika ni sehemu mojawapo tu katika nchi hii ambayo sasa hivi zimeharibika sana kwa sababu ya mvua zinazonyesha. Kwa hiyo, tutaangalia uwezekano wa kuzifungua sehemu hizo zote ambazo zimeharibiwa sana na Mvua ili barabara hizi ziweze kupitika na siyo mwaka 2005 kabla ya mwisho wa mwaka huu. *(Makofi)*

Na. 112

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Mwanza**

**MHE. STEPHEN M. KAZI** aliuliza: -

Kwa kuwa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza kiko katika mipango ya kujengwa kufikia Kiwango cha Kimataifa. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi huo na unategemewa kukamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Masaba Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu na mchango wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza katika kuboresha na kuinua uchumi wa Taifa na wananchi wa Mwanza kwa ujumla, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Nchini, imekuwa na mipango ya muda mrefu na ya muda wa kati katika kukijenga kiwanja hiki kufikia hadhi ya Kimataifa. Ili kufikisha malengo hayo, tunafanya mambo yafuatayo kwa awamu ili kukamilisha ujenzi wa kiwanja hicho:-

- Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeshakamilisha upembuzi yakinifu na kuandaa *Master Plan* ambayo ni dira ya uendelezaji wa kiwanja hiki kwa miaka ishirini ijayo hadi kufikia 2022; na

- Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeshakamilisha usanifu wa miundombinu na majengo yale muhimu ya kiwanja. Kazi ya usanifu wa maegesho na viungio imegharimu Shilingi milioni 22.8.

Kwa upande mwingine kazi ya usanifu wa majengo ya kisasa ya abiria, jengo la mizigo na *hangar* imegharimu Shilingi milioni 185. Gharama ya ujenzi wa majengo na miundo mbinu yote inakadiriwa kuta Shilingi bilioni 8.1. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 4.1 ni kwa ajili ya majengo na Shilingi bilioni 4.0 ni kwa ajili ya maegesho na viungio.

Mheshimiwa Spika, kutokana na gharama ya ujenzi kuwa kubwa, Wizara yangu imekuwa ikitafuta fedha toka kwa wafadhili mbalimbali ili kukamilisha mradi huu muhimu na pale inapowezekana kutumia mfuko wa ndani katika kutekeleza baadhi ya miradi. Wizara yangu imekwishawasilisha maombi kwa ajili ya mkopo wenye riba nafuu wa dola za Kimarekani milioni 6.5 kwenye Benki ya Uwekezaji ya Ulaya *(European Investment Bank - EIB).* Maombi haya yamefanywa kupitia Wizara ya Fedha na bado tunasubiri majibu toka Benki hiyo. Fedha nyingine kiasi cha Shilingi 8.1 bilioni zinaendelea kutafutwa kutoka kwa wafadhili mbalimbali. Kupitia mpango wa ushirikishaji sekta binafsi kuwekeza katika viwanja vya ndege, tayari Makampuni kadhaa

yameonyesha nia ya kuwekeza katika jengo la mizigo na jengo la kutengenezea ndege *(hangar)*. Utaratibu mzima bado unaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, mbali na mipango ya muda wa kati na muda mrefu, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, inaendelea na ukarabati wa miundombinu, kuimarisha usalama wa kiwanja kutoka Bajeti ya ndani ya mamlaka, kama vile ujenzi wa uzio, awamu ya kwanza ambapo ni km. 10 unagharimu Shilingi 189 milioni na ununuzi wa *X-ray machine* ambao pia unagharimu Shilingi milioni 80, unaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Mbunge, kwa juhudi zake za karibu katika kuangalia shughuli hizi za wapiga kura wake na namhakikishia kwamba, Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, itaendelea kushirikiana naye. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri na pia juhudi za Wizara kama zilivyoelezwa, mimi kwa kweli nawapa pongezi kubwa na ninawatakia heri kwamba kazi hii ifanikiwe. Pia nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba ifahamike kwamba Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, kimezungukwa na viwanja jirani kama vitatu ambavyo ni vya Kimataifa na ni vikubwa kama cha Entebe, Kigali na Bujumbura, ambavyo vinainyang'anya Mwanza biashara. Kwa hiyo, Kitaifa tunapoteza fedha na abiria kutokana na ule uzuri wa vile viwanja, hizo ndege hazitui Mwanza. Sasa kwenye utekelezaji wa haraka, je, Wizara inasemaje kama ilivyofanya shughuli za kujenga Kiwanja cha Arusha iweze kuchukua hatua za haraka namna kujenga Kiwanja cha Mwanza? *(Makofi)*

Swali la pili, linahusiana na msongamano mkubwa katika kiwanja chenyewe ambao ni mkubwa, *actually* hali ya mahitaji ni *demand pushed* kwa mfano, ndege tatu za *Boeing* zinatua pale kila siku asubuhi na kuondoka na ndege zingine ndogo ndogo zinatua pale.

**SPIKA:** Hebu punguza maelezo uliza swali.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, sasa ningependa kufahamu kwamba, katika hili pamoja na maelezo yaliyotolewa, Wizara inachukua hatua gani na itaanza na eneo lipi kwanza ili kutunasua kwenye msukumano na msongamano tulionao katika Kiwanja cha Mwanza? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Kiwanja cha Mwanza kinazungukwa na viwanja vitatu vya nchi jirani vya Entebe, Kigali na Bujumbura. Kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba, juhudi zinafanywa kukiboresha Kiwanja cha Ndege cha Mwanza na kama atakubaliana nami, Mheshimiwa Mbunge, ataamini kwamba, *runway* tuliyokuwa nayo wakati ule siyo tuliyonayo hivi sasa, ni *runway* ambayo inasifika kwa nchi zote za *East Africa* na ni madhubuti zaidi kuliko zote.

Mheshimiwa Spika, msongomano huu wa ndege nakubaliana nao upo na nilipata nafasi hivi karibuni ya kufuatana na Mheshimiwa Mbunge kwenda Kwanja cha Mwanza, tulijadiliana na tukakubaliana. Ninamuahidi kwamba, yale tuliyokubaliana tutaendelea kuyatekeleza. *(Makofi)*

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza kinafanana sana na Kiwanja cha Ndege cha Wawi Pemba na kwa kuwa SMZ wakati huu haina uwezo wa kutengeneza kiwanja kile kufikia kiwango cha kimataifa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, ana mpango gani wa kuisaidia SMZ ili kukiendeleza kiwanja kile kifikie Kiwango cha Kimataifa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa kuwa viwanja vinafanana na majibu yake yanafanana. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Kiwanja cha Ndege cha Wawi Pemba, mimi nasema kinahitaji kuongezwa urefu, lakini kwa umadhubuti kiko katika hali inayofaa. Labda nimkumbushe Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid kwamba, mapato yanayotokana na maegesho ya ndege na mengine, ndiyo yanayosaidia kujenga viwanja vya ndege na kwa bahati nzuri mapato yanayoingia kule yanaingia kwenye Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Tutaendelea kusaidiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kuona masuala haya yanatekelezwa. *(Makofi)*

Na. 113

**Usafiri Katika Visiwa vya Jimbo la Muleba Kaskazini**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa Ziwa Victoria ni pana sana na lina visiwa vingi vinavyokaliwa na watu wanaojishughulisha na uvuvi, ukulima, biashara na ufugaji; na kwa kuwa Visiwa vya Bumbile na Goziba katika Jimbo la Muleba Kaskani, vinakisiwa kuwa na watu wapato 15,200; na kwa kuwa eneo hili ni zuri linaweza kufaa kwa utalii na uwekezaji lakini hakuna usafiri unaoaminika kati yake na nchi kavu:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka usafiri wa meli kati ya nchi kavu na visiwa na kati ya visiwa na visiwa ili wananchi waweze kufaidika na mali na mazingira mazuri ya visiwa hivyo?

(b) Je, kufuatia kilio cha muda mrefu cha Wabunge wa Kanda ya Ziwa kuhusu usafiri wa meli katika Ziwa Victoria kuboreshwa, Serikali imefikia hatua gani na inatoa kauli gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli Wilaya ya Muleba ina visiwa vingi ambavyo havifikiwi kwa urahisi kwa kutumia meli zenye usalama wa kutosha kwa abiria na mizigo. Visiwa hivyo ni pamoja na Bumbile, Iroba, Maihega, Iramba, Kitua na Nyaburu. Kusini mwa mkusanyiko wa visiwa hivi kuna Visiwa vya Mazinga, Kivumba, Runenke na Majeje, ambavyo pia havifikiwi kwa urahisi kwa sababu ya kutokuwa na meli za kuaminika na ambazo ni salama. Visiwa hivi kwa sasa vinahudumiwa kwa kutumia mitumbwi mikubwa yenye injini pamoja na madau, usafiri ambao kwa ujumla si salama inapotokea kuwa kuna dhoruba kali katika ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera ya Serikali hivi sasa ni kujitoa katika shughuli za kibiashara na kuachia sekta binafsi. Hivyo, Wizara yangu inawahamasisha watu binafsi au wawekezaji ili walete vyombo vilivyo salama katika maziwa ikiwa ni pamoja na visiwa vilivyo katika Wilaya ya Muleba. Vile vile, Wizara yangu inaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji katika usafiri wa majini ili kuwavutia wawekezaji wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe wito kwa Mheshimiwa Mbunge wa Muleba, pamoja na Serikali ya Halmashauri ya Wilaya ya Muleba kuwa, tushirikiane kwa pamoja kutafuta wawekezaji ili wasaidie kuchangia uboreshaji wa usafiri wa majini katika Wilaya ya Muleba.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kuboresha usafiri wa meli katika Ziwa Victoria, Serikali imekuwa ikifanya mambo yafuatayo:-

(i) Kuendelea na maandalizi ya kubinafsisha kampuni ya huduma za meli kwa lengo la kupata wawekezaji wenye uwezo mkubwa;

(ii) Kuendelea kuhamasisha watu binafsi kuwekeza katika usafiri wa majini katika Ziwa Victoria. Mpaka sasa kuna jumla ya meli 14 za watu binafsi ambazo zinatoa huduma katika visiwa vilivyoko Kusini Magharibi ya Ziwa Victoria, pamoja na nchi ya Kenya. Meli hizi zinatoa huduma kutokea Mwanza. Tunawaomba wawekezaji wajenge meli ili kuhudumia visiwa vilivyoko katika Mkoa wa Kagera;

(iii) Aidha, Wizara yangu inaendelea kuhamasisha watu binafsi kuwekeza katika meli za mwendo kasi ili kutoa huduma kwa wasafiri kati ya Mwanza na Bukoba na Mwanza na *Port Bell* (Uganda), ambapo kwa sasa hivi wasafiri wanaotoka Mwanza kwenda *Port Bell* wanalazimika kupitia Bukoba na Mtukula au Nairobi ili waweze kufikia Uganda. Mpaka sasa yako makampuni machache yaliyoonyesha nia ya kuwekeza na mojawapo ni ile ijulikanayo kama *Speka Shipping Line Ltd.,* ambayo imeonyesha nia thabiti ya kuleta meli iendayo kwa kasi aina ya *Catamaran* itakayotoa huduma kati ya Mwanza na Bukoba. Meli hiyo itaundiwa Mwanza na itakapokamilika itakuwa na uwezo

wa kubeba abiria 490 na mizigo tani 350 yakiwemo magari. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa mradi huo kwa wananchi, Serikali tayari imepata nafasi ya kuunganisha meli hiyo kwenye karakana za Kampuni ya huduma za Meli mara itakapofika Mwanza.

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru Mheshimiwa Ruth Msafiri, kwa kushirikiana na wananchi wake kufuatilia masuala yanayowakera wananchi wake kwa karibu zaidi. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Lakini kwa ruhusa kabla sijauliza swali nilikuwa naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa kifo cha ghafla cha Mtendaji wa Kata ya Bumbile, aliyefariki wiki iliyopita. Ninaomba sasa niulize maswali yangu kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba inaelekea kujitoa katika huduma za jamii isipokuwa inahamasisha wawekezaji binafsi na Wilaya ya Muleba inahamasishwa kushirikiana na Serikali. Nilikuwa naomba basi kuiomba Serikali kwamba wawekezaji watakapofika watahitaji kuzikuta *gate* zinazowezesha meli kuegeshwa pale, kwa hiyo, naiomba Serikali inieleze ina mpango gani wa kuboresha *Gates* za Kyamkwikwi, Amshenye na Kelebe, ambazo zipo katika Visiwa vya Goziba, Kerebe na Bumbile?

Mheshimiwa Spika, vile vile swali la pili, katika swali la msingi nimeonyesha kwamba, wananchi wanajishughulisha sana na shughuli mbalimbali, lakini shughuli ya uvuvi ni shughuli ambayo ni kubwa sana na inawapatia kipato wananchi wengi lakini haiendelezwi ipasavyo kwa sababu ya kukosekana kwa uwezo wa wananchi.

Je, Serikali itasaidia vipi wananchi wa visiwa hivi kwa kuviimarisha ili kuwasaidia wawekezaji na kuwasaidia watu mbalimbali na wavuvi wa kawaida kujiimarisha katika uvuvi ili waimarishe kipato chao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, napenda nijibu swali moja la nyongeza, nafikiri la pili Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii labda atakuwa tayari kulijibu.

**SPIKA:** Siku nyingine.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, juhudi zinafanywa na Wizara yangu katika kuweka hali ya *gates* zetu katika nchi katika nafasi inayofaa. Kama atakubaliana nami, kipindi cha kilichopita tulikuwa hatupati hata senti tano ya kuendeleza ma-*gate*. Bunge lililopita nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, mlitusaidia kupata hela kidogo kwa ajili ya *Gate* la Bukondo, *Gate* la Shirati, *Gate* la Nansio na Kinesi na *Mbamba Bay.* Haya yalikuwa ni *feasibility study* tu ndogo ndogo kwa sababu hela ambayo tuliipata haikuwa nyingi. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, fedha itakapopatikana, hamu yetu ni kuona kwamba angalau tunakuwa na ma-*gate* yanayoaminika katika maziwa yetu na wawekezaji waweze kuwekeza kwa njia muafaka. *(Makofi)*

Na. 114

## Mpango wa *NARLEP* na Ufugaji

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI (k.n.y. MHE. GWASSA A. SEBABILI)** aliuliza:-

Kwa kuwa ni dhahiri kwamba mpango wa *NALERP* ulileta hasara badala ya faida katika sekta ya mifugo wakati ulipokuwa ukitekelezwa na kwa kuwa watumishi wengi waliacha kazi, mafunzo kazini yakatoweka, watalaamu wakati wa sekta ya mifugo walielekezwa kwenye sekta ya kilimo na wale wa kilimo wakapelekwa mifugo, lakini jambo baya zaidi ni kwamba watumishi vijijini walinyang'anywa vifaa na vyombo vya kazi kama vile vya kuhasi madume, kuunguzia mapembe, kukatia kwato, mabomba na kadhalika na matokeo yake sasa ni ufugaji usio wa kitalaam/kisayansi, mifugo mingi inaendelea kufa na wafugaji hawajui la kufanya kwa sababu ya kukosa watalaam, madawa na vifaa mbalimbali vimetoweka moja kwa moja:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kusahihisha hali hiyo mbaya na inayokatisha tamaa haraka iwezekanavyo?

(b) Je, Serikali inaandaa utaratibu gani sasa kwa kuinua sekta hiyo ya ufugaji kama ule wa Wizara ya Kilimo na Chakula wa kuwa na mfuko wa kuendeleza ufugaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** atajibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mbunge wa Ngara, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kutokana na huduma na ushauri kwa wakulima na wafugaji kuwa siyo za kuridhisha kati ya miaka ya 1970 hadi 1989, Serikali ilibuni Mradi wa Kuimarisha Huduma za Ushauri kwa Wakulima na Wafugaji *(National Agricultural and Livestock Extension Rehabilitation Project - NALERP).* Mradi huu ulitekelezwa katika Mikoa 16 ya Tanzania Bara isipokuwa Mikoa ya Mbeya, Iringa, Ruvuma na Rukwa, ambayo ilikuwa na mradi kama huo chini ya ufadhili wa *IFAD.* Mradi wa *NALERP* ulitekelezwa kwa gharama ya dola za Kimarekani milioni 28.6 kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulikuwa na lengo la kuboresha utaalam, miundombinu na vitendea kazi vya huduma ya ugani. Mtalaamu mmoja aliweza kutoa huduma na ushauri wa kilimo na mifugo kwa pamoja ili kurahisisha utoaji wa huduma hiyo kwa wananchi walio kwenye eneo lake.

Katika kutekeleza mradi huu, jumla ya magari 169, pikipiki 896 na baiskeli 9,483, zilinunuliwa. Pia vifaa mbalimbali vya kuhudumia mifugo *(Extension Kits),* kama vile sindano na mabomba yake, majokofu ya kutunzia madawa, vifaa vya kuhasi madume, kung'oa na kuchoma pembe, kukata kwato, darubini na kadhalika vilinunuliwa na

kusambazwa. Aidha, mradi ulijenga jumla ya nyumba 160 za kuishi watalaam wa ugani vijijini. Jumla ya watalaam 1,446 wa sekta ya mifugo walipatiwa mafunzo rejea na wengine 16 walipata mafunzo katika ngazi ya Shahada ya kwanza na Shahada ya Uzamili. Baada ya mradi kuisha, vifaa na vyenzo mbalimbali vilikabidhiwa Halmashauri za Wilaya ili viendelee kutumiwa na watalaam hao.

Hivyo, siyo kweli kwamba, Mradi wa *NALERP* haukuleta faida. Kupitia mradi huu, wafugaji waliweza kufundishwa mbinu mbalimbali za ufugaji bora, utunzaji bora wa mifugo, kukinga mifugo yao dhidi ya magonjwa na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wataendelea kupata mafunzo ya namna hiyo kupitia mpango wa *Agriculture Sector Development Pragramme,* ambao umeanzishwa hivi karibuni na unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Miji. Mpango huu unazingatia sana dhana ya ushirikishi wa wafugaji. Ili kuendeleza Sekta ya Mifugo, Serikali imeanzisha Mfuko wa *Livestock Development Fund,* ambao una lengo la kusaidia sekta kutekeleza malengo yake mbalimbali.

Halmashauri ya Wilaya na Miji nazo zimeagizwa kutenga si chini ya asilimia 15 ya mapato yatokanayo na mifugo ili kuanzisha Mifuko ya Mifugo katika Halmashauri. Naamini nia hizi mbili za mifuko zitasaidia sana kuendeleza mifugo nchini.

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru Naibu Waziri amejibu swali vizuri. Nina swali moja tu kama ifuatavyo: Wakati *NALERP* inatekelezwa kukawa na sera tena ya kuwahamisha watu wa *extention* toka mikoani kwenda katika Wilaya, lakini walihama watu na mishahara yao na sehemu kubwa hawakuhama na vitendea kazi hasa magari pamoja na mafuta yake. Kwa hiyo, je, Serikali itafikiriaje kuoanisha kazi pamoja na vitendea kazi vya watumishi hawa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, baada ya muundo wa Serikali kubadilika, wafanyakazi ambao nimewaeleza kwenye jibu langu la msingi, walihamishiwa Tawala za Mikoa na hivyo ni wafanyakazi katika Halmashauri za Wilaya na Miji. Kwa hiyo, mipango yote ya jinsi gani wafanye kazi na jinsi gani watatue matatizo ya wafugaji, inapangwa kwanza na Wilaya halafu Wizara yangu inashirikiana nao kwa karibu ili kutekeleza majukumu ambayo wanakuwa wamejiwekea. Kwa hiyo, katika kutatua matatizo ambayo tumeyaeleza chini ya mpango wa *Agriculture Sector Development Program,* tunawashirikisha moja kwa moja ili kuona kwamba unakuwa na manufaa kwa wafugaji kupitia Halmashauri za Wilaya.

Na. 115

**Serikali Kuwalipia Ada - *Medical Students***

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeamua kuwalipia ada *Medical Students* kwa kuanzia na wale wanaoanza masomo hayo. Je, isingekuwa vyema Serikali ikawalipia wanafunzi wote hata wale ambao wamekwishaanza kuliko kuwabagua?

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimira Dr. Thadeus Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uwiano wa wataalam wa tiba na wananchi Tanzania ni mdogo sana ukilinganisha na nchi zingine kusini mwa Sahara, mfano uwiano huu nchini Kenya ni mtaala mmoja kwa wananchi 7,000, nchini Uganda ni mtaala mmoja kwa wananchi 9,000, wakati Tanzania bado imebakia mtaala mmoja kwa wananchi 23,0000, uwiano unaopendekezwa na Shirika la Afya Duniani ni mtaala mmoja kwa wananchi 10,000. Serikali imechukua hatua kadhaa kwa lengo la kuongeza idadi ya madaktari nchini, kwa kutekeleza Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999. Katika kutekeleza Sera ya Elimu ya Juu, Serikali imeweza kupanua udahili katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili, ambacho ndiyo Chuo Kikuu pekee cha Umma kinachofundisha fani hii, kutoka wanafunzi wa udaktari 123 mwaka 1998/99 hadi 212 mwaka 2003/2004.

Aidha, Serikali imeweza kusimamia uanzishwaji wa vyuo vikuu binafsi, ambavyo pamoja na kutoa mafunzo mengine, vinatoa mafunzo ya udaktari. Vyuo Vikuu binafsi vinavyotoa mafunzo ya udaktari ni *Kilimanjaro Christian Medical College, Hubert Kairuki Memorial University, Bugando University College of Health Sciences* na *International Medical and Technological University.*

Mheshimiwa Spika, matatizo mbalimbali yamekuwa yakijitokeza ikiwa ni pamoja na wanafunzi hao kushindwa kuendelea na masomo kutokana na kushindwa kumudu gharama za masomo na hivyo kuchelewesha azma ya Serikali kujipatia madaktari kufikia uwiano ulipendekezwa na Shirika la Afya Duniani.

Ingawa Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999 imeweka utaratibu wa kuchangia gharama za elimu ya juu, sera inaruhusu Serikali kugharamia fani ya mafunzo ambayo ni nyeti ama muhimu. Kwa msingi huo, Serikali imeamua kulipia gharama za mafunzo ya madaktari katika vyuo vikuu binafsi kuanzia mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali kugharamia mafunzo ya wanafunzi wa udaktari wa mwaka wa kwanza wa 2003/2004, hauna lengo la kubagua wanafunzi wengine ambao wana udhamini binafsi katika fani ya udaktari, bali unatokana na sababu za kibajeti.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, ameridhika na muda wa maswali umekwisha. Kwa hiyo, tunaendelea na matangazo ya vikao kwa leo. Kamati mbili zimepangiwa kukutana, Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sophia Simba, anaomba Wajumbe wake wakutane leo kuanzia saa 5.00 chumba Na. 227.

Kamati ya pili ni ya Mambo ya Nchi za Nje, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. William Shija, anaomba Wajumbe wakutane saa 5.00 katika Chumba Na. 231 ghorofa ya pili. Mheshimiwa Paul Kimiti, jana nilimtangazia kikao cha wanachama wake, Wabunge wa masuala ya idadi ya watu na maendeleo, lakini hawakuweza kukutana jana, sasa ameniomba nitangaze kwamba, watakutana leo baada ya kuahirisha kipindi cha Bunge cha asubuhi saa 7.00 mchana humu humu ndani ya Ukumbi wa Bunge.

Mwisho wa matangazo, isipokuwa kwa faida ya Wabunge Vijana, ningependa kuwapa kumbukumbu kwamba, tarehe 22 Aprili, 1964 ndipo Waasisi wa Muungano, Marehemu Mwalimu Nyerere na Marehemu Mzee Karume, walipotia saini Mkataba wa Muungano katika Ikulu ya Zanzibar, siku kama ya leo. *(Makofi)*

Mwisho wa matangazo, Katibu tunaendelea na *Order Paper.*

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Madhara yanayotokana na Wanyamapori Dhidi ya Wananchi na Mali zao

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo yafuatayo kuhusu hoja binafsi ya Mheshimiwa Lydia Boma, Mbunge wa Viti Maluum, aliyoitoa tarehe 19 Februari, 2004 katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge, kuhusiana na madhara yanayotokana na wanyama wakali na waharibifu dhidi ya wananchi na mali zao.

Awali ya yote, nakubaliana na Mheshimiwa Boma kwamba, nchi yetu ni moja ya nchi chache duniani, iliyojaliwa kuwa na utajiri mkubwa wa raslimali ya wanyamapori wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wanyamapori waliopo hapa nchini ni raslimali ya Taifa na taratibu za uhifadhi wa wanyama ni tofauti na baadhi ya nchi nyingine za Afrika. Nchi yetu ina bahati ya kuendesha uhifadhi wa wanyamapori kwenye mazingira yao bila kuwawekea wigo *(fences).* Raslimali hii ni mali yetu sote na inatumiwa kwa faida ya Taifa hili. Wizara yangu imepewa dhamana kwa niaba ya Watanzania wote kusimamia Uhifadhi na matumizi endelevu ya raslimali hii. Hivyo, wanyamapori hawa ni muhimu wahifadhiwe na kulindwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, ili kulinda maisha na mali ya wananchi dhidi ya wanyama waharibifu, Serikali inahitaji ushirikiano wa dhati kati ya Serikali Kuu, Halmashauri za Wilaya na wananchi wote. Katika jitihada za kulinda maisha na mali za wananchi dhidi ya wanyama waharibufu, Serikali imekuwa ikiwatumia Maafisa na Askari Wanyamapori waliopo katika maeneo ya Wilaya husika kudhibiti tatizo hilo. Aidha, maafisa hao wana wajibu wa kuwaelimisha wananchi kuhusu tabia na mienendo ya wanyama wakali na waharibifu kama vile mamba, simba, tembo na kadhalika ili waepuke adha zinazosababishwa na wanyama hao. Hivyo ni vyema Wilaya zenye matatizo ya wanyama wakali na waharibifu zihakikishe zinaajiri Maafisa na Askari Wanyamapori wa kutosha, wenye sifa na ujuzi unaotakiwa ili kudhibiti ipasavyo tatizo la wanyama hao.

Katika ngazi ya wananchi, Serikali inajenga uwezo wao wa kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya wanyamapori waharibifu kupitia mpango maalum wa kuanzisha maeneo ya Jumuiya ya Kuhifadhi Wanyamapori *(Wildlife Management Areas - WMAs),* pamoja na kuwapatia mafunzo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 1998/99 hadi Juni, 2003, Wizara imepeleka jumla ya risasi 1,890 za aina mbalimbali Mkoani Mtwara kwa ajili ya kudhibiti wanyama wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa, Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974, hairuhusu Serikali kulipa fidia kwa madhara yatokanayo na wanyama wakali na waharibifu. Hata hivyo, kifungu cha 50 cha Sheria hiyo, kinatoa ruhusa ya kuuawa kwa mnyama mkali au mharibifu pindi anapoleta uharibu kwa maisha au mali za wananchi.

Aidha, dhana ya kulipa fidia kwa wananchi wanaoathirika kutokana na wanyama wakali na waharibu ni nzuri, lakini inahitaji kufanyiwa utafiti wa kina na wa kutosha kabla ya maamuzi ya kuwa na utaratibu wa kulipa fidia. Suala hili ni la msingi kwa kuwa wanyamapori wanapatikana karibu nchini kote, utaratibu wa kufanya tathmini ya uharibifu wa maisha na mali na kupata thamani ni ngumu hivyo unahitaji kuwa makini, gharama za fidia ni kubwa, pia mbinu za kudhibiti rushwa na kuzuia uwezekano wa hujuma kutokana na watumishi wasio waminifu ni mgumu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2003/2004, niliiarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Sheria ya Wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974 inarekebishwa. Kauli hiyo niliirudia tena tarehe 18 Februari, 2004 wakati nilipokuwa nikijibu hoja binafsi ya Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea na taratibu za kurekebisha Sheria ya Wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974. Taratibu za awali katika kupitia Sheria hiyo ikiwa ni pamoja na kupata maoni ya wadau katika ngazi mbalimbali zinaendelea.

Baada ya taratibu hizo kukamilika, Muswada wa Sheria utaandaliwa na kisha kuwasilishwa katika Bunge lako Tukufu ili uweze kujadiliwa na kupata ridhaa ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Muswada wa Sheria huu utafikishwa Bungeni, Waheshimiwa Wabunge, akiwemo Mheshimiwa Lydia Boma, watapata fursa ya kuchangia maoni na kutoa mapendekezo juu ya suala la fidia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Taarifa kuhusu Maandamano yaliyofanywa na Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Tarehe 19 Aprili, 2004**

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari mbalimbali nchini vilitoa na vinaendelea kutoa taarifa kuhusu maandamano yaliyofanywa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, sehemu ya Mlimani, kupinga Muswada uliopitishwa na Bunge hili tarehe 19 Aprili, 2004 kwa madai kwamba, hawakushirikishwa katika kuujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nirejee kwa ufupi utaratibu uliotumika hadi Bunge lako Tukufu likakubali kwa kauli moja, kuupitisha Muswada huu. Rasimu ya Muswada wa kuanzisha Bodi ya Kusimamia utoaji na urejeshwaji wa mikopo kwa wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu, ilianza kwa kujadiliwa na wadau wakuu wa sekta ya elimu ya juu tarehe 29 mpaka tarehe 30 Agosti, 2002. Katika majadiliano hayo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiliwakilishwa ikiwa ni pamoja na Serikali ya Wanafunzi ambayo iliwakilishwa na Rais na Katibu wa Serikali ya Wanafunzi ya wakati huo.

Baada ya kupitia hatua mbalimbali, Muswada ulisomwa mara ya kwanza Februari, 2004 na kuwekwa katika tovuti ya Bunge ili wadau mbalimbali wa elimu ya juu, wakiwemo wanafunzi, waendelee kuusoma na kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, tarehe 5 Aprili, 2004 Kamati ya Huduma za Jamii ya Bunge, iliandaa na kuendesha *public hearing,* yaani kukaribisha wadau kuujadili Muswada huo mbele ya Kamati hiyo huko Jijini Dar es Salaam. Wadau wakuu wote ikiwa ni pamoja na wawakilishi wa Serikali za Wanafunzi wa Vyuo mbalimbali walialikwa na kuhudhuria. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilialikwa kwa barua Na. BA.50/155/02 ya tarehe 9 Machi, 2004, lakini hawakutuma mwakilishi na hakuna sababu zilizotolewa kwa kutokuhudhuria.

Wawakilishi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, baadaye waliwasilisha maoni yao kuhusu Muswada kwa Mwenyekiti ya Huduma za Jamii, tarehe 13 Aprili, 2004. Mwenyekiti wa Kamati, aliyapokea maoni hayo. Aidha, Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Balozi Dr. Pius Ng'wandu, alikubali kuwaona wawakilishi hawa na akawasilikiza kwa makini. *(Makofi)*

Ujumbe wa wanafunzi uliongozwa na Rais wa *DARUSO.* Viongozi wengine walikuwa ni Katibu wa wanafunzi na Wajumbe wengine watatu. Hoja zao zilifanana na za wenzao kutoka Vyuo Vikuu vya Umma, nazo zilikuwa kwamba, gharama za wastani wa shilingi milioni 6.2 ni kubwa, kipindi cha miezi 12 kabla ya kurudisha mkopo ni

kifupi, tatizo la kupata ajira baada ya kuhitimu ni kubwa na mwisho, Serikali inajitoa kugharamia elimu ya juu.

Baada ya kukutana na Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, wanafunzi hao walirudi Dar es Salaam ili kutoa taarifa kwa wenzao. Tarehe 19 Aprili, 2004, Uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ulitoa ruhusa na kufuta masomo yote kuanzia saa 9.00 alasiri ili Viongozi wa *DARUSO* waweze kutoa taarifa kwa wenzao. Viongozi wa *DARUSO*, walitoa taarifa kwa wenzao kuwa baada ya kuonana na Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, pamoja na kuonana na Wabunge mbalimbali katika Kikao cha Bunge, maoni yao juu ya Muswada yamezingatiwa. Baada ya taarifa hii kutolewa, baadhi ya wanafunzi wakiongozwa na Bahati Tweve, walikataa taarifa hiyo na kuamua kwamba, wangeandamana na kuwaita viongozi wao kama ni wasaliti. Viongozi wa Serikali wanafunzi hususan wale waliofika Dodoma, hawakukubaliana na matakwa ya kundi hilo linalodai kufanya maandamano hivyo walitoka katika Kikao hicho.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 20 Aprili, 2004, baadhi ya wanafunzi wakiongozwa na Bahati Tweve, walianzisha maandamano kuelekea Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Kwa vile wanafunzi wengine walikuwa hawaungi mkono maandamano hayo, walitolewa madarasani kwa nguvu. Bahati Tweve, mwanafunzi wa mwaka wa pili, Kitivo cha Sheria ni kati ya wagombea walioshindwa katika Uchaguzi wa Serikali ya Wanafunzi uliofanyika mwanzoni mwa Aprili, 2004. *(Makofi)*

Maandamano hayo yalianzia chuoni na kuelekea Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu wa Majengo *(UCLAS),* ambapo waliwalazimisha wanafunzi wa Chuo hicho kukatisha masomo na kujiunga na maandamano hayo. Maandamano hayo yalipofikia eneo la *Survey,* wanafunzi walivamia maduka na kupora soda na biskuti, yote yameandikwa katika matukio ya habari na baadaye maandamano hayo yalivunjwa na Kikosi cha Kutuliza Ghasia.

Maandamano ya tarehe 20 Aprili, 2004 wanafunzi wa Chuo Kikuu sehemu ya Mlimani, hayakutimiza masharti yanayotakiwa kwa vile kwanza, maandamano hayo hayakuwa na kibali. Pili, waandamanaji wengi walilazimishwa. Tatu, yalihatarisha amani kwa vile yaliandamana na vitendo vya unyanyasaji na uporaji wa mali.

Mheshimiwa Spika, kumeanza kujitokezahabari za kupotosha kwamba, Muswada unanufaisha matajiri au watoto wa vigogo. Tofauti na dhana hii potofu, lengo la Muswada huu ni kuunda chombo cha utoaji na urejeshwaji wa mikopo usiokuwa na riba ili kuwasaidia wanafunzi wenye sifa toka familia zenye kipato cha chini kama inavyobainishwa katika ibara. *(Makofi)*

Narudia tena, wenye kipato cha chini kama ilivyobainishwa katika ibara ya 17(i)(d). Pili, Muswada huu unakusudia kuongeza idadi ya wanafunzi katika Taasisi za Elimu ya Juu, inakadiriwa kwamba katika miaka mitano ijayo, idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kwa kutekeleza mpango huu itaongezeka hata kufikia 50,000 kutoka 18,000 ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu dhamana, kipengele kinachohusu dhamana kinaelekea vile vile kutoeleweka vizuri na kinatumika kupotosha ukweli. Katika utoaji wa mikopo ni suala la kawaida kwa vile inamhakikishia mkopeshaji, urejeshwaji wa mkopo na inamhimiza kutimiza wajibu wake. Ndiyo maana ya dhamana. Hoja ya msingi hapa ni aina ya dhamana ambazo hata wananchi wa kawaida wanaweza kumudu kama ambavyo zinapendekezwa. Baadhi ya dhamana ambazo Bodi inakusudia kuzitumia ni hati ya ardhi au shamba, hati ya nyumba, maana yake kila moja wapo hapa inajitegemea siyo kwamba zote uwe nazo, mojawapo inatosha.. Hati ya nyumba, hati ya Bima ya maisha, akaunti ya benki, ajira ya kudumu ya mkopaji au mdhamini na sehemu ya biashara au leseni yoyote ile na pia utaratibu utawekwa katika ngazi ya Kata, Kijiji, Mashirika ya Dini, Vyama vya Hiari, Halmashauri za Wilaya, ili waombaji waweze kudhaminiwa au kujidhamini wao wenyewe. *(Makofi)*

Kurejeshwa kwa mikopo kuanzia Julai, 1994, wanafunzi wa Taasisi ya Elimu ya Juu walitakiwa kujigharamia chakula na malazi. Kwa wakati huo gharama hizo zilikadiriwa kufikia shilingi 350,000 kwa mwaka. Kiasi hiki cha fedha kwa wakati ule kilionekana kikubwa kwa mwanafunzi wa kawaida kuweza kuimudu gharama hiyo.

Ili kuhakikisha kwamba, wanafunzi wenye sifa na ambao wanatoka kwenye familia maskini, hawashindwi kuendelea na masomo kwa sababu ya uwezo mdogo kiuchumi. Serikali ilianzisha utaratibu wa kutoa mikopo kwa ajili ya chakula na malazi. *(Makofi)*

Mikopo hiyo, ilitolewa kwa masharti ya kurejeshwa mara baada ya kuhitimu. Wakopaji kabla ya kupewa mikopo walitakiwa kujaza fomu maalum za maombi ya mkopo na kuwekeana mkataba na mkopeshaji. Sheria inayopendekeza kuundwa kwa Bodi ya Mikopo inatoa tu mamlaka kwa Bodi kukusanya mikopo iliyokopeshwa toka mwaka 1994 kwa masharti ya wakati huo. Hivyo, hakuna mantiki kudai wanafunzi waliosoma kabla ya mwaka 1994 eti nao kwamba kwa sababu wamegharamiwa na Serikali walipe kwa vile hapakuwa na makubaliano au mkataba wa namna hiyo, kwamba Serikali imejitoa kugharamia elimu ya juu. Huu vile vile ni upotoshaji. Kumejitokeza wasiwasi miongoni mwa wanafunzi kwamba, Serikali imejitoa kugharamia elimu ya juu. Wasiwasi uliopo miongoni mwa wanafunzi hasa wale wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hauna msingi kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, wastani wa mkopo kwa mwanafunzi anayesoma kwa miaka mitatu ni shilingi milioni tatu na laki tisa. Katika kipindi hicho cha miaka mitatu cha masomo pamoja na ule wa nafuu *(Grace Period)*, Serikali itaendelea kutoa fedha kwa Bodi wakati wahitimu hawajaanza marejesho. Katika kipindi hicho, Serikali inatarajia kuchangia shilingi 65 bilioni kwa idadi ya wanafunzi 16,000 waliopo sasa. Pili, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Taasisi zake kwa wastani wa shilingi bilioni 42 kwa mwaka. Tatu, Serikali itagharamia mafunzo ya watumishi ambao wako kwenye Vyuo Vikuu hivyo. Nne, kwa vile mkopo hauna riba, narudia, kwa vile mkopo hauna riba, gharama za uendeshaji wa Bodi zitabebwa na Serikali. *(Makofi)*

Tano, Serikali itatoa *scholarships* kwa wanafunzi wachache waliofaulu vizuri ambao watasoma masomo yenye umuhimu wa kipekee kwa Taifa ndani na nje ya nchi, mfano, madaktari. Kwa hiyo, Serikali imo kabisa katika kugharamia. Gharama halisi ya elimu ya juu kwa mwanafunzi ni wastani wa shilingi milioni moja na laki sita katika Vyuo Viku vya Umma. Ada tu *(Tuition Fee)* ni wastani wa kati ya shilingi laki sita na milioni moja. Mwanafunzi atakopeshwa shilingi laki sita tu kwa ajili ya ada. Tofauti baina ya gharama halisi na kiasi cha mkopo wa ada utakuwa ni mchango wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinyume na taarifa potofu zinazoenezwa na wanafunzi wachache na baadhi ya vyama vya siasa, Wanafunzi wamepewa uwakilishi mkubwa katika Bodi inayopendekezwa kuundwa na Muswada kwa mujibu wa Ibara ya 5 fasili ya (1). Miongoni mwa Wajumbe wa Bodi ni pamoja na wanafunzi wawili kutoka Vyuo vya Elimu ya Juu nchini. *(Makofi)*

Ni dhahiri kwamba, wanafunzi hao walioandamana ama hawajausoma Muswada au hawakuelewa, vitu vyote viwili havifanani kabisa na Taasisi ya Elimu ya Juu. Kwa vile hawakutaka kushiriki katika majadiliano mbalimbali yaliyohusu Muswada huu, hawaelewi pia marekebisho yaliyofanywa baada ya kuzingatia maoni ya wadau walioshiriki katika Warsha ya Morogoro tarehe 29 mpaka tarehe 30 Agosti, 2002. Vile vile hawakuhudhuria kwenye *public hearing* ya Dar es Salaam ya tarehe 5 mpaka 6 Aprili, 2004 na maoni ya Waheshimiwa Wabunge, ambayo waliyatoa hapa Bungeni nayo vile vile hawayazingatii. Wanafunzi wa Taasisi za Umma wanaolalamikia Muswada wa kuanzisha Bodi ya Mikopo kwa wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu, wanabainisha wazi ubinafsi wao dhidi ya wenzao wapatao 4,000 waliopo katika Taasisi Binafsi na za Umma ambao wao wanatoka katika familia maskini na wanalipa ada kubwa zaidi kati ya shilingi milioni moja na laki nane hadi milioni tatu kuliko wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia vitendo vya utovu wa nidhamu uliofanywa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, sehemu ya Mlimani, Uongozi wa Chuo Kikuu, uliitisha mkutano wa Kamati ya Wakuu wa Vitivo na Wakurugenzi, kujadili na kupendekeza mbinu za kukabiliana na mgogoro huo. Kamati hiyo ilikutana tarehe 20 Aprili, 2004 na kupendekeza kwa Kamati ya Utendaji ya Baraza la Chuo Kikuu kwamba, wanafunzi wote isipokuwa wale wa Shahada za Uzamili na wanaotoka nje ya nchi, wasimamishwe masomo kwa muda usiojulikana kutokana na vitendo vya kuvunjika amani hapo Chuoni. Hatua hiyo, itatoa fursa kwa Chuo kuwatambua wanafunzi ambao ni chanzo cha mgogoro na wale wasiohusika ili wasiohusika warudishwe madarasani haraka iwezekanavyo na wale ambao wanahusika wachukuliwe hatua za kinidhamu. *(Makofi)*

Serikali imesikitishwa na mwenendo, tabia na vitendo ya utovu wa nidhamu, uliofanywa na wanafunzi hao. Baadhi ya vitendo hivyo ni uharibifu wa mali za watu, ambao ulihusisha uvunjaji wa vioo vya magari, uporaji wa mali za watu, uvunjaji wa Sheria za nchi kwa kufanya maandamano bila kibali. Serikali haiamini kuwa maandamano ndiyo ilikuwa njia pekee ya kuwasilisha maoni ya wanafunzi hao. Serikali inalaani vikali vitendo hivyo vya utovu wa nidhamu na uvunjaji wa masingi ya

kidemokrasia na inaunga mkono hatua za awali zilizochukuliwa na chuo hicho. Serikali itachukua hatua kali za kinidhamu dhidi ya wale wote watakaobainika kuchochea maandamano ikiwa ni pamoja kuwafutia udhamini. *(Makofi)*

Aidha, Serikali inawapongeza Viongozi wa *DARUSO* kwa ujasiri wao wa kujaribu kuwaeleza wanafunzi wenzao, matokeo ya majadiliano yao na Waziri na Wabunge. Utumiaji wa vitisho na nguvu sio sifa au mhimili wa demokrasia. Huu ni uhuni na udikteta ambao unahitaji kulaaniwa na wananchi wote wapenda amani na demokrasia. Chuo Kikuu ni mahala pa heshima. Narudia, Chuo Kikuu ni mahala pa heshima kubwa katika ngazi zote za elimu, ni kitovu na chimbuko la uhuru wa kujieleza, nguvu ya hoja, subira na nidhamu ya fikra zilizokomaa. Kupageuza Chuo Kikuu kuwa mahala pa ghasia, huu ni utovu wa kufikiri. Utovu wa kufikiri ni hasara kubwa kwa Taifa hili na vizazi vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati umefika kwa Taifa letu na hasa kwa wanafunzi wa Vyuoni kulinda haki zao za kusoma kwa amani, uhuru na utulivu. Matatizo hutatuliwa kwa majadiliano, ushirikishwaji na subira.

Matatizo hayataisha duniani katika maisha yetu, tuyakabili kwa busara, subira na ujasiri wa kujenga nguvu ya hoja. Wasomi wanajua fika kwamba watu wenye busara huona katika matatizo fursa ya mafanikio na pia wasomi hao hao wanajua fika kwamba watu wasio na busara na hugeuza fursa au bahati kuwa tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu kimsingi sio tatizo, la hasha, bali ni fursa ya kuzisaidia familia maskini pamoja na Taifa hili kusomesha vijana kwa wingi. Mikopo ikirejeshwa itatumika kusomesha vijana wengine maskini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaahidi kuwa makini zaidi katika kutumia raslimali nyingi zaidi katika kujenga miundombinu ya Elimu ya Juu, Ufundi na Utafiti ili kuongeza nafasi za utahili wa wanafunzi katika Vyuo Vikuu vyetu. Tayari Mfuko wa Elimu ulioundwa hivi karibuni umeshatoa misaada mbalimbali katika kuboresha miundombinu katika Vyuo Vikuu 12 nchini. *(Makofi)*

Aidha, Serikali hususan Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, imekuwa mstari wa mbele kuwa karibu na Taasisi na Vyuo vyetu vya Elimu ya Juu.

Wizara pia imekuwa karibu sana na uongozi wa wanafunzi wa Vyuo hivi ili kubaini kwa haraka mahitaji na matatizo ya wanafunzi kwa lengo la kutoa majibu na utatuzi kwa haraka. Ushirikiano wa hali ya juu uliokuwa umekwishajengeka kati ya wanafunzi, Vyuo na Wizara hii, tusikubali ukavurugwa na tukio hili.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha. *(Makofi)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004**
***(The Income Tax Bill, 2004)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wanaokwenda kunywa chai ruksa. Namwomba Mheshimiwa Naibu Spika, anipokee Kiti.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Muswada huu muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuungana na wenzangu walionitangulia kuwapongeza kwa moyo wa dhati kabisa, Waheshimiwa Wabunge wenzetu Mheshimiwa Getrude Mongella, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa William Shija, Mheshimiwa Kissassi na Mheshimiwa Dr. Kabourou, kwa kuchaguliwa kwao kuwa Wabunge wa Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyosemeka, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kama 11 ambazo nazo zimegawanyika katika vipengele vidogo vidogo mbalimbali. Kama ilivyo desturi ya Miswada, jicho la Muswada huwa katika sehemu ya kwanza ambayo inaorodhesha ni lini Muswada utaanza kutumika pamoja na tasfiri ya maneno yaliyotumika ndani ya Muswada wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 1(3) ya Muswada huu, iko kwenye Sehemu ya Kwanza, napenda kuzungumzia katika Ibara ya 3 na Ibara nyingine nne ikiwemo Ibara ya 17, 18, 21 na 22. Sehemu ya Pili ya Muswada inatoa misingi ya utozaji wa kodi, nani atozwe, kiwango gani na ni aina gani ya kodi ilipwe. Pamoja na kwamba Muswada una sehemu nyingine nane zaidi, kama nilivyosema mchango wangu uko-*limited* kwa Ibara ya 3, 17, 48 na 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada huu ni pamoja na kuboresha makusanyo ya Kodi ya Mapato. Taratibu zilizotumika kuleta Muswada huu, kwangu hauniridhishi. Kodi ya Mapato inamgusa kila Mtanzania, kila mtu yeyote anayeishi Tanzania awe mtoto, mzee awe mwanamke au mwanaume. Kwa mantiki hiyo basi, ingekuwa jambo la busara kama ungetanguliwa na Kamisheni kwanza ambayo ingeweza kuzungumza na wadau wote kuona ni jinsi gani ya kuweza kuboresha Muswada huu maana Muswada wenyewe ni mpya, wa kigeni unafuta Sheria ya mwaka 1973, ni Muswada mkubwa kabisa. Sasa Watanzania watajuaje kweli kama Muswada huu utawasaidia? Kama leo tukiupitisha Muswada huu ina maana kwamba kila Mtanzania ama kila mtu anayeishi Tanzania anatakiwa alipe kodi kwa kiwango ambacho kwa kweli yeye hakijui. Sasa mimi nadhani ungekuwa *preceded* na Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao uzoefu mkubwa huko nyuma Serikali ilipotaka kubadilisha Sera ya Benki iliunda Tume chini ya Balozi Nyirabu ikatoa mapendekezo yake baadaye sheria ikatungwa ya *Banking and Financial Institution Act.* Pia Serikali ilipotaka kuangalia upya Sheria ya Ardhi iliunda Tume chini ya Profesa Shivji wakafanya uchunguzi mkubwa ambao uliweza kuonyesha ni jinsi gani wanaweza kuboresha Sheria ya Ardhi baadaye ndio tukawa na Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999. Kwa maoni yangu, nadhani ilikuwa vema kama Serikali ingefanya hivyo badala ya kuleta Muswada huu bila matayarisho ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara ya kufanya hivyo ni kwamba Muswada kama ulivyo haueleweki kabisa, Kiingereza chake cha ovyo ovyo tu hata sijui kikoje na siamini kama kweli sisi Wabunge tukiusoma Muswada huu kweli tunauelewa. Mimi nimebobea kidogo kwenye mambo ya sheria lakini ninapoangalia maneno yaliyotumika kwa kweli mtu anayetoka kijijini kwangu huko Musoma siamini akiusoma atauelewa. Nasema hivyo kwa kuwa Sheria yoyote ya Kodi lazima itungwe kwa kutumia maneno ya wazi yasiyo na kasoro, yenye ulaini, ya kuvutia kusoma ili uweze kuelewa mfukoni kwako unaambiwa na Kaizari utoe kipi? Kama Muswada wa Kodi hauna sura hiyo, haufai kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitanukuu kwa Kiingereza wataalam waliobobea kwenye mambo ya utungaji wa Sheria za Kodi. *"The purpose of Legislation is most likely to be expressed and communicated successfully by the drafter who is ardently concern to write clearly and to be intelligible. The obligation to be intelligible and to convey the intended meaning so that it is comprehensible and easily understood requires the unremitting pursuit of clarity by the drafter". (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *clarity in a legislative context requires simplicity and precision.* Ukiuangalia Muswada huu una-*fail to meet test* hiyo, hauko *simple,* hauko *clear* na uko *confused* kabisa. Sijui kwa nini haraka hii imefanyika kufanya matendo kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria iliyopo ya Mwaka 1973 ina *meet criteria* hii ya kuwa Sheria ya Kodi lakini hii haikidhi mahitaji haya. Nitatoa mifano mingi kujua ni kwa nini ninasema hivyo. Kwanza kabisa, ukiangalia Muswada huu pamoja na kusema kuna tasfiri iko *contained* kwenye Ibara ya 3, utakuta kila ukurasa unasema *subject to this Act, subject to this Act,* sasa hujui ni kipi hakipo *subject to this Act,* mimi sijui. Ukifuta *subject to this Act,* unaanza kupata sura mpya kabisa lakini kila Ibara ukienda inasema *subject to this Act.* Hii inamaanisha kwamba hata *definition* pia ni *part* ya hiyo *Act,* sasa ukisema *subject* ina maana gani, mimi sijui.

Nitakupa mfano, tukiangalia Ibara ya 21, hapa nazungumzia ukosefu wa *clarity na precision,* inasema: *"Subject to this Act, a person shall calculate their income according to generally accepted accounting principles".* Sasa unajiuliza maana ya *generally accepted accounting principles* ni nini? Ukiangalia kwenye *definition* hakuna, jambo la muhimu kabisa! Anasema a *person shall* calculate their income, sasa a person ni singular, shall calculate ile their pale inakuwa plural Kiingereza gani hiki kinatungwa na

Wizara ya Fedha? Hapo hapo, unatakakuta inasomeka narudia tena *subject to this act, a person shall calculate their income,* huwezi ku-*calculate income, income maana yake* nini? Mimi leo nimepata kibahasha nadhani nimepewa posho yangu ya kuhudhuria sasa si-*calculate hiyo* posho hiyo ndio *income* yangu ya leo. Mimi nadhani *drafter* alitaka kusema *a person shall account for his income, correct term* ilikuwa ku-*account for income* sio ku-*calculate income. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu Muswada wote umejazwa na maneno kama haya ambayo siyo ya Kiingereza wala hayaeleweki wala sio Kiswahili mimi nadhani walipa kodi watakuwa na matatizo sana kuelewa Muswada huu. Atakayeutafsiri atakuwa ni nani, nadhani atakuwa ni Kamishna wa *Income Tax* maana yake ni kwamba kesi zitazidi sana kwenye *Tribunal* huko watakaoshiba nadhani ni Mawakili, siyo *Treasury.* Maana ubishi utakuwepo una maanisha ku-*calculate* au ku-*account* haya siku tatu, nne, ubishi wa namna hiyo hautaongeza kabisa mapato ya nchi. Sasa tumeingia kwenye utandawazi karibuni tutajiunga na *Commonwealth* tumeshaingia mle ndani, wenzetu Kenya na Uganda hawana Muswada ulikuwa *drafted* vibaya, vibaya hivi na ndio sasa tushindane nao. Mimi siamini tuko *serious* kwa karne ya 21 tukashindwa kupata mtu wa ku-*draft* Muswada wa Kodi unaoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, itikadi inasema ni lazima niunge Muswada kama huu. Sasa mimi kwa shingo upande nasema ndio nitaunga kwa kuwa lengo ni kukusanya kodi kuendesha nini?

**MBUNGE FULANI:** Nchi.

**MBUNGE FULANI:** Na wewe ni mwana CCM.

**MHE. NIMRODI E. MKONO:** Na mimi ni mwana CCM, lazima. Kwa hiyo, naunga mkono Muswada huu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa masharti haya, nenda ukafanye marekebisho makubwa, andika Kiingereza *simple* na kina *clarity,* kodi utakusanya kwa urahisi. Watu wataelewa wajibu wao ni nini na sio kuwaburaza kwenda kwa *Tribunal* kujua ni nini Kaizari anataka na nini sio cha Kaizari. Wazungu wanasema: *"Render unto Caesar what belongs to Caesar",* mpe ulichompa, Muswada huu hauonyeshi tumeipa Serikali kipi na kipi tunabakiza mfukoni mwetu. Kwa kuwa nimeshachangia kwa maandishi, nimechambua Ibara hadi Ibara na nimempa Mheshimiwa Waziri wa Fedha maoni yangu, nadhani watazingatia maoni na mchango wangu ili waweze kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, Ibara inayo-*deal* na mambo ya *partners* iangaliwe upya. Nitatoa mfano, *partnership* siyo *cooperation* kwa mantiki ya Muswada huu siyo *cooperation* lakini *partnership* ni ubia. Mimi pale *PPF Tower* ninayo ofisi tulipewa *floor* nzima tu ambayo iko wazi tukafanya *partitioning* zile gharama za kufanya *partitioning* ni *capital expenditure* kwa kuwa sisi ni *partnership* siyo *cooperation* hizo *capital allowances* hazipatikani lakini mwenzangu ghorofa ya pili

ambapo yeye ana *trade* chini ya *cooperation* anapewa hizo *capital allowances.* Ningeshauri Serikali iangalie upya *taxation* ya *partnership.*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda umeniishia, ahsante sana na naunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Muswada huu. Pamoja na kupongeza Wizara ya Fedha kwa kuuleta Muswada huu kwa lengo la kuuboresha na kuweka wigo mkubwa zaidi wa viwango vya Kodi ya Mapato, ningependa kutoa maoni yangu katika maeneo kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaelekeza maoni yangu katika maeneo mawili muhimu hasa kwa kutizama ile *first schedule of tax rate and second schedule of tax rate.* Ukichambua hizo kwa makini kabisa na kwa dhati kabisa utaona kuna tatizo la uwiano wa viwango vya kodi kati ya wafanyakazi na wafanyabiashara. Nitatoa mifano. Kwa mfano kwa kima cha chini cha mshahara wa Sh.50,000 ni kwamba mshahara huu hauna kodi ni mshahara wa Sh.600,000 kwa mwaka hauna kodi. Tukisogea katika ngazi inayofuatia tuchukue mfano wa mshahara wa Sh.60,000 kwa mwezi ambao ni sawasawa na Sh.720,000 kwa mwaka kwa kiwango cha kodi kilichoonyeshwa katika jedwali nililolitaja kwa mshahara huu kodi ni Sh.22,200 kwa mwaka ambapo ni sawasawa na 3.08% ya pato lenyewe. Kwa upande wa pili wa biashara kwa kiwango hicho kinachofanana na mshahara huo au kipato hicho ambacho ni kati ya Sh.500,000 hadi 3,000,000 kwa mwaka, kodi ambayo ni *turnover* ya Sh.500,000 hadi Sh.3,000,000 kodi yake ni Sh.20,000 kwa mwaka ambapo ni sawasawa na wastani wa asilimia 0.7. Kiwango kingine cha mshahara cha juu kidogo ukikifanyia mahesabu mshahara wa Sh. 970,000 kwa mwezi ambao ni sawasawa na Sh.11,600,000 kwa mwaka, kodi yake kwa mwaka ni Sh.2,796,000. Ukienda upande wa pili wa biashara kwa kiwango kinachofanana na kiwango hicho nilichokitaja cha jumla ya *turnover* kati ya Sh.7,000,000 na 14,000,000 kodi yake kwa mwaka ni 165,000. Sasa tunaweza kuona tofauti kati ya Sh.2,796,000 na Sh.165,000 kwa mwaka. Kwa upande wa mshahara kiwango nilichokitaja ni sawasawa na wastani wa 23.5% wakati kwa kiwango cha biashara kwa kodi hiyo ya Sh.165,000 kwa mwaka ni sawasawa na 1.42%.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama mshahara nilioutaja wa Sh.970,000 kwa kiwango cha kodi inayotozwa kwa mwezi ambao ni wastani wa Sh.2,033,000 maana yake inakaribia robo ya mshahara wenyewe unaozungumziwa, sasa robo ya mshahara unaichukua kutoka kwa mfanyakazi kama sehemu ya kodi. Nadhani ukilinganisha na eneo hili la biashara utaona kwamba uwiano katika kodi hii ya msingi ambayo ni Kodi ya Mapato Kitaifa uwiano huo haupo, upo mbali sana. Nadhani ni vizuri basi kama tunafanya marekebisho ya Kodi ya Mapato, mapato kwa wananchi wote Kitaifa, basi ni vizuri mfumo wetu wa kodi na sheria yetu ya Kodi ikaonyesha angalau dalili za uwiano katika viwango vya kodi na hapo tutakuwa tumeijengea heshima nchi yetu, tumeijengea heshima sheria ambayo kwa kweli inawakabili au inakwenda kwa wananchi wetu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoka hapo, nielekee katika kodi nyingine ambazo pengine zimeguswa kidogo tu huku lakini ni kodi ambazo zinalenga katika mapato ya mwananchi lakini zinabuniwa na taasisi nyingine kwa mfano mamlaka za Miji, Halmashauri na Manispaa. Kodi ninazotaka kuzungumzia hapa ni kodi hizi za Majengo. Ukienda katika Manispaa, Halmashauri na Miji utakuta kodi hizi ni kubwa sana kwa jengo ambalo pengine wala si jengo la biashara. Kodi ya jengo Sh.150,000 kwa mwaka sasa kiwango hiki ni kikubwa mno kuliko wastani wa pato la kawaida na kodi ya kawaida ya mapato. Sasa uwiano uko wapi? Ni vizuri basi tukaangalia kama tuna Sheria ya Kodi ya Mapato basi hii iwe ndio *overall,* Msimamizi Mkuu na Mhimili wa kodi za aina nyingine zote ili taasisi na mamlaka nyingine zisibuni viwango vya kodi ambavyo ni vikubwa zaidi ya viwango vya kawaida vya Kodi ya Mapato Kitaifa chini ya Sheria ambayo tunaitunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hili ni eneo pia ambalo lazima tulitazame na ili tuondoe mwanya huo ambao unatumika na vyombo vingine ambapo wamepewa kisheria kwa sababu wanaruhusiwa kutoza kodi mbalimbali. Sasa ili kuondoa mwanya huo, basi ni vema ndani ya sheria hii tukasema kabisa wazi kwamba hakutakuwa na mamlaka itakayoruhusiwa kutunga au kubuni viwango vitakavyokuwa vikubwa zaidi ya viwango hivi vinavyotumika sasa kama viwango vya kodi ya Mapato chini ya sheria ya Kodi ya Mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba tufanye marekebisho kidogo ambayo ninaona ni muhimu yafanyike katika hii *first schedule* ukurasa ule wa 131 au katika *schedule of amendment* ukurasa ule wa 12, katika sehemu ndogo ya tatu pale kuna tasfiri inayosema *where turnover is less than three million shillings* maana yake unazungumzia kiwango ambacho hakifikii shilingi milioni tatu. Ukiteremka chini pale unakuta *item* nyingine inasema *where turnover exceeds shilling three million but does not exceed seven million shillings.*

Sasa unapoiacha hivyo maana yake ni kwamba kiwango kwa mfano *turnover* ikiwa ni *exactly* shilingi milioni tatu haiko *covered* maana yake sehemu ya kwanza inasema *where turnover is less the three million,* hujaigusa *three million* na ukienda ya pili inasema *where it exceed three million* maana yake *three million* itakaa kati kati na upo uwezekano mkubwa kabisa wa kuwa na *turnover* ya *exactly three million shillings.* Sasa pendekezo pale ni kwamba badala ya kusema *where turnover is less than three million shillings* tuseme *where turnover is less than or equal to three million shillings.* Hapo utakuwa umeiingiza ndani ile figure ya three million shillings ambayo inawezekana kabisa ikawa *turnover* ya mfanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoka hapa labda nizungumzie jambo lingine ambalo linagusana kidogo na Sheria hii ya Kodi ya Mapato. Ni sheria ambayo tunayo ya *Stamp Duty.* Sasa kuna sheria ya *Stamp Duty*, sheria ambayo vile vile *basis* yake kwa kweli ni pato au mauzo ya kila siku ya mfanyabiashara. Sasa haya mauzo ya kila siku maana yake nini? Maana yake ni kwamba yanagusa ile *income* ya mfanyabiashara huyo au faida yake inakuwa inaguswa ndani ya hiyo kodi au mauzo yake ya kila siku. Sasa unapomwambia chini ya Sheria hii ya *Stamp Duty* ulipe *stamp duty*

wewe kama mfanyabiashara. Halafu mfanyabiashara huyo huyo unamgeukia tena kwa upande wa pili na sheria hii ya *Income Tax* unamwambia utalipa *income tax* inayofanana na *turnover* yako ya mwaka, maana yake nini? Maana yake ni kwamba unagusa *income* ya mtu na kui-*tax* mara mbili kwa *Stamp Duty Act* na vile vile kwa *Income Tax Act.* Sasa huyu mtu atabaki na nini kama huku unamchukulia na upande wa pili pia unamchukulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndiyo maana kuna matatizo kweli ya kukua kwa biashara zetu hasa biashara ndogo ndogo, hazikui kwa sababu wanachukuliwa hela nyingi sana kwa mfumo wa kodi tuliouweka kuliko kile kinachobaki mfukoni kwake. Sasa ataendeleaje kama sehemu kubwa ya faida anayopata inachukuliwa kama kodi. Kwa hiyo, ni vema katika kuweka uwiano mzuri basi tuangalie kama kweli kuna haja ya mwenye kulipa *income tax* lazima tena kwa upande wa pili alipe *Stamp Duty.* Kama hilo litaonekana lina mantiki ndani yake basi tufanye marekebisho katika sheria hii na tuseme waziwazi kwamba kwa mfanyabiashara ambaye analipa *income tax* chini ya sheria hii basi hatakuwa na ulazima wa kulipa *stamp duty.* Kwa kuweka rekebisho hilo dogo maana yake tutakuwa tumemwondolea *double taxation* mfanyabiashara huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni sehemu hii ya sita *section ya 89(2b)* ambapo yapo maneno mazuri yameandikwa pale yanasema: “Makadirio ya kodi ya mapato ya mwaka unaohusika yatiwe saini kwa ufahamu na uelewa na usahihi na ukweli wa mlipa kodi”. Sasa hayo ni maneno mazuri kweli na kama *principle* ndiyo hiyo nadhani ni vizuri kwamba *principle* hii hatuitumii vizuri. Sasa ni vizuri chini ya utaratibu huu sasa basi tu-*exercise* hizi *principles* tunazojiwekea vizuri, tuwatendee haki wafanyakazi, nitatoa tu mifano michache.

Mheshimiwa Naibu Spika, fomu ile ya *assessment* yenyewe ni ngumu kweli kuielewa kwa mfanyabiashara ambaye kwa kweli hana upeo mkubwa wa elimu kuielewa ile peke yake nini kinachofanyika, mimi ni mfanyabiashara vile vile najua nini kinachofanyika. Mara nyingi unaonyeshwa tu mahali pa kutia saini basi unatia saini pale, halafu wakubwa wanaandika zile namba zao, matokeo yake unakuta wewe badala ya kulipa kiwango cha shilingi elfu ishirini hawa jamaa wana-*target* tu ulipe elfu hamsini au laki moja sitini na tano. Kwa hiyo, watakuwekea kiwango ambacho kitafanana na kiwango hicho atakachokwambia ulipe. Sasa nasema tuwatendee haki wafanyabiashara na wananchi wetu. Fomu hizi mara nyingi nimeshawahi kusema kwamba zipo *complicated* kweli, najua sasa mtapata matatizo ya kuzichapisha upya na mnaona itakuwa ni gharama na kwa hiyo zinaendelea kutumika, lakini mimi mwenyewe pamoja na usomi wangu nimewahi kuletewa fomu nikashindwa hata namna ya kuijaza, pamoja na usomi wangu na *Masters* nilizokuwa nazo. Sasa huyo mfanyabiashara mdogo ambaye elimu yake haijafikia hata kiwango cha elimu ya sekondari ataweza kweli kuzimudu. Sasa nasema tutekeleze haya tunayoyasema na vile vile tufanye fomu zetu zile ziwe *simple* kwa kiwango ambacho kwa kweli wafanyabiashara wataelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba basi angalau mawasiliano mazuri yawepo kati ya wakati Muswada unapopitishwa Bungeni, muda ambao pengine utachukua ili kungojea Rais aupitishe na baadaye uweze kuandikishwa katika gazeti la

Serikali na sheria ianze kutumika. Mara nyingi watu wetu wamekuwa wakidhani kwamba baada ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni basi kodi zinaanza kutumika mara moja. Sasa ni vizuri wananchi wakaeleweshwa kwa sababu hili limetokea sana. Waliposikia viwango vimefika shilingi elfu ishirini kila mtu alikwenda kutaka kulipa kodi kwa haraka sana, lakini kumbe taratibu zilikuwa bado hazijakamilika na mimi hapa ninayo nakala tu ya gazeti la tangazo la *TRA* wanazungumzia habari ya sheria hizi. Ukitazama tarehe hizi utaona kwamba imepita zaidi ya miezi mitano, Muswada umeandikishwa tarehe 21 Novemba, 2003 lakini tangazo linatoka kwenye gazeti la Uhuru tarehe 9 Februari, 2004. Sasa kama hawa watu walikuwa hawa-*enjoy* viwango fulani vya *VAT exemptions*.

Mheshimiwa Naibu Spika naomba kusema kwamba naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. AMAN W. A. KABOUROU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi nichukue dakika moja kwanza kuwapongeza ndugu zangu Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Ntagazwa na Mheshimiwa Ngw'andu kwa nyadhifa kubwa walizopata kama wawakilishi wa Tanzania katika mikutano ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa niongelee Muswada huu wa Kodi kwa kuzingatia kitu kimoja tu kwamba mimi nadhani kodi ndiyo kiwanda kikuu cha Serikali yoyote ile, ndiko inakopata pesa zote. Jana tu tulikuwa katika uzinduzi wa barabara ya Dodoma-Manyoni na yalisemwa maneno mengi pale, Mheshimiwa Rais alilalamika sana kuhusu suala zima la kujitegemea na kwamba hatuwezi kujitegemea kama tutakuwa ombaomba na kuwa kwa kweli Urais katika nchi hizi imekuwa zaidi ni kutekeleza matakwa ya wale wenye pesa na akasema pale kwamba hata hao tunaowaona wenye pesa hawazipati hivi hivi, wanawatoza kodi ndugu zao huko halafu ndiyo wanatuletea sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mimi naona ajabu sana nchi kama Denmark au Finland inatupa sisi pesa na sisi tunashangilia. Wao wapo watu milioni sita au nane, hawavuki kumi, sisi tupo watu milioni thelathini na nne na kidogo.

Lakini ni dhahiri kabisa kwamba *our production per capita* ni ndogo sana kiasi kwamba Serikali haiwezi kukusanya kodi. Sasa tunaishia kuwa watu wengi lakini kipato kidogo na Mheshimiwa Rais alisema hayo kwa uchungu kwa sababu alikuwa anazindua barabara ambayo inajengwa kwa pesa ya kodi za Watanzania kwamba tumeweza kukusanya bilioni mia nne na kidogo kujenga hivi vipande ambavyo sasa vinamalizia au vinaunganisha nchi nzima kitu ambacho zamani kisingewezekana kwa sababu tungewategemea wafadhili wasingetupa. Sasa naona ajabu kwamba suala la kodi bado hatujaliona kama ni la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia sana Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Kasaka akipendekeza kwamba kwa kweli tulitakiwa tuwe na program endelevu ya muda mfupi na muda mrefu kuhusu suala zima la kodi na lazima iwepo

sheria vile vile ya kufanya tathmini kuhusu suala zima la kodi. Leo vile vile nimemsikia Mheshimiwa Mkono anasema kwamba labda kwanza kungekuwa na Tume ya kutuambia kwa nini tulipe kodi na tulipe vipi. Lakini labda vyote hivi vitawezekana ila mimi hoja yangu ni ndogo tu. Nayo ni kwamba hatuna pesa lakini kila mtu anakiri kwamba pesa zipo na kwamba sidhani na humu haisemi, *TRA* sasa hivi hawakusanyi hata asilimia ishirini ya mapato yetu ambayo yapo na kila mtu anakiri yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, humu nimeangalia huu Muswada au sheria hatuambiwi kwa mfano huku nyuma huwa kuna vijisehemu vinatwambia hata kwa kiswahili madhumuni na sababu. Sasa tumeambiwa tu kwamba sheria ya mwaka 1973 ilikuwa ngumu, kwa hiyo sasa tunaibadili inakuja ya mwaka 2004. Sawa, lakini je, ni sheria iliyofanya tushindwe kukusanya mpaka tukusanye chini ya asilimia ishirini na ni kwa vipi? Kama ni kweli sheria ya 1973 ndiyo iliyokuwa kikwazo cha kukusanya kipato ili Watanzania waweze kupata maendeleo je, sheria hii tunayoletewa hapa inatwambia yenyewe kwa uzuri wake itakusanya kipato hicho kwa asilimia ngapi maana yake bado *agent* wetu ni yule yule *TRA,* haisemi hapa.

Kwa mfano Mheshimiwa Naibu Spika, tungeambiwa hapa madhumuni, kwa mfano tangu 1973 kwa kuwa sheria ilikuwa ni ngumu na mbaya tuliweza kukusanya tu asilimia kumi na tano. Lakini kwa sheria hii jinsi tulivyoitunga kipengele (a), (b), (c), (d) tunasema hapa kwamba sasa tutakusanya asilimia tisini na kama tukishindwa kukusanya asilimia tisini hii itakuwa ni upuuzi wa watendaji. Haisemi ila inasema tu ilikuwa sheria mbaya, sasa tunaletewa sheria nyingine, lakini hatujui hii nayo itasimamiwa vipi mpaka kwa kweli tuwe na uhakika kwamba kuibadili sheria ya mwaka 1973 ni kwa manufaa yetu sisi Watanzania. Maana yake sisi tungependa kulipa kodi, lakini haiwezekani ulipe kodi ambayo unajua dhahiri unakwenda kuwanufaisha magenge fulani. Sheria ambazo zina fomu ngumu hata mtu mwenye *Masters* hawezi kuijaza. Sheria ambazo zinasababisha watu wajinyonge kwa sababu hataki kumwona hata mkusanya kodi wa *TRA*. Huko Mbeya haya mambo yametokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa kwa kweli Mheshimiwa Waziri aniambie kwa kuibadili sheria ya mwaka 1973, kwa hiyo sasa kwa sheria hii na mpangilio huu kwa kweli *TRA* wakishindwa kukusanya asilimia 95 tunakufa na Kamishna wa *TRA,* hilo halisemi. Tunaongeza tu vyeo humu na migao na nani atamsamehe nani lakini ni huyu huyu mtu mdogo ndiye anatakiwa abebe mzigo wote huu na hatujasema hapa hiyo *production per capita* tunaiongeza vipi ni *Alfu Lela Ulela.* Mimi kwa bahati nzuri silazimishwi na itikadi kusema mambo mazuri, ndiyo bahati nzuri ya kuwa upande huu na mimi ningeweza kusema hapo kwamba naunga mkono.

Lakini mimi naunga mkono kwa sababu hatuwezi tuka-*function* bila sheria, lakini hizi sheria zetu tunazitunga tukizingatia ukweli kwamba zinakuja kutuletea manufaa au tunatunga ili tuonekane tu tumetunga sheria. Hili ningependa niambiwe na kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni mtaalam wa masuala haya yeye atatuambia kwamba kwa uzoefu wake hii itatuondoa katika asilimia hiyo kumi na tano na itatufikisha kwenye asilimia sitini, litakuwa ni jambo zuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio cha Watanzania wengi ni umaskini na kwa kweli umaskini utaondolewa pale tu watakapoweza kuzalisha, lakini kumekuwa na stadi nyingi tu zinazoonyesha kwamba *more and more,* Watanzania wengi wanaoingia katika biashara au kujishughulisha wanakuwa kwenye hiyo *economy* isiyojulikana, kwa hiyo sijui, sasa labda tuendeleze tu kutozana hapa maana yake niliona hata wazo la kusema sasa hata posho zitozwe lililetwa ili kuzidi tu kukamua wale wale ambao wanaweza kukamatika.

Hiyo ni kukiri kabisa kwamba wale ambao wapo kwenye *informal economy* hawapatikani na hata sheria hii haina mikakati yoyote ya kwenda kuwakwamua kule na wamekimbia nini? Wamekimbia kodi hizo za *stamp duty.* Kila siku alipe na mwisho wa mwaka unamlipisha. Sasa mfanyabiashara ana miaka ishirini bado anatembea kwa miguu, ananuka jasho Mjini, kwa nini afanye biashara? Mtu angetegemea kwamba akifanya biashara atanufaika lakini sivyo, kodi ni nyingi na hatutaki kuwa wabunifu katika kuongeza kipato chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia lingine hapa, mimi niliwahi kupendekeza sikumbuki ni lini, nashukuru kwamba Serikali ilisikia hilo. Tulipendekeza kupitia Kamati yetu ya *PAC* kwamba kwa kweli tukitaka kuleta *efficiency* katika ukusanyaji wa kodi ni bora tuondokane na kila Halmashauri kukusanya visenti vyake na mzigo huu ukaachwa kwa *TRA* halafu pesa zikagawanywa kwa uwiano wa maendeleo nchini. Nashukuru, *of course* hilo naona likatumika kama kisiasa kidogo, wakasema ahaa, tunawaondolewa kero. Mimi sidhani kwamba ni kuwaondolea kero bali tunajaribu kuleta *efficiency* kwa nini vijikodi elfu kumi kwa Mtanzania mmoja lakini mpaka sasa sheria hii haituambii kwamba sasa tunataka ku-*harmonize* kodi za nchi. Bado kama ilivyosemekana hapa kuna *Property Taxes* zitakusanywa na Halmashauri na zenyewe ni kodi vile vile ambazo zinamwandama Mtanzania yule yule, lakini zingekuwemo humu zikawa ni kodi zinazoeleweka kutokana na uwiano wa ulipaji kodi watu wengi wangekubali kuzilipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunapenda kulipa kodi, lakini tunakimbia kodi zisizokuwa na kichwa wala miguu. Labda nikifika hapo nijiulize sasa hivi Tanzania tupo katika kipindi cha ubinafsishaji, tunabinafsisha kila kitu, wengine wanasema ni vibaya, lakini mimi nafurahia. Napenda tu uwe ni ubinafsishaji ambao kwa kweli unaangalia maslahi ya Taifa. Tumeona pale ambapo tumebinafsisha vizuri kumekuwa na matunda. Mwanzo ilisemekana kwamba ni bia tu na sigara, lakini sasa hivi inaonekana vitu vingi vinaanza kupatikana na ikiwezekana hata *Net Group* watatuongezea ufanisi wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiisoma *Roman Empire history* na nini utakuta kulikuwa kuna watu wanaitwa *tax farmers* wanapewa kazi hiyo na Serikali wanakusanya kodi *efficiently, sometimes too efficiently* mpaka inaudhi lakini nadhani hiyo ndiyo kazi ya Serikali kusimamia kwamba wasije kuwa *too harsh.* Lakini katika hilo mimi sioni tofauti yoyote na *regime* zetu ambazo mtu anajinyonga ili asimwone mtoza kodi. Nchi nyingi tu mpaka leo duniani zinafanya hivyo *I think hata Mozambique* wanafanya hivyo, sisi wenyewe hapa nchini kwetu tumeweza kufanya hivyo kwenye Halmashauri.

Halmashauri yangu ya Mji wa Kigoma-Ujiji tulikuwa tunakusanya milioni kumi na mbili kwa mwaka, tukajikuta tunakusanya milioni mia tatu kwa kuwapa watu ambao ni *efficient* kwenye kazi zao. Labda na kodi nayo ibinafsishwe, watu wanaweza kuona ni jambo baya lakini mimi sidhani. Tumebinafsisha huduma za maji, huduma zote tu *honestly,* sijui kama nilivyosema kwamba *we are too sure* kwa mfumo tulio nao sasa hivi sheria hii inaweza sasa ikatuondoa kutoka kwenye asilimia kumi na tano mpaka ishirini tunazokusanya kama kodi ya nchi hii au tunakwenda tena kuanza utaratibu mwingine na baada ya miaka mitatu tuje kulaumiana tena hapa kwamba *nothing has happened* pamoja na mabadiliko makubwa kama haya ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nasema basi tuwe kidogo *optimistic,* labda tusibinafsishe *TRA* yote na kuwanyima kazi maana yake tunajua kuna *civil servants* wengi huko, lakini mbona kwenye utaratibu kama wa bandari kwa mfano tumeibinafsisha *Container terminal*, sasa inafanya kazi vizuri kuliko bandari yoyote nyingine Afrika. *Container terminal* tumewapa watu nadhani ndugu yangu mmoja yupo humu, lakini *infrastructure* tumebakia nayo sisi wenyewe.

Sasa vitu kama hivi *Income Tax, Customs* si vinaweza kweli vikatozwa na watu wenye ujuzi na watu wanaoweza kufanya *studies* wakatuambia katika hali ya uchumi wa namna hii sisi tunaweza kukusanya *a certain amount* na wakawa wameiweka pale na sisi tukaanza kutumia kuliko sisi kila siku kuletewa sheria na kubadili sheria ambazo utekelezaji wake hatuna uhakika nao na kwa kweli ni sawasawa na kutoa au kutia mvinyo mpya ndani ya chupa ya zamani. Sheria hii *can you really teach an old dog new tricks,* hana meno, tena miguu imechoka, unamwambia sasa kimbia mkamate swala yule, hamwoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi wazo langu ni hilo kama kweli tunataka kuwa *efficient* tuangalie kwamba kodi ndiyo kiwanda kikuu cha Serikali na kama hatujalifanyia utafiti wa kutosha na kujua tunapata ngapi, tunakosa ngapi na kwa sababu gani, tutaendelea kuwa hivi hivi, tutashindwa kujenga barabara, tutashindwa kufanya nini na jana Mheshimiwa Rais akasema kwa sababu hatuna pesa ndiyo maana barabara ya kule Tunduma-Kigoma itangoja mpaka hizi ziishe kwanza. Barabara ya kwetu Kigoma hakuna lakini huku wanajenga kwa sababu tumewahi kupata pesa. Mimi nasema tunazitaka hizo pesa mwaka kesho na barabara ya Tunduma-Kigoma iwepo kujengwa kama ambavyo zipo nyingine za lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi angalau nichangie machache katika Muswada huu ambao ni muhimu katika maendeleo yetu. Kwanza nataka kusema wazi kwamba nauunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka pia nitumie nafasi hii kwanza kumpa pole Rais wetu na familia yake na Watanzania wote kwa janga lililompata.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitumie nafasi hii pia kuwapongeza Wabunge wenzangu waliopata heshima na nyadhifa mbalimbali akiwemo Mheshimiwa Getrude Mongella, Mheshimiwa Dr. Pius Ngw'andu na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na wengine wote ambao wamepata nafasi. Tunawaombea kila la kheri watuwakilishe vizuri katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nataka nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Basil Mramba, pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya wakisaidiwa na wakuu wao, akiwemo Katibu Mkuu Ndugu Gray Mgonja, pamoja na Ndugu Lyimo na watumishi wote. Naelewa kwamba Kamishna Mkuu Ndugu Kitilya ana kazi kubwa sana, lakini kwa kipindi kifupi ameonyesha jitihada kubwa sana za kufuata nyayo za viongozi wenzake waliotangulia. Tuna imani kwamba ataendelea na jitihada hizo ili angalau hii hali ambayo tulikuwa nayo kwa kipindi kirefu hairudi nyuma tena. Nawapongeza wote kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuunga mkono hoja hii nina mambo machache ya kusema. Kwanza, nataka nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kusikiliza kilio cha wadau, kusikiliza Kamati yetu ya Fedha na Uchumi na kutoa ushauri ambao kwa asilimia kubwa ameukubali. Nimejaribu kupitia katika *schedule of amendment* ambayo aliitoa Mheshimiwa Waziri, nimeona karibu maeneo 120 yamefanyiwa marekebisho. Hii ni heshima ambayo ameitoa kwa Bunge hili kukubali kufanya marekebisho, si kawaida.

Mimi nimekuwa kiongozi wa Serikali sehemu nyingi, huwa wakati mwingine ni wabishi sana. Kubadilisha hata neno moja unaona kwamba inaweza kuleta maana nyingine. Lakini Mheshimiwa Mramba kwa kushirikiana na Mheshimiwa Chenge, Mwanasheria Mkuu wetu wamekuwa kabisa ni mfano mzuri wa kuigwa na wengine. Kama kuna matatizo tunaogopa nini kubadilisha! Hivyo huu ni mwanzo, ndiyo maana Muswada huu kwa kweli sasa hata ile *pressure* ambayo Wabunge walikuwa nayo imepungua sana. Kazi tutakayoifanya sasa ni kushauri yale maeneo ambayo tunadhani ni vizuri tukaona namna ya kuyaboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia imebadilika na sisi lazima tubadilike. Wataalam wanasema kila dakika watu wanabadilika, sisi tuliomo ndani ya Bunge hili tangu tuingie tumeshabadilika hatujui tu. Tangu asubuhi tulipoingia mpaka sasa si watu wale wale tumebadilika, ila tunaona mabadiliko baada ya muda mfupi. Baada ya miaka miwili au mitatu ndiyo maana mtu anasema mwenzangu mbona umezeeka?

Lakini ujue kwamba kila dakika ulikuwa unazeeka na kama unabadilika kila dakika hivyo fikra na mawazo yako lazima pia yabadilike kutokana na mfumo na hali halisi inavyobadilika. Sasa najua kwamba kodi watu hawaipendi, duniani kote watu hawapendi kodi.

Hata mimi ungeniambia mshahara wangu niwe napeleka kila mwisho wa mwezi tungekimbizana hapa. Lakini kodi ina umuhimu wake. Wote tunatoa kodi kwa sababu

tunaogopa tutabanwa na sheria. Ingekuwa ni kila mtu ajitolee kodi anavyotaka tungepata matatizo makubwa sana. Hakuna anayetambua kwamba ni kodi hii hii ndiyo inatusaidia kutuletea maendeleo. Hakuna hata misaada tunayopata kutoka nje isiyotokana na kodi. Ni wachache wanaotambua kwamba ni kodi ndiyo inasaidia kuleta maendeleo. Katika hali hiyo nilitaka nishauri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kodi hii ambayo tunaizungumzia ni kodi ya mapato. Ukiangalia takwimu tulizonazo utakuta kwamba kodi hii inanatupatia karibuni asilimia ishirini au ishirini na tano kati ya kodi zote tulizokuwa nazo. Lakini kwa kweli ukiangalia wanaolipa si wengi, ndiyo maana Waziri amekuja na hoja ya kwamba kwa nini sasa asipanue wigo.

Lakini tunapozungumzia juu ya kupanua wigo ni akina nani hawa unataka kuwaongezea kodi. Hapo ndiyo tatizo linaanza. Mimi nataka kushauri tukitaka kupanua wigo yapo mambo matatu muhimu lazima tuyafanye. Kwanza, lazima tuhakikishe tunawawezesha wananchi wetu ili wawe na uwezo wa kulipa kodi. Huwezi kumwambia mwananchi alipe kodi wakati hana hata uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tulikuwa tunashangaa, katika maeneo yetu kuna hii inaitwa *Property Tax,* ni kodi ya nyumba. Leo mzee wangu ambaye amerithi nyumba hiyo kutoka kwa babu yake na mtoto amerithi kutoka kwa baba yake na mjukuu atakuja kurithi kutoka kwa wazazi wake ambao hawana hata kipato, unamwambia utalipa *Property Tax* ambayo ni sawa labda na shilingi ishirini elfu kwa mwaka na hela zenyewe hana.

Sasa ili aweze kulipa lazima umsaidie huyu apate hela. Kwa wakulima wetu ambao ni wengi katika nchi nyingi kwa kweli sisi tungetegemea watoe fedha nyingi sana kuchangia uchumi, lakini ukiangalia mahesabu yanavyokwenda kilimo ambacho kilikuwa kinaongoza kutoa pato kubwa la Taifa sasa kinazidi kuporomoka. Viwanda ndiyo vinakuja, biashara za madini zinakuja, utalii unakuja juu, wakulima wanazidi kuporomoka, hali hiyo siyo nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali siyo nzuri kutegemea mashirika machache ndiyo yaendeshe nchi hii, yakija kukwama au wakiondoka ndiyo mwisho wa uchumi wa nchi hii. Lazima tuwe na wigo mpana wa wananchi wetu wenyewe ndio waweze kuwa na uwezo wa kuendeleza na kulipa kodi nzuri kwa maendeleo ya nchi hii. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano, mkulima ukitaka kumwezesha mpe pembejeo. Atakuwa na uwezo wa fedha na atalipa kodi vizuri, lakini pembejeo anapata namna gani. Tunaiomba Serikali iangalie upya utaratibu mzima wa jinsi mbolea inavyoingia katika nchi hii. Kuna wafanyabiashara wanapata faida kubwa sana kwa kumwumiza mkulima kwa kumtoza bei kubwa sana ya mbolea.

Bei ya mbolea sisi tunavyofahamu ni ya chini sana, lakini kwa sababu kuna upungufu watu wanatumia nafasi hiyo kuwalangua wakulima kwa kuwauzia shilingi thelathini elfu kwa mfuko mmoja badala ya shilingi kumi na tano elfu.

Mkulima huyu ambaye tulitegemea sasa awe na uwezo wa kulipa kodi unazidi kumpunguzia uwezo wake na hii hali ikiendelea mkulima ataendelea kuwa maskini kama kwa makusudi kabisa hatutamsaidia na hasa kwa pembejeo. Tunataka kwa makusudi mazima Serikali iingilie kati taratibu zote za pembejeo kwa ajili ya wakulima, wavuvi na wafugaji. Tunaomba bei za pembejeo zisimamiwe vizuri ili haki itendeke na hapa ndiyo tutapanua wigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi hawa wengine maskini ya Mungu! Leo nilikuwa naangalia marekebisho Mheshimiwa Waziri ambayo wafanyakazi wamelalamika, wengine wametuletea barua hapa ya kwamba tunataka wakatwe kodi kwenye posho wanazozipata. Kwanza kodi za kwenye posho zingeongeza kiasi gani? Kwa kweli ukiangalia kodi ya kwenye posho ingeongeza kiasi gani? Hivyo, Mheshimiwa Waziri nataka uliangalie suala hilo badala ya kukazania hizi kodi ndogo ndogo za kwenye posho na za kwenye usafiri ambazo nashukuru umeanza kuziondoa. Sasa tuangalie kuwawezesha wananchi ili wawe na uwezo wa kulipa kodi. Na mimi nakuhakikishia kwamba tukipanua wigo badala ya asilimia 20 tu wanaolipa kodi ya mapato katika nchi hii, tukiingiza angalau asilimia 50 mpaka 60 na 70 utashangaa nchi hii itakwenda vizuri sana na hatutaendelea kuwategemea watu wa nje watusaidie. Watu wa nje jamani kutusaidia ni kwa muda tu, wakiamua *we don’t want* tumekwenda na maji. Sasa tusiendelee na utaratibu huo lazima tubadilike. *(Makofi)*

La pili, Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba sana utaratibu mzima wa kukusanya kodi lazima tuuangalie upya. Tunaongeza wigo lakini lazima tuwaongezee uwezo wenzetu wa *TRA* uwezo wa kukusanya, tena kukusanya bila upendeleo wowote, kuhakikisha haki inatendeka kwa kila mtu. Kuna wafanyakazi na wafanyabiashara wengi sana wametoroka katika baadhi ya miji, taarifa tunazo. Walio wengi wanakimbilia Dar es Salaam. Kuna nini Dar es Salaam? Katika Mikoa, wafanyabiashara wanazidi kupungua kwa kuogopa wanabanwa sana kuliko wanavyobanwa wa Dar es Salaam, hivi hii ni haki! Miji mingine ikose wafanyabiashara kwa kuogopa kubanwa au ni kwa ajili ya viwango tunavyowawekea katika Mikoa yetu kuwa ni vikubwa, hivyo wanasema hawa wachache waliopo lazima wafikie viwango hivi? Lazima tuliangalie upya ama sivyo tunaweza kuua hali ya ushindani ambao ni wa haki na usalama kwa watu wetu. Lazima tuangalie hilo.

Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou pale amezungumzia baadhi ya viongozi wengine wamesababisha watu wakajinyonga katika baadhi ya maeneo kwa ajili ya kodi. Lakini tunadhani kwamba ni vizuri tukafanya uchunguzi tatizo liko wapi? Ni vizuri tukawa na utaratibu wa kukusanya kodi kwa kutumia Sayansi na Teknolojia. *(Makofi)*

Nchi nyingine ni *computer* tu zinafanya kazi, hakuna kuonana mtu na mtu, ni *computer* tu, utalipa kwa *computer* itakuletea madai kwa *computer.* Lakini mambo ya kukutana tena kwenye vilabu vya pombe, mnadaina kodi ndiyo tunakuwa tunaingia

katika mambo ya rushwa na hii itatuharibia. Tunakokwenda katika ulimwengu wa Sayansi na Teknolojia lazima na sisi tubadilike kidogo. Utaratibu wetu wa kukusanya fedha uwe ni utaratibu wa haki bila kupendelea mtu yeyote na uwe wa manufaa kwa maendeleo yetu. *(Makofi)*

Mwisho, kwa sasa tabia imezuka ya baadhi ya wafanyabiashara kuanza kutoa taarifa ambazo si sahihi na nawatoa taarifa ambazo si sahihi kwa kuogopa watakuja wabanwe katika kodi na Watanzania hawajajenga uzoefu wa kudai risiti kwa kila kitu wanachonunua. Hata risiti hiyo unayopewa unahakikishaje kama ni ya kweli au ni risiti ambayo wametengeneza vitabu vingi ili huyu mtu akwepe ile kodi. Ndiyo maana nasema kwamba ni vizuri tukawa na utaratibu wa kuhakikisha kwamba unajua biashara fulani mpaka biashara fulani kodi yake itakuwa wastani ni huu ili mtu asianze kubabaishwa kama mwaka jana alitoa kiasi fulani, mwaka huu atakubana kiasi fulani. Hivyo, kinachotakiwa sasa ni kuwa na timu ambayo itafanya kazi ya kuzunguka na kuona maeneo ya biashara na viwango ambavyo vingetakiwa vitolewe na viwe wazi kwa kila mtu bila kuficha ili kila mtu ajue kwamba mimi jukumu langu ni hili. Kila mtu akijua jukumu lake atatekeleza wajibu wake kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwaomba wenzetu upande wa *TRA* waandae mfumo kwa sababu wigo wa ukusanyaji wa kodi utaongezeka na sasa mfumo lazima uendane na utaratibu huu mpya ambao unakuja ili watu wakionekana wako wengi lakini wafanyakazi ni wachache, tunaweza kupata matatizo ya kurudi pale pale tulipokuwa. Mheshimiwa Waziri nina imani kabisa utatupa maelezo machache baada ya kuleta *Amendments* zote hizi kama zitakuwa na *effect* kubwa sana katika matarajio yako ya makusanyo ya fedha. Kwa sababu kweli ukiangalia tutakuwa tume-*affect* sana makusanyo katika utaratibu huu wa *Amendments* ambazo zimekuja. Tuna imani utajaribu kutafuta nafasi ya kuweza kuelezea kwa ufupi utaratibu ambao unaweza kuwa ni mzuri ili kukamilisha matarajio ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nataka nikushukuru tena, nataka nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake yote na ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba na mimi niwapongeze ndugu zetu humu ndani waliopata nyadhifa mbalimbali kama vile Mheshimiwa Getrude Mongella, kuwa Rais wa Bunge la Afrika, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kuwa Rais wa Baraza la Mazingira na Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, kuwa Rais wa Mawaziri wa Elimu wa Afrika. *(Makofi)*

Lakini pia napenda nitoe pole nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, na nawaomba Watanzania wote waendelee kuzidi kumwombea ili apate nafuu kabisa na apate nguvu za kulihudumia Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Muswada huu ni kukuza uchumi na ku-*encourage investment* pamoja na kuhakikisha kwamba kodi zinazopatikana zinaendelea

ku-*stimulate investment* pamoja na kuangalia uchumi wote kwa ujumla wake, na kwa hiyo zile ambazo zitaweza ku-*stimulate investment* kodi hizi zinaendelea kupunguzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la *Registration* ya hivi sasa ni mpangilio wake mbaya hii ambayo tunafuta sasa *Inefficient Organizations.* Kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi tulipokuwa tukizungumzia Muswada huu tuliangalia mpangilio wake, ueleweka wake pamoja na jinsi ulivyo-*effective,* na tukaona kwamba yote haya yanawezesha wadau wengi kuuelewa vizuri zaidi na hivyo kuelewa matumizi ya Muswada vizuri zaidi, lakini pia tukasema ni vyema upunguze nafasi kwa watoza kodi kumhisi mlipa kodi kwa kumtoza kodi kutumia sehemu au vipengele vingine vya sheria kwa sababu nyinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake nzima, Katibu Mkuu, Manaibu Mawaziri, Kamishna wa *TRA* na timu nzima ya *TRA* kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wanaifanya. Kwa kweli tulipata ushirikiano mkubwa sana kutoka kwao katika Kamati ya Fedha na Uchumi na kwa hiyo ninachokitegemea ni kwamba tutakuwa na *a maxim improvement* kwa Muswada huu ambayo itaweza kusaidia huko siku zijazo iweze kufanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo bado yapo matatizo mengi. Moja, ni lile linaloliita *cross referencing, in particular* katika sehemu nyingi za Muswada wenyewe ambazo ni *fairly publicizing to even a good tax practitioner* na ni matumaini yangu kwamba tatizo hili la *cross referencing litapu*nguzwa na ile tuliyosema *practice notes* ambazo ni vyema ikiwezekana kila Mbunge azipate tuzitumie katika Majimbo yetu, na naomba wajitahidi kuziandika kwa ufasaha zaidi ili wafanyabiashara walio wengi waweze kuzielewa na kuzitumia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala moja ambalo napenda tujiulize wote humu ndani ni kwamba h*ow effective is proposed income tax Registration in implementing the desired Policy.* Kwa mfano, unapoangalia kipengele cha *Employment Income* na jinsi kodi inavyofanywa kwa mtumishi wa umma, hivi sera ilikuwa nini? Ilikuwa ni ku-*maximize the tax take from the narrow reachable employment tax payer base* na kwamba *would surcharge a tax structure assist employers in attracting and retaining competent staff.* Je, huu utaratibu uta-*support gross* ya *employment opportunities* katika nchi ambayo watu wengi wanaomaliza Vyuo, wanaomaliza shule hawana kazi. Masuala haya ni muhimu na ndani ya Kamati ya Fedha na Uchumi haya tuliyajadili kwa kina sana. Namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba baadhi ya vipengele katika hili viweza kufutwa. *(Makofi)*

Hata hivyo, bado *circumstances* zinazohusu *Employment Income* inaonekana kama ni *over tax* kwa sababu *assumption* nyingi za misingi ya kutozwa kodi *Employment Income* zinaonekana kwamba bado *unreal* kama tungeweza kuchambua moja baada ya nyingine kama nadharia inavyoeleza. Lakini pengine sitakuwa na muda wa kuyaangalia yote haya.

Lakini niseme tu kwamba Taxation Employment need to support gross objectives, na kwamba hii keki tunayoiangalia ambayo lazima tui-tax tunahitaji kuifanya iwe kubwa zaidi, ikishakuwa kubwa ndipo tuanze kuitoza kodi. Hivi sasa hao wafanyakazi tunaowaangalia kwamba ndiyo watakwenda ku-*support others sectors* ziweze kukua pato lao ni kidogo sana. Matokeo yake ni kwamba hao wachache wanakuwa push into *poverty,* na tuona katika *sectors* mbalimbali umaskini umekuwa ukiongezeka Vijijini na Mijini, ombaomba sasa wamekuwa wengi. *(Makofi)*

Utaratibu tunaoufanya huu wa *comprehensive reform of tax policy* na ku-*widen tax base* bado ni mdogo. Bado mimi nafikiri kwamba inadequate na pengine Tanzania ndiyo nchi pekee ambayo inatumia fedha kidogo kwenye sectors muhimu kwa maendeleo ya nchi na kwa uwezekano wa kupunguza umaskini. Kwa mfano, elimu Tanzania tunatumia shilingi 13,000/= kwa kila mtu kwa mwaka na kwenye afya ni fedha kidogo zaidi tunatumia shilingi 5,500/= *spent on health per person per year.* Lakini bado iko ile *donor syndrome* ambayo iko. Mfumo huu wa kodi ni lini utatuondolea utegemezi kwa wafadhili? Hivi sasa *domestic revenue at the percentage of domestic expenditure* ni 53 peke yake. *The rest forty seven percent is shared by donors.* Ni dhahiri kwamba kama mipango yetu ya kodi haijielekezi katika kuondoa utegemezi huu, hata mafanikio tuliyoyapata katika *reform process* yetu yatakuwa *highly unsustainable.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria yoyote ya kodi ili ipate *compliance* ni lazima iwe *rational, transparent and equitable.* Sasa napenda kuuliza *is this true* katika Muswada huu, matumizi ya maneno mengine katika *Bill* hii, kwa mfano, *associate broadly defined is considered as being very futile for conflicting interpretation by tax officials,* akalitumia tu anavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama nilivyosema tunashukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yake, tumepata ushirikiano mkubwa sana katika Kamati ya Fedha na Uchumi. Lakini ziko *challenges opportunities* katika *transaction* ambayo tunayo. Sasa napenda niseme kwamba *Tanzania has moved from situation where the Government virtually controlled every aspect of the economy to one where decisions occur through markets,* haziko nchi ambazo zimepitia hiyo. Lakini ushauri mwingine ambao tunaupata kutoka kwenye *market fundamentals* ambao wana *-preach the use of simplified version of market economies zinazo-pay scant attention to the dynamic of change.* *(Makofi)*

Sasa katika kutekeleza haya tunayapata matatizo mengi sana. Katika kushughulikia uchumi wa nchi yetu. Tunayo mabenki ambayo *I can only explain it in English they don't govern savings.* Tulikuwa Mashirika mengi yakizalisha mali lakini mengi hayafanyi maamuzi juu ya nini wazalishe, walikuwa wanazalisha walichoambiwa na nyenzo kutoka nje kama vile *raw materials, labour na machines* tunazopewa toka nje. Sasa pengine ni vyema tukaelewa kwamba *a real and effective banking system requires strong banking regulations. New forms need to able to acquire land and these requires and land registration.* Haya yatasaidia kupanua wigo pamoja na kuongeza kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii iwe na nafasi nzuri kuona tunapokwenda na tunapotoka. Nchi yetu inatekeleza mambo mengi tunayoambiwa *IMF* na *World Bank,* kama vile tume-*liberalize if not completely but achieved partial, macro stability inflation rate brought down dramatically,* na tume-*privatize significantly*. Lakini *proceeds* za Mashirika haya zaidi ya robo tatu pengine hazijaingia kwenye *offer,* Serikali na Mashirika haya mengi hayafanyi kazi. Na mimi ningetegemea baadhi ya Mashirika haya ndiyo yangekuwa yameongeza kodi ya nchi hii kwa kiwango kikubwa. Kiasi ambacho tumepata kutokana na Mashirika yaliyouzwa ni kidogo sana. Haya Mashirika watu wamenunua ni kama wamekaa na mali, wengine wamekuwa wanauza. Sasa haya yote yanatuweka mahali pabaya.

Mheshimiwa Naibu Spika*, of course it is easy to privatize quickly if one does not pay any attention how one privatizes, essentially give away valuable State property through various means.* Profesa Joseph Stigiris anasema *and I quote: "Indeed privatization can be highly profitable for governments to do so, whether the kick backs come back in the form of cash payments or in campaign contributions or both, these policies emphasis foreign direct investment that demand for higher returns to compensate them for bringing in capital."* Tanzania imekuwa *under pressure* kutoka *IMF* na *World Bank* ku-*privatize rapidly, turned over to state assets for the piteous and this had been done without putting in place an effective tax system in place.* Tunachotakiwa kujiuliza hapa ni kama a *powerful class of businessman* tulionao wanalipa kodi sawasawa au la na ni kodi kiasi gani wanadaiwa. Tunataka hawa walipe kodi. *(Makofi)*

Mwisho, Naibu Spika, ni sera ya kuwezeshaji *(Empowerment Policy).* Jambo hili tulimwuliza Mheshimiwa Waziri katika Kamati ya Fedha na Uchumi kwa nini sheria imecheleweshwa. Mheshimiwa Waziri alijibu kwamba imecheleweshwa Waziri Mkuu ndiyo mhusika mkuu wa masuala ya uwezeshaji. Lakini mambo ya kila siku yanafanywa na Waziri wa Viwanda na Biashara, Waziri wa Fedha aliongeza kwa kusema kwamba upo ucheleweshо na akaahidi kwamba yeye ataanza kuchomoa mambo fulani fulani muhimu kutoka kwenye sera ya uwezeshaji ayalete hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Juni, wakati wa bajeti alitoa mfano wa uwezeshaji kama vile *withholding tax on lease aircrafts.* Sasa hawa ni watu wachache sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa taarifa yake nzuri na hiyo *perception.* Lakini tunachosema sera ya uwezeshaji ni suala ya walio wengi siyo sera ya Watanzania 100, 50 au 10. Tunataka sera itakayowagusa wakulima wetu wadogo wadogo, wachimbaji madini wadogo wadogo, wafanyabiashara wadogo wadogo, wavuvi na wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili linahitaji kufahamu kuna tatizo gani na ni nini? Nahisi lipo tatizo na ni vyema tuelezwe hapa ndani ya Bunge. Mwezi Juni mwaka huu wakati wa bajeti tutaomba maelezo sahihi na kwa nini Serikali inapata kigugumizi kulileta humu ndani ya Bunge? Lazima tuelezwe kwamba kwa kutoleta sheria hii ya *empowerment, we are continuously under value capacity* ya watu wetu na kuwa *marginalize* zaidi.

Kwa mfano, kwa nini baadhi ya makampuni hapa ndani yanafanya biashara kuanzia ya kuuza matairi, kuuza chakula, mpaka na kuziba pacha wakati Watanzania wapo, Watanzania watafanya nini? *We are continuously going to become beggars in our country and I think we should be right in our own approach* kama Waheshimiwa Wabunge tunaowakilisha watu maskini. Tuendelee kulinda hadhi yetu maana haya ndiyo mambo muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sidhani kama unaweza kutoza kodi watu wanaoendelea kuwa maskini tu, maskini tu, ndiyo maana naendelea kuyasema haya. Maana haya ni msingi kutuwezesha sisi, kisha na sisi to contribute kwa maendeleo ya Taifa letu.

Lakini huyu mfanyakazi wa Serikali ambaye yuko kwenye tax net yaani kwa sababu yupo tu yeye mwenyewe atakuwa maskini na akitoka pale yuko hoi na tumepata mifano ya wafanyakazi wengi ambao ni maskini na hawana uwezo wa kufanya chochote, hivi sasa tunavyozungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote ni hatari kwa Watanzania walio wengi. Ninachokiona ni wengi pamoja na sisi wenyewe kuwa *beggars in our own country.* Sasa yote haya naomba yawe ni mchango ambao utaweza kusaidia kukuza uchumi wa nchi hii. Maana ndiyo msingi wa Muswada huu tunaozungumzia.

Pengine ule uchambuzi wa kina tumesema tunahitaji uendelee kuwa katika mabadiliko kupata *constant changes,* na hizi zitatusaidia sisi kutuelewesha zaidi mapungufu ambayo tunayo ili tufike mahali tuseme na sisi tuna-approach hayo mengine ambayo wenzetu wanayafanya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tumesema Mtanzania akiwa na nyumba tatu, mmoja aachiwe akitaka kuuza auze, suala linakuwa eti tutajuaje kwamba hiyo nyingine atakayokuja kuiuza siyo yake. Ni kwamba tunahitaji kufanya research zaidi tuelewe hawa tunaowatoza kodi. Maana hata tufika mahali itabidi tuendelee hata kuwalinda hao wafanyakazi wetu.

Hivi wewe unalipa kodi, unalipia watoto wa shule 10, hawa 10 wakiacha kusoma kesho Taifa si litapata hasara, kwa nini huyu asipate *tax deduction* akasamehewa kodi, kwa sababu anasomesha watoto, maana hana uwezo mwingine wa kupata fedha atakayokwenda kumsomesha huyu mtoto mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ili nitoe mchango wangu kuhusiana na Muswada huu wa Kodi ya Mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Manaibu Mawaziri wake na watumishi wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri waliyofanya. Ni kazi kubwa sana. I japokuwa mimi siyo mtaalam wa sheria za kodi, lakini Muswada huu unaeleweka vizuri zaidi kuliko ile sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 1973. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia kwa njia waliyotumia katika kutafuta maoni ya wadau. Muswada huu umekaa muda mrefu sana katika Tovuti. Yeyote aliyekuwa na interest ya kuufuatilia, pamoja na matangazo yaliyotolewa kukaribisha watu waufuatilie na watoe maaoni yao, hakuna mtu anayeweza kulalamika leo kwamba hakupewa nafasi ya kutoa mawazo yake.

Ninaomba huo mfano uigwe na Serikali nzima, Miswada itolewe na iwekwe kwenye Tovuti kwa muda mrefu kadri iwezekanavyo na wananchi waarifiwe juu ya kuwepo Miswada hiyo. Hivyo tunaweza labda tukaepuka matatizo ya malalamiko ya watu ambao watakuwa wanasema hawajakuwa-*consulted. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kodi ni suala ambalo halina ubishi, hata kwa sisi waumini wa dini ya Kikristo Bwana Yesu alipoulizwa na wale jamaa waliokuwa wanamtega: Je, ni halali kumlipa Kaisari kodi, Bwana Yesu alijibu: "Mpe *Ceasar* yaliyo yake *Caesar*," akiashiria kwamba lazima tutekeleza wajibu wetu kwa Serikali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili linatambuliwa na Ibara 138(1) ya Katiba ya nchi yetu ambayo inatoa mamlaka ya kutoza kodi na mamlaka ya kutoza kodi yako mikononi mwa Bunge lako Tukufu kwa kutunga sheria kama hii tunayotunga sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi ya mapato haitozwi kwa mara ya kwanza sasa, imetozwa muda wote ambao tumekuwa na Serikali katika Tanzania. Kitu ambacho Muswada huu unafanya ni kuboresha ile sheria ambayo inatumika katika utozaji wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa ni muhimu hili jambo lifanyike kwa sababu tumetoka kwenye zile enzi za uchumi hodhi na tuko sasa kwenye enzi za uchumi unaoendeshwa na watu binafsi. Utozaji wa kodi ya mapato zamani mara nyingi ulikuwa unaegemea wafanyakazi. Kulikuwa na njia ya moja kwa moja ya kuwatoza kwa kutumia *procedure* za *withholding*.

Lakini kwa sasa kwa ajili ya uchumi ambao ni *private* na uwekezaji wa watu binafsi lazima *approach* ya utozaji wa kodi uwe tofauti na ile iliyokuwepo hasa kwa sababu *Private Enterprise* ziko nyingi zaidi ya zile ajira ambazo ni *formal.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyosema Muswada huu kwa ujumla hauna matatizo. Matatizo ambayo yameonekana ya kiuandishi ni matatizo madogo sana ukilinganisha na kazi ambayo Muswada huu unafanya. Yapo matatizo ya kiuandishi ambayo yanaweza yakasahihishwa tu kirahisi.

Mfano ulioonyeshwa kwenye kifungu cha 21(1) cha hii sheria ni wazi kwamba kwenye kile kifungu kidogo cha kwanza, aliyeandika alikuwa anataka kusema *Accounting.* Kwa sababu hivyo vifungu vinavyofuata vyote vinasema *Accounting* na *marginal notes* zinasema *Bases of Accounting for Income.*

Kwa hiyo, hii mimi nasema ni zile *accidental omission* ambazo ikiwa Serikali imezionyesha, hakuna sababu ya kung'ang'ania maneno ambayo yataleta ubishi baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mawazo ya ujumla ambayo yanahusiana siyo tu na hii kodi ya mapato ila na kodi zote ambazo zinatozwa kwenye nchi hii. Utaratibu mzuri wa utozaji kodi ni ule utaratibu ambao unafanya mtu alipe kodi kwa hiari na siyo ashawishike kukwepa kulipa kodi.

Kwa hiyo, utozaji wa kodi kuzidi kiwango cha watu wanachoweza kulipa au utozaji wa kodi kwa njia ambayo mtu anaona anaonewa na kushawishika kukwepa ulipaji wa kodi, hiyo haitakuwa ni sheria nzuri. Kwa hiyo, kwa mawazo yangu yapo mambo matano ambayo ninaomba Serikali iyazingatie wakati wa kutekeleza hii sheria mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kwa wale wafanyabiashara ndogo ndogo tu, siyo watu wa kule vijijini hata sisi ambao tumekwenda shule na tumeelimika sana, sheria ya kodi ni ngumu sana. Hata sisi wengine tunashindwa kuitii kwa sababu hatuielewi sawasawa. Siyo kwamba tunakwepa kwa makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningeomba Serikali pamoja na jitihada za kile kitengo cha Elimu ya Kodi kwa Umma kufanya kazi nzuri, itambue kuwa matangazo ya Redio, ya Televisheni na ya magazeti tu yenyewe hayatoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba juhudi kubwa zaidi zifanyike katika kuelimisha umma siyo tu juu ya wajibu wao wa kulipa kodi bali pia juu ya namna ya kulipa kodi iliyo halali na iliyo sahihi. Mimi naamini sana kuwa mfanyabiashara yeyote akiweka vitabu vyake vizuri kodi haiwi ni mzigo mzito. Kodi inakuwa mzigo mzito pale ambapo vitabu vyake haviwekwi vizuri. Lakini ni wachache sana kati yetu ambao tunaweza tukaweka vitabu vyetu vizuri.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara ifikirie utaratibu, na sasa hivi kuna *computer programmers* wazuri kabisa, kututengenezea *computer program* ambayo wafanyabiashara wadogo wadogo na yule mtu anayetaka kuitumia aweze kuitumia. Hiyo *computer programme* iuzwe. Itarahisisha masuala ya kuweka mahesabu, masuala ya kuweka *returns* na ukaguzi wakati watu wa kodi watakapotujia. Mimi nafikiri ni gharama ambayo itakuwa inatumika kihalali ikiwa hiyo programu itakuwepo *unique* kwa *taxation system* ya nchi yetu. Sio lazima mtu aende akachukue programu inayotumika Uingereza au programu inayotumika na Mashirika makubwa kwa ajili ya biashara ambazo zina *turnover* ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri tunakwenda kwenye zile zama za sayansi na teknolojia katika kufanya biashara. Kama imeweza ikatolewa maelekezo kwa ajili ya

masuala kama *VAT* wafanyabiashara watumie zile *cash registers* hakuna sababu kwa nini kusiwe na utaratibu wa kuwa na hizo *programs.* Tuuziwe sio kwamba tupewe bure. Jambo la pili, nililokuwa nataka kupendekeza na kwamba Serikali ilizingatie ni kwamba kwa sasa sio wote lakini kuna wachache kati ya wakusanyaji na wakadiriaji wa kodi ambao wanafanya kazi yao kwa njia ya ku-*harass* au kunyanyasa walipa kodi. Mahesabu yanakwenda yanarudi bila maelezo. Wanakuja kukagua mahesabu ofisini wanakuwa kama ndio Polisi amekuja na warrant wa kukamata. Mimi nafikiri mlipa kodi anatakiwa ashauriwe na aelimishwe zaidi kuliko kuwa harassed. Tunaomba kwa wale wakadiriaji na wakusanyaji ambao wana tabia ya ku-*harass* walipa kodi wajue kwamba kama sio walipa kodi Serikali haingeweza kufanya kazi. Kwa hiyo *actually* wanatakiwa waheshimiwe hata kama wako kwenye *default,* mwenye deni hauwawi na ndio utaratibu wa madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, naomba Serikali ijaribu ku-*devise* njia ambayo *assessment* ya kodi na ukusanyaji wa kodi uweze kumsaidia mfanyabiashara mlipa kodi kuendelea na ile kazi yake sio kufilisika. Kuna wafanyabiashara wengi sana wameamua kufunga biashara zao kuliko waendelee kulipa kodi. Hii hasa inatokea kwenye zile biashara ambazo zinakadiriwa kama biashara za maduka, biashara ndogo ndogo, biashara za mabaa, biashara za migahawa watu wanakuwa *assessed* wanaona faida wanayopata haitoshi hata kufidia zile *operating costs.* Sasa naomba utafiti ufanywe vizuri zaidi katika kufanya hizi *assessment. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna wafanyabiashara wakubwa ambao wanatumia Wamachinga kukwepa ulipaji wa kodi. Wale vijana ambao wanatembea mchana kutwa hawanywi maji wala hawali actually wanafanya biashara za wakubwa. Naomba Idara ya Kodi nayo ichunguze hili na iweze kuhakikisha kwamba huu mwanya wa kukwepa kodi unazibwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine naomba ufafanuzi kuhusu baadhi ya vifungu. Kwa sababu nimepigiwa kengele nitakwenda haraka. Kifungu cha 16 ambacho kinasema "Mlipa kodi atapunguziwa kodi kwa kile kiwango ambacho anakitoa kama mchango wake kwenye religious institutions.

Naomba nipate ufafanuzi je nikilipa zaka au sadaka Kanisani mwisho wa mwaka naweza nikatoa mahesabu niliyolipa? Na hiyo haingilii zile amri kwamba nikitoa kwa mkono wa kulia mkono wa kushoto usijue? *Section 64* nilivyoisoma nimeielewa kwamba Mashirika ya Dini yachukuliwe kwamba yanafanya biashara kwa hiyo yakatwe kodi. Je, hii ina-*involve* hata kuwakata kodi kwa sadaka na zaka ambazo waumini wao wametoa? Kama ni hivyo mimi nafikiria hilo sio jambo la busara. La tatu, Mawakili kulipa kodi *on cash basis accounting.* Na-*declare interest* mimi ni Wakili. Tunapokea *deposits* za wateja wetu, tunakaa na kesi miaka 6 ndipo tunakuwa na haki ya kuchukua zile *deposit* na kuziweka kwenye *Advocate's account.*

Sasa ikiwa nitatozwa kwenye *cash basis* nitakuwa mimi ninalipa kodi kabla sijapata income. Kwa hiyo, naomba Idara ya Kodi pia ifikirie jambo hilo. Napongeza Serikali katika Muswada huu ku-*clarify* juu ya ulipaji kodi wa *partnerships* ilikuwa

inatukera sana. Kifungu cha *35 "Tax Avoidance Arrangement"*. Naomba Serikali ifikirie juu ya wale wawekezaji wanaokuja wanapewa *Tax holiday* halafu kabla tu ya ile *Tax Holiday* kwisha wanauza ile biashara na yule anayenunua anategemea tena apate *Tax Holiday.* Tunaibiwa mali yetu kwa hii *Tax Holiday.* Naomba hiyo iwe *reviewed* na ikiwezekana kuwe na *regulations* kwamba ukipewa *Tax Holiday y*ule anayenunua ile biashara ile *Tax Holiday* inakuwa imesham-*cover.* Kwa hiyo, ikiwa ni kipindi ambacho kimefika kwamba anaweza akalipa kodi basi yule atakayenunua ile biashara asiwe *entitled* kwa *Tax Holiday* ya pili. Naomba ni-*comment* juu ya kifungu cha 124 kwamba *assessment* ikishatolewa una uhuru wa kufungua rufaa yako, una uhuru wa kutoa *objection* lakini hiyo haisimamishi utekelezaji wa *collection.* Mimi nafikiria hiyo inaondoa ile nia ya *appeal.*

Sasa kama mimi niki-*object* au niki *appeal* bado Kamishna atakuwa na haki ya kukusanya, hakutakuwa na haja ya ku-*appeal* basi na isitoshe sheria ya *Tax Appeal Tribunal* inavyosema nikitaka ku-*appeal* lazima ni *deposit* pesa *one third.* Hiyo ina maana kwamba mimi nitashindwa kwenda ku-*appeal* kwa sababu nikiwa *assessed* pesa nyingi ambazo sina *automatically* sutaweza kwenda ku-*appeal.* Kwa hiyo, naomba kifungu cha 124 kifikiriwe ikiwa ku-*appeal* na mtu anaomba asimamishiwe utekelezaji wa *collection* iwe ni haki yake wasubiri ku-*collect* mpaka wakati ule ambapo uamuzi utakuwa umefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo niliyoyasema naomba niseme kwamba naunga mkono hii hoja mia kwa mia na nampongeza Waziri na wenzake. Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Nataka niseme toka mwanzoni kwamba kwa kuwa nimeisoma sana kwa makini hoja hii naunga mkono toka mwanzoni kabisa. Nitakayoyasema haya nitakuwa najaliza lakini nimeunga mkono toka mwanzoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo machache ambayo mimi nataka nisaidie kuchangia ingawa wenzangu wengine wameyasema kwa hiyo nayaacha. Lakini kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na wasaidizi wake na wataalamu, Manaibu wake wote wawili kwa jitihada ambayo kwa kweli wameifanya sana katika kuongeza mapato katika Hazina ya nchi yetu. Kazi wanayoifanya ni kubwa na matokeo tumeyaona kwamba tumeweza kukusanya kodi nyingi na imetuwezesha kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, tunampongeza sana yeye na wataalamu wake. Niwapongeze zaidi hasa wa *TRA* nao wamefanya kazi yao kwa uadilifu mkubwa. Vile vile Menejimenti nao wamefanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi ninasema mambo machache tu kwanza ukusanyaji wa kodi katika nchi zote unapaswa kufanywa kisayansi. Ukifanya kienyeji hata ukiweka mbinu namna gani watu nao wanatafuta njia zao. Kila ukigundua mbinu na wao wanaotaka kukwepa wanagundua mbinu. Wapo vijana ambao wanaweza wakawa wanakusanya kodi lakini kwa kutumia vitabu vyao tu ambapo Hazina inakosa mapato. Wako vijana wajanja sana. Iwapo watu wanaweza kuigiza kutengeneza noti

kwa nini watashindwa kutengeneza kitabu cha risiti tu ambacho ni rahisi sana. Lakini wapo watu ambao wanaweza wakatumia mianya kukusanya mapato ambayo yanakwenda mfukoni kwao na Serikali ikapata kidogo. Ndiyo maana nikasema ni vizuri kukusanya kisayansi. Kwa hiyo, nafikiri Waziri na Wizara yake watakuwa na mbinu ya kuhakikisha kwamba kisayansi wanakusanya kama mtu anaiba basi iwe ni kidogo sana. Hilo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, mimi nilikuwa napata taabu nasema hivi kuna risiti ambazo watu huwa wanapewa wanaponunua vitu. Ukienda hasa nchi za wenzetu kila ukiingia kwenye duka huwezi kuondoka na bidhaa bila kupewa risiti. Lakini nikiongea na wenzangu hawa waliosomea mambo ya fedha wanasema risiti hizo unapopata risisi unaponunua zinasaidia sana mapato ya Serikali. Nafikiri ndio kweli Prof. Mporogomyi, alinifundisha hilo.

Sasa sisi katika nchi yetu risiti ni kitu kama ambacho hakina maana yoyote. Mtu anakwenda kwenye kituo anajaza lita 160 anaondoka. Risiti Mzee aah acha tu. Sasa, mimi nadhani kuwe na mkakati kabisa au kuwe na sheria na kadhalika, kusema kwamba lazima mtu adai risiti. Hiyo watu walazimishwe na wakikosa waelimishwe, kuwepo na usimamizi kwamba watu wanadai risiti. Kwa sababu kama kweli risiti kupata kwake *according to* Prof. Mporogomyi alivyokuwa ananieleza kwamba inaingiza mapato basi risiti zidaiwe kwa maana kama sisi na watu wengi mbalimbali tuko *busy* tunaacha kuchukua risiti basi tunaibia Serikali, sisi wenyewe. Kama hatuwezi kudai risiti na kumbe risiti ile ingedaiwa ingemfanya yule bwana biashara alipe kule kwenye Serikali basi tutakuwa tunaiibia Serikali. Mimi naomba suala la risiti lipewe kipaumbele na kama kutakuwa na utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi na sisi wengine wote ili kusudi kodi kupitia kwa risiti za manunuzi tuweze kupata fedha.

Lakini vile vile kama ninakumbuka amesema nadhani amegusia Dr. Lamwai. Tulipoanzisha *VAT, VAT* ilianza na vurugu. Nia ilikuwa njema kabisa lakini nadhani kwa sababu kitu kipya lazima mkiweke sawa sawa ilianza kama na vurugu ya namna fulani. Tunashukuru na tunapongeza kwa Wizara kwamba walau wamerekebisha kwa kiasi kikubwa. Sababu walipoanza wale vijana wa *VAT* kutoa hayo mapato walivamia maduka na watu walitaharuki na wengine walijiua. Mimi nakumbuka Mbeya kuna mfanyabiashara mmoja alijiua. Alipelekewa kodi kiasi ambacho yule kijana alipata *heart attack* yaani ule ugonjwa wa moyo. Amekufa na habari zipo, mtu amekufa. Yuko mwingine alijipiga risasi akasema afadhali kufa maana yake nitapata wapi hizi fedha. Hiyo ilikuwa ni mbaya. Lakini sasa naona Wizara pamoja na watendaji waliona jambo hili wakaendelea kurekebisha. Kwa hiyo, tunawapongeza katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kusisitiza kwamba kuwamotisha watoa kodi ni jambo moja zuri isionekana kama mtu anayetoa kodi yoyote yule ni adui wa anayekusanya kodi. Pawepo na mahusiano mazuri sana kati ya wanaotoa na wale wanaokusanya kodi. Lakini hali ilivyokuwa kama kuna uadui kati ya mtoa na mkusanya kodi kiasi kwamba akimwona anasema Mumiani anakuja anaanza mbio. Ubabe wa kusema utaona, tutakukomesha hapo. Watu wameweka ubabe pale na kwa hiyo kuleta mfarakano na uadui ambao ni *unnecessary* kati ya mtoa kodi na anayekusanya kodi.

Kwa hiyo, haya mahusiano yakiendelea na kwa sasa hivi kwa kiwango kikubwa jitihada imeonekana. Kwanza niwapongeze, kuna matangazo mengine ambayo mtu akipita barabarani anayasoma. Kwenye mabango unakuta picha ya watoto wanasoma: "Linasema lipa kodi kwa sababu kodi hii inasaidia kutoa huduma ya elimu". Hayo ni matangazo mazuri sana yale.

Vile vile kuelimisha kwa njia ya redio jitihada tunaiona. Lakini hasa kuendelea kila mahali hasa ngazi ya chini watu wakakuta kwamba kuna mahusiano watu wanakuwa *motivated,* wanaona kwamba wako pamoja na Serikali na Serikali ipo pamoja nao. Sio akija mtu wa kodi watu wanakimbia mbio. Nadhani ndiyo maana ilifika mahali Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ikaamua kufuta kodi ya maendeleo. Kwa sababu watu walikuwa wanakimbia nyumba. Anakaa porini mpaka msako utakapomalizika. Serikali ilipofuta Waziri amepongezwa na Serikali kwa ujumla sisi Wabunge tumempongeza sana kwa sababu tulikuwa tunakosa wananchi wengine muda mrefu. Sasa ndio tunapongeza na kwa sababu mahusiano yalikuwa ni mabaya mtu akikamatwa pale anaburuzwa anapelekwa wapi anadhalilishwa mbele ya mke wake na watoto. Sasa hivi watu wako huru na sasa tuna haja katika kodi zingine kujenga mahusiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika biashara Mheshimiwa Lamwai ameligusia vile vile kama nilivyosema watu ni wajanja. Kila ukitumia njia hii nao wanatumia njia nyingine. Mimi nashangaa mafuriko wa bidhaa nzuri sana zinazobebwa barabarani. Unamkuta kijana amebeba duka kubwa mgongoni. Duka haswa mmoja nimemwuliza unafikiri kilo ngapi akasema kama kilo 15 hivi au mpaka 20. Bidhaa hizo nzuri na mpya kabisa. Sasa hiyo biashara na vijana wako wengi wamejaa pale Dar es Salaam na miji mingine. Biashara imebebwa mgongoni na pale huwezi kutoza kitu chochote pale maana yule anaonekana anatembea na biashara. Kwenye *Literature* kuna ndege mmoja aliulizwa kwa nini wewe siku hizi unaruka bila kutua *"Why do you fly without perching"*. Akasema *"Since they learnt to shoot without missing, I have learnt to fly without patching"*. Kwa hiyo, na mimi wanapopiga hawakosei wakilenga na mimi nimeamua kuruka bila kutua kwenye mti. Maana ndege kama anatua lazima uwe na shabaha kali sana. Utampiga kama yuko ametua, lakini kama anaruka ukimpiga unampata. Ukimpeleka Mheshimiwa Kimiti kule kwenye *range* anapiga anatushinda hutampata. Ukipeleka watu wawindaji wanapiga sasa anasema basi kibao kile kinakwepa kwepa tuone kama atapiga.

Wale wanasema okay sasa *VAT* ipo na huyu Pesambili sasa amekuwa Pesa nyingi. Mheshimiwa Mramba sio Pesambili tena ni Pesa nyingi anakusanya kweli. Sasa sisi tukikaa na maduka yetu hapa tutapata shida tutafute vijana, tuwagawie maduka watembee nayo mtaani na wanatembea kweli na tunaona. Tena makubwa sana hapo sasa wametushinda akili maana hakuna anayesema. Pale wametushinda tu na kweli ungewakusanya kama sita au saba ujenge kanyumba useme ebu lundikeni hizi bidhaa hapa zingejaa duka. Sasa tutafute basi biashara halali kama na zile nazo zinalipiwa. Lakini unajua wale vijana wanapata fedha kidogo sana. Wakati fulani sisi Wabunge tunawahurumia. Unanunua hata kitu kwa kweli huhitaji kwa sababu kwanza unacho.

Lakini kwa kuwaonea huruma jinsi wanavyosaga mguu unamkuta Manzese ukianza kusema nikae kidogo basi Bulyaga nipate kasoda kangu unamwona kijana uliyemwona Manzese yuko pale. Anatembea vipi anajua mwenyewe. Siku nzima anatembea na sisi tuna watoto kama wale basi unasema ngoja ninunue *something.* Nunua hata hivi tu nipate chakula sijala toka asubuhi. Biashara hiyo hata watoto wamekaa kama Watumwa wanatembea basi tutafute namna ya kuwasaidia. Lakini vile vile ile biashara yenyewe tutafute namna gani wale wanaowatuma tunawabana kwa kodi zetu. Sio bidhaa zao zile nafikiri hilo limeeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, Muswada umekuwa ukiongelea juu ya maeneo ya ukusanyaji wa kodi kwamba kukusanya kodi kutoka kwenye ajira, biashara, raslimali. Mimi nilitaka kuongelea kwenye biashara hasa biashara ya madini. Mimi nazungumza siku zote sijui kama naeleweka. Kwamba mtu amekamata mgodi. Migodi nafikiri mnaifahamu. Halafu sielewi kama siku moja Waziri alinijibu hii *Tax Holiday* bado ipo. Maana kuna siku moja aliniambia haya tumeshaondoa huku tumeondoa, bado ipo. Kwa nini wasi wasi wangu uko mkubwa kusikia sisi tunapata asilimia 3. Nasikia kaasilimia 3. Ziko nchi kama Botswana nafikiri wanapata 50 kwa 50. Sasa huwa nauliza sababu ni nini kwa nini mtu anakuja anakwenda kuchimba anachukua vitu anauza sisi tunapata asilimia 3 halafu tunasema eeh kodi zingine halipi, au analipia wapi? Mtanieleweshe baadaye mtakapokuwa mnajibu hoja zetu. Yeye anachukua *Tax Holiday* ipo mpaka sasa na ni bado miaka mitano kwa hao kwenye Makampuni haya bado ni miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tumeshuhudia kwamba mtu amechukua Kampuni anachimba na anaona anakaribia miaka mitano, amefika miaka mitatu yaani ni *very simple logic.* Anasema *he declares bankruptcy* Anasema mimi hapa naona hii Kampuni imenishinda kwa hiyo nawauzia watu wengine, anawaachia watu wengine. Sasa nauliza je yule naye atakayekuja ameuziwa naye anaingia kwenye hiyo na anapata ile ya kwake ya miaka mitano. Halafu naye akifanya miaka miwili, mitatu naye akishasema aah mimi naona imenishinda je, naye anayekuja anapata miaka mitano hapo tutakuwa tunafanya namna gani.

Mimi nilitaka nieleweshwe tu. Mimi naona labda miaka ingepunguzwa kwamba mwaka mmoja, miwili mtu ajiandae kuseti mitambo yake. Lakini sasa yule anayekuja wa pili amekuta mitambo *already there,* kila *infrastructure* ziko pale anapewe *Tax Holiday* ya nini tena. Kwa sababu tayari mitambo ipo. Yule anayeanza anaweza akaanza kwa shida kweli miaka miwili, mitatu sawa. Lakini kweli ukivuta kwenye tovuti zetu hizi ulimwengu umekuwa mdogo namna hii unaweza ukapata *Tanzanite* iliyouzwa *millions of US dollar.* Lakini sisi tutakuwa tumepata kidogo, *"kale ka mpete".* Kale kidogo.

Sasa mimi naulizia hivi bado miaka mitano hivi mwingine akija naye anapata hivyo hivyo. Hivi sasa huu mchezo utaendelea halafu watatuonaje hawa watu tunaowaruhusu huo mchezo huo wa round. Mnapigana tu kuna mtoto anampiga yule anazunguka tu anayemkuta mwenzake anampiga. Huu mchezo hivi kweli utaendelea hivyo au tutasema basi yule wa kwanza ameshaleta *infrastructure* wewe unayekuja utaanza kulipa baada ya mwaka mmoja. Ukisha *settle after one year* tulipe. Mimi hii

inanipa taabu nataka nieleweshwe. Lakini nadhani Botswana hawana hiyo. Nadhani Sweden na mahali pengine. Sasa sisi tuna huruma au vipi? Maana mimi najua wanapata na baadaye watu wanakuwa wajanja wanahamisha wanahamisha yale madini, wanahamisha mgodi wanapeleka mahali pengine. Halafu nyinyi wakiondoka wanasema aah Mungu awabariki sana ni watu wema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka tusibarikiwe kwa kebehi tubarikiwe kwa kuwa tunasimamia kodi yetu vizuri. Lakini mimi hii nina wasi wasi nayo ndiyo nilitaka nalo nadhani wanielemishe tu. Sina nia mbaya lakini kwa nini mtu anaweza kuchukua hivi vitu ambavyo Mungu ametupa yeye anachukua asilimia 97 yote halafu sisi tunatazama, nini? Hata kama ni msaada anatupa lakini msaada kweli unalingana na anachopata yeye. Hilo ndilo nilikuwa nataka nijue mchezo huu utaendelea namna gani. Mara wanabadilisha jina mara huyu amemwuzia huyu jina limebadilika. Linatoka kwenye jina fulani linakwenda kwenye jina fulani. Sasa ni ujanja. Ujanja huo kama upo basi tukae tulijadili; Mheshimiwa Waziri tunajua ana uwezo kabisa wa kuona mianya hiyo ili tufike mahali tuseme tunaona hapa tunaibiwa. Hilo nilitaka nisisitize.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo nashukuru sana kwa kupata hii nafasi na nawapongeza Waziri na Manaibu Waziri wote, Menejimenti pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote walionisikiliza. Naunga hoja mkono, nilishasema sana nasema ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge muda uliobaki hautoshi kwa mchangiaji mwingine. Lakini nataka kuwahakikishia wale wote ambao waliomba kuchangia nafasi ipo. Kwa hiyo, tutaendelea jioni na Mheshimiwa Waziri atapewa nafasi ya kujibu kesho baada ya maswali. Kwa hiyo, nafasi ya wale wote walioomba bado ipo na watapewa nafasi. Kwa mchana huu tutakaporejea ataanza kuchangia Mheshimiwa Mwalyego, kwa hiyo ajiandae kwa kuchangia mchana huu.

Baada ya maelezo hayo pia Mheshimiwa Paul Kimiti Mwenyekiti wa Chama cha Idadi ya Watu anawaomba Waheshimiwa Wabunge wabakie humu ndani baada ya kuahirisha kikao hiki mchana huu ana masuala fulani fulani ya kuwaeleza. Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.53 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. YETE S. MWALYEGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe pole kwa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa kuunguliwa na makazi yake Ikulu na kupoteza mali zote za kwake binafsi. Tunampa pole sana, mimi mwenyewe pamoja na wananchi wa Mbeya Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ningependa niungane na wenzangu kumpongeza Waziri wa Fedha, Basil Pesambili Mramba, Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Katibu Mkuu wake pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa kutuletea Muswada safi baada ya kufanya uchambuzi wa kina na baada ya kuwasiliana na watu mbalimbali. Hivi ndivyo inavyotakiwa kwani kunakuwa hakuna maneno, lakini wangekuja na Muswada moja kwa moja kutoka ofisini kwao walete hapa kwa kweli ingekuwa shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kushinda kwa kishindo kule Addis Ababa, uchaguzi wa kuwa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika. Kweli hiki siyo kitu kidogo ni kitu kikubwa, tunampongeza sana na tunaomba aendelee kufanya kazi hiyo kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nampongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Mazingira. Pia, Mheshimiwa Balozi Dr. Pius Ng'wandu, kuwa Rais wa Mawaziri wa Elimu Afrika. Bunge letu kwa kweli naona limetukuka sana. *(Makofi)*

Baba wa Taifa alisema: "Uhuru ni kujitegemea." Pia, aliagiza kwamba tuache kupiga magoti kwa wafadhili tujitegemee, tulete maendeleo ya nchi yetu kwa kujitegemea, hayo ndiyo maendeleo ya kweli. Tukingoja wafadhili miradi inachukua muda mrefu na gharama kubwa na hivi sasa tumeona utengenezaji wa barabara kwa kutumia fedha zetu sisi wenyewe, fedha zinazotumika ni kidogo sana. Hii maana yake tulipe kodi, hakuna nchi hapa duniani ambayo haitozi kodi. Tulipe kodi kwa uaminifu, tutoe kodi na sisi kama Wabunge tuhamasishe wananchi wote kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee mambo ya Muswada kwa mapana yake ili wataalam wetu, Mawaziri pamoja na Serikali wayaangalie. Kama nilivyosema, marekebisho mliyofanya kwa kweli yanafanya kusiwe na kurekebisha vile vipengele kwenye Muswada. Tunaunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Lakini naomba niongelee mambo ya msingi ambayo mnatakiwa myalete katika Bunge lijalo kwenye Bajaeti ili tuone kweli haya yametekelezwa. Siyo siri, kodi zipo juu na hasa inayolalalamikiwa sana ni *VAT.* Wafanyabiashara wote na wananchi wote wanalalamika kuhusu *VAT.* Hata ukiangalia fedha mnazopata nyingi ni za *VAT.* Kwa kweli inabidi mje kwenye *level* inayotakiwa kwani Afrika Mashariki na Kati, Tanzania *VAT* ndiyo *the highest.* Kwa hiyo, tunaomba tuirekebishe ili tuje kwenye *level* inayofanana na uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, hiyo ni kazi ya kitaalam siwezi kusema ni kiasi gani, lakini mnaweza kukokotoa namba, lengo liwe ni kuja kwenye *level* inayotakiwa, lakini siyo *20 percent. 20 percent* ni juu mno, watu wanalalmika. Mimi kama Mbunge nimetembelea Makampuni mengi na nimetembelea wananchi wengi kule Mbeya, wote wanalalamika wananiambia, bwana kodi ya *VAT* ipo juu, tunaomba uwaeleze wahusika ipungue. Tutafurahi sana kama mtaipunguza. Tukishapanua wigo wa mapato kuna watu wengi

zaidi wanaolipa kodi, huwi na wasiwasi kupunguza *VAT* kwamba mapato yatapungua. Kwa hiyo, ndiyo *philosophy* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii maana yake ukipunguza *VAT,* Makampuni na watu binafsi watabaki na fedha ambazo wangelipa Serikalini. Wakishabaki na zile fedha wanapanua mtaji wa Kampuni, wanaajiri watu wengi zaidi na wanalipa kodi nyingi zaidi. Kwa hiyo, siyo kwamba labda tunataka kuiibia Serikali, hapana, *actually* tunataka ku-*stimulate growth* ya uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu biashara ya mafuta. Biashara ya mafuta ina mchango mkubwa kwenye kodi za Serikali, lakini wote ni mashahidi tumeacha biashara ya mafuta holela.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna usimamizi wa biashara ya mfuta na hatujui ni kiasi gani cha mafuta yanaingia, ila tu kwa kukadiria *TRA* wametoza kiasi gani ambapo anatakiwa awepo mdhibiti na tulishapitisha sheria na maswali kila wakati yanaulizwa hapa, *EWURA* itaanza lini? Unapo-*liberalize* uingizaji wa mafuta bila kuwa na msimamizi wa ku-*regulate* hiyo biashara ya mafuta, kwa kweli unaweka milango wazi kwa wizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kwamba Serikali itueleze watabana hiyo mianya lini kwa sababu bila kuanzisha *EWURA* huwezi kubana mianya. Mnaanzisha lini *EWURA?* Hayo ndio mambo ya msingi, tuwe na msimamizi wa maji na mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niongelee suala moja ambalo tunatakiwa tufanye ili tuongeze mapato yetu kule Mbeya. Mwaka 1999 Serikali iliagiza kufuta ukulima wa Pamba Mbeya. Maana yake ni kwamba wananchi hawalimi Pamba, vile vile viwanda vya kuchambua Pamba havifanyi kazi. Kile kiwanda cha *New Mbeya Tixtile* ambacho tulikibinafsisha mwaka huo huo wa 1999, nina uhakika tungebinafsisha baada ya hapo mwekezaji asingekubali kukinunua kwani anaagiza Pamba kutoka Shinyanga, wakati mwingine anaagiza kutoka Cameroon na Nigeria.

Kwa hiyo, utakuta gharama kwa kiwanda ni kubwa sana na kodi analipa kidogo. Hawa wakulima ambao walikuwa wananunua mabati, vyakula, *cement* na kadhalika hawanunui tena, kwa hiyo kodi hatupati. Wananchi waliokuwa wanafanya kazi kiwanda cha kuchambua Pamba pale Mbeya Mjini wamefutwa kazi hawana mapato na kodi hailipwi tena. Hivi hatuoni haya yote, kwamba umefukuza pato lako!

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kusema kwamba, nimetumwa na wananchi wa Mbeya, wanachotaka ni kulima Pamba na wameniambia bwana usirudi hapa, usirudi Mbeya bila kutuletea jibu halisi. Nadhani Mheshimiwa Charles Keenja, ananiangalia hapa, naomba sana mwezi wa Juni kwenye Bajeti tutangaziwe rasmi tulime Pamba, bila hivyo mnataka mimi nisirudi hapa? Bila ya hivyo mnataka Mheshimiwa Njelu Kasaka na Mheshimiwa Paul Ntwina wasirudi hapa? Bila hivyo mnataka huyo Mheshimiwa wa Mbarali asirudi hapa? Hivi jamani mnataka tuondoke wote! Tunajua wengine hamrudi tena, lakini mnataka na sisi tuondoke! Huu ni uamuzi wa Serikali ya Awamu ya Tatu, ni

matatizo yaliyoletwa na Awamu ya Tatu, tunaomba mwezi Juni mwaka huu mrekebishe, bila hivyo hatutakuwa tunaelewana humu ndani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda na kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Muswada huu wa kodi ya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda niungane na wenzangu wote kumpa pole Mheshimiwa Rais kwa janga la moto. Ni kweli Watanzania wote tumefadhaishwa na kitendo hicho na tunaamini kwamba suala hilo litapatiwa ufumbuzi unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kusema kwamba nampongeza sana Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba. Mheshimiwa Basil Mramba amekuwa kila siku akiongeza chati. Ukiangalia *trend* ya Bajeti zake na Miswada anayoleta hapa Bungeni kwa kweli inazidi kumpandisha chati kwa hali ya juu sana. Naamini kwamba timu aliyonayo ya watendaji wake na wasaidizi wake ndiyo inamfanya aweze kutekeleza majukumu yake vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma tumekuwa na tabia ya kurithi sheria mbalimbali. Lakini Muswada huu itakuwa ni sheria yetu sisi wenyewe kwa sababu imezingatia matakwa yote ya wadau katika sekta mbalimbali, matakwa ya Serikali na hasa matakwa ya walipakodi wenyewe. Zamani tulikuwa tunasema kwamba, mtoza kodi au mtoza ushuru hakuna kuona ufalme wa mbingu, lakini nadhani Mheshimiwa Basil Mramba na timu yake ya *TRA* na Watanzania wote tutaona ufalme wa mbingu kwa msingi huo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze sana Ndugu Harry Kitilya, Kamishna Mkuu wa Kodi ya Mapato na timu yake. Kwa kipindi kifupi tunaweza kuona jinsi uchumi unavyokua Tanzania. Lakini uchumi unakua kwa sababu ya uwezo wetu wa ndani. Mapato yetu ya ndani yameweza kuongezeka. Sasa hivi tumekuwa na nidhamu ya kukusanya mapato na tumekuwa na nidhamu ya kutumia pesa tunazozipata. Kwa hiyo, hiki ni kigezo kizuri sana kuona kwamba nchi yetu sasa hivi inaaminika nje na ndani kwa sababu hali yenyewe inajidhihirisha na nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwa yeye ndiye kinara wa mambo yote haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi labda niseme kwamba, bila Waziri Basil Mramba kukusanya mapato, Mheshimiwa Charles Keenja, hatafanya kazi, Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi hatafanya kazi, barabara hazitajengwa, malambo au maji hayatapatikana. Lakini sasa uwezo mkubwa wa Serikali unafanya mambo yote haya yaweze kufanyika vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania si kisiwa, ni kijiji ndani ya dunia katika mfumo mzima wa *Information Technology* na *Globalisation.* Kwa hiyo, haiwezekani sisi Muswada wetu huu ukawa tofauti na matarajio ya wenzetu wote. Kamati ya Fedha na

Uchumi ambayo pia mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati hiyo na wenzangu wote tulishiriki sana kuona kwamba angalau tunaweka input itakayoweza kusaidia Muswada huu uweze kuangalia maslahi ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu una sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inahusiana na mapato yanayotokana na ajira, mapato yanayotokana na biashara na mapato yanayotokana na vitega uchumi. Kwa kuzingatia vipengele vyote kwa kweli nasema kwamba sina mahali pakubwa pa kukosoa kwa sababu yale yote ambayo tulikuwa nayo Mheshimiwa Waziri ameweza kuyazingatia na ndiyo maana nasema kwamba Mheshimiwa Basil Mramba anastahili sifa ya pekee kwa kuwa msikivu na kuwa ni mtu ambaye unaweza kumshauri na akashaurika. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Rudia tena.

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Mheshimiwa hapa kuniomba nirudie, lakini naomba niendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho napenda kukiweka wazi na kujaribu kumuomba Mheshimiwa Basil Mramba ni kwamba Muswada huu wa kodi tujaribu kuuoanisha na baadhi ya sheria nyingine za mapato za nchi jirani, kwa sababu sasa hivi tunaingia kwenye soko huru ambalo nchi yetu itakuwa ni moja kati ya washiriki au wadau. Kwa hiyo, ninaamini kabisa kwamba katika marekebisho yatakayokuja hapo baadaye yajaribu kuoanisha kodi zetu tunazotoza hapa na kodi za nchi jirani.

Vile vile, bado kuna haja ya kuangalia sana uwezekano wa kuweza ku-*harmonize* kati ya Muswada huu na sheria ya *VAT* pamoja na sheria ya ushuru wa forodha kwa sababu zile bado hazijafanyiwa marekebisho ya kutosha na hii unakuta inachanganya kwa baadhi ya watozakodi hata walipakodi wenyewe kwa kuwa kuna vipengele ambavyo vinahitaji vifafanuliwe vizuri zaidi na tuweze kuweka mambo yote sawia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja moja kidogo ilileta utata kuhusiana na *Powers of the Minister to exempt tax.* Kweli ilikuwa ni hoja ambayo kidogo ilikuwa ni nzito, lakini nashukuru kwamba Mheshimiwa Basil Mramba tuliitana tukazungumza na baada ya kuzungumza akawa bayana akasema kwamba yeye toka amekuwa Waziri ametoa misamaha 10 kati ya 12 peke yake na yote akaweza kuielezea ni misamaha ipi na kwa kweli tukaona kwamba ni misamaha ambayo imelenga katika kuboresha utendaji kazi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo ni ya msingi ni kwamba, leo hii Mheshimiwa Basil Mramba anafanya kazi vizuri na kuna *checks and balances,* lakini naamini kwamba utamaduni wa uwazi uendelee kuhimizwa kwa sababu tumeishakuwa na historia huko nyuma kwamba nchi hii ilifikia mahali ikawa inasamehe kodi kwa kila kitu, matokeo yake tukakosa hata mapato na hii tukaweza ku-*learn* hata *repetition* yetu mbele ya wahisani. Sasa hivi tumeweza kujenga mahusiano mazuri ni bora tukaweza kuyaendeleza kwa msingi wa kuwa wazi zaidi katika shughuli zetu hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nakiona kwamba katika Muswada huu kimeweza kujenga jamii yetu vizuri zaidi ni kule kutokutoza kodi zile gharama ambazo mwajiri anazitumia anapokuwa anam-*train employee* wake. Hii kwa kweli itasaidia sana, sana, sana, kuweza kuwa-*encourage* wale *employers* katika ku-*train staff* wao kwa sababu hiyo *already* itakuwa ni *tax datable.* Ina maana kwamba inakuwa ni *expense* kwenye *business employer.* Kwa hiyo, hili nadhani ni wazo zuri zaidi na naomba basi kama kuna uwezekano tuweze kulitekeleza na kujaribu kuwashawishi waajiri wengi waweze kufundisha watumishi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nchi yetu ina walipakodi wapatao kama 190,000. Hii ni idadi ndogo sana ukilinganisha na jumla ya Watanzania ambao tuko karibu milioni 34 au 35. Sasa ukiangalia uwiano huu ni mdogo sana. Kwa Muswada huu tumeona tayari tunapanua wigo kwamba kila mwenye kufanya biashara halali, kila mwenye kupata pato halali ni lazima alipe kodi. Nakumbuka miaka ya nyuma aliyekuwa Waziri wa Fedha alitoa tamko kwamba, kila mtu atabeba msalaba wake mwenyewe. Watanzania hatukumlewa kwa kipindi hicho na kama ni matatizo basi yeye aliyabeba zaidi kwa sababu hatukumwelewa. Lakini leo hii *this is not the case* kwa sababu kila Mtanzania anajua kwamba sasa hivi lazima abebe msalaba wake yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda kuchangia hayo tu. Nashukuru sana na naunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe.

Kwa kuwa nilikwishawapongeza Mheshimiwa Mama getrude Mongella na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, pengine nimpongeze Waziri Dr. Pius Ng'wandu kwa kuteuliwa kuwa Rais wa Mawaziri wa Elimu ya Juu. Pia, nimpongeze Waziri wa Fedha, wenzangu wote waliochangia wamempongeza kwa kazi nzuri yeye pamoja na Naibu wake na watendaji katika Wizara, Katibu Mkuu na wasaidizi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama walivyopongeza wenzangu, mimi nafikiri lazima tukumbuke kwamba aliyopo jikoni ndiye anasifiwa kwa kupika chakula kizuri. Kwa hiyo, *TRA* wasifiwe sana kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Ndugu yetu Sanare alivyoondoka tulikuwa na wasiwasi kwamba Kitilya pengine atashindwa, lakini ameweza kuvaa kiatu cha Sanare vizuri sana, tunampa pongezi nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nimpongeze Spika na wewe mwenyewe kwa kubuni utaratibu mzuri wa kujadili Miswada kabla haijaletwa Bungeni. Hivi leo watu wanashangaa ni kwa nini Miswada inaweza kupita kwa siku moja au nusu siku, lakini hii inatokana na sera ya ushirikishwaji. Wadau wote wanashirikishwa, kwa hiyo, unakuta malalamiko yanakuwa kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wa Chuo Kikuu waliofanya vurugu Dar es Salaam juzi siyo kwamba hawakushirikishwa, waliitwa lakini nasikia wao hawakwenda. Hawakuwa katika kikao kilichojadili, wangekuwepo pale wangetoa mawazo yao. Naamini kabisa utaratibu wa ushirikishwaji na utaratibu huu wa kutoa nafasi kwa

walengwa kujadili Muswada utatufikisha mahali pazuri sana katika kupitisha Miswada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije katika lile ambalo ninapaswa kuchangia. Muswada huu unahusu Sheria ya Kodi ya Mapato. Tunazo aina mbili za kodi kubwa ambazo ni kodi ya *VAT* na kodi ya mapato. Muswada huu una lengo kama ile sheria nyingine ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato au kuimarisha Mfuko wa Serikali ili Serikali ipate mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kupanua wigo na kuipatia Serikali ili Serikali ipate mapato ya kutosha na tatu, kuboresha Muswada uliokuwepo kwa sababu kulikuwepo na Muswada, unaboreshwa ili tuweze kupata zaidi. Sasa, binafsi nitajielekeza zaidi katika hiki kipengele cha pili cha dhumuni, kupanua wigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo ambalo linaeleweka wazi kwamba asilimia 50 ya mapato yanayotokana na aina hii ya kodi ya mapato inatokana na kodi ya ajira. Kodi ya ajira ndiyo inayotoka asilimia 50 ya mapato yanayotokana na kodi ya mapato. Nikizungumza kodi ya ajira ina maana wale walioajiriwa na wanaoeleweka kwamba hawa wameajiriwa na wanalipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utafiti uliofanywa kuna karibu waajiriwa milioni 2 ambao wanafahamika, lakini ziko ajira ambazo hazijafahamika takriban kama milioni 15 hazijaingizwa katika wigo wa kodi. Sasa tunafanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba tunaendelea kuwapa mzigo mkubwa hawa waajiriwa milioni 2 ambao wanatambulika kama ilivyosemwa leo asubuhi. Mimi nina tabia sana ya kutetea tetea watu, lakini ni tabia nzuri kwa sababu Sera za Chama cha Mapinduzi ni kuangalia utu wa mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyosemwa asubuhi, hivi sasa mwananchi aliyeajiriwa anakatwa karibu asilimia 25 ya mshahara wake, ndiyo kodi ya mapato. Kama ilivyotolewa mfano, mtu anayepata kama shilingi 900,000/= kwa mwezi kama Waheshimiwa Wabunge wanavyopata, anakatwa karibu shilingi 205,000/=, ndiyo kodi ya mapato. Ukizidisha hiyo unapata karibu shilingi 2,600,000/=. Kwa hiyo, ukiangalia kwa ujumla ni karibu asilimia 25.

Sasa ukiangalia katika jedwali lililoko katika ukurasa wa 131 mfanyabiashara anayefanya biashara ya kati ya shilingi 3,000,000/= mpaka shilingi 5,000,000/= anatozwa shilingi 20,000/=. Anayefanya biashara ya mpaka shilingi 7,000,000/= anatozwa shilingi 50,000/=, anayefanya biashara ya shilingi 7,000,000/= mpaka shilingi 14,000,000 anatozwa shilingi 165,000/=, anayefanya biashara ya shilingi 14,000,000/= mpaka shilingi 20,000,000/= anatozwa shilingi 385,000/=. Hebu angalia tofauti inayotokana na hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nimeishauri sana Serikali, bwana punda unaweza ukampandisha mizigo, lakini kuna siku moja atafika mahali analala chini anakwambia mzigo huu umenitosha siendi. Sasa tufike mahali tutayarishe utaratibu wa

kupanua wigo, tunawezaje kuupanua wigo wa walipa kodi kutokana na ajira? Ajira siyo lazima iwe ya kuajiriwa ofisini, lakini ajira inayotokana na mapato ambayo sasa ndiyo ili tuwasaidie hawa waajiriwa ni lazima tuiangalie hii, kukuza ajira isiyo rasmi. Ajira isiyo rasmi ni ajira ya hawa ambao tunawaona wanatembea barabarani, wenye biashara ndogo ndogo, wenye shughuli ambazo siyo rasmi, tukiweza kuwatoza kodi hawa basi wale ambao tunawafahamu rasmi kwamba wameajiriwa tunaweza kupunguza viwango vya kodi, vinginevyo kwa sasa ukisema uwapunguzie Serikali itashindwa kuendesha.

Kwa hiyo, mimi ushauri wangu kama nilivyosema suala la uwezeshaji wa Tanzania, ni suala muhimu sana, ili tuweze kupata mapato yaliyojificha. Kama hatutaangalia kwa mfano, kama ilivyosemwa, hivi wale wenzetu walio na maduka ambao siyo raia wa nchi hii wanamlipa nani kodi ya mapato? Wameajiriwa na nani, wanaendesha biashara humo Kariakoo, kodi yao inakwenda kwa nani? Kikubwa atakuja kulipa ile kodi ya mwisho ya mapato. Lakini kodi ya kuajiriwa huwezi ukamshika. Lakini ukipanua wigo na ukaweza kuwawezesha Watanzania wengi ni ukweli kwamba wigo huu wa kupata mapato utainuka.

Kwa hiyo, suala la uwezeshaji, suala la kuweka mikakati ambayo itawasaidia Watanzania, walio na mapato madogo waweze kuumuka wafanye shughuli zao, hata kama leo ungesema hawa Wamachinga wanaotembea waambie tu kwamba mimi sina ugomvi na wewe zunguka utalipa kodi ya shilingi 100 au hata shilingi 50 kwa siku na ufanye biashara yako kwa uhuru na eneo lako la kufanyia biashara ni hapa tutapata mapato ya Serikali mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili niliona nilikazie sana na tuangalie sana hawa wafanyakazi wachache ambao tunawakamua sana, tusipoangalia tutakuta mahali wanakata tamaa. Lakini vile vile ningesisitiza mara nyingi yule tunayemkata kodi basi tumpe moyo. Kwa hiyo, katika hilo sina zaidi ya kuongeza.

Sasa nije katika utaratibu wa kawaida na napenda kuwapongeza wafanyakazi wa *TRA*. Huko nyuma *TRA* waliokuwa na utaratibu wa kutishia walipa kodi na hii napenda nimsifu sana ndugu yangu Kitilya na wafanyakazi wote. Hivi leo tabia ya wakusanyaji kodi imebadilika sana, wamejenga tabia ya kukaa na mteja na kuzungumza naye na kumwuliza sasa wewe utalipa kiasi gani? Ile tabia ya ukubwa ile ya zamani mtu anaingia utafikiri askari ameingia ofisini kwako imepungua. Naomba muendelee kukaza kamba. Kodi haishikwi hata siku moja. Hata wale wa Kaizari walikuwa wanaogopwa lakini walikuwa na utaratibu mzuri wa kuwakuta watu sokoni anamwuliza wewe umeuza shilingi ngapi? Anamwambia ameuza shilingi mbili anamwambia basi katika mbili nipe theluthi moja anatoa pamoja na kuogopwa, walikuwa wanaogopwa kwenye masoko hawawaogopi majumbani kwao. Lakini huko nyuma tulifikia mahali mtu akija dukani una wasiwasi kwa hiyo, tunaishukuru sana idara na tunashukuru sana *TRA* kwa kubadilisha mawazo ya wafanyakazi katika ukusanyaji kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningelizungumza kwa sababu muda ni mfupi ni hii *clause* ya 3 kifungu cha *definition* ya *investment of assets*. Hili limezungumzia hata katika *amendment* kwamba kitakachotajwa kwa mtu kuuza nyumba yake ni kulipa *excess* ya shilingi milioni 15 ukurasa wa pili katika *amendment.*

Sasa mimi nina wasiwasi kwa sababu tunapoweka kodi ni vizuri tuweke taratibu za kodi ambazo tuna uhakika tunaweza kuzifanyia kazi na zikaleta mapato kwa Serikali. Sasa mimi nina wasiwasi sana unapomwambia mtu alipe shilingi milioni 15 katika thamani ya nyumba yake, hivi unajuaje hiyo thamani yake? Kwa hiyo, ina maana ya kwamba mtu atakavyokuwa mjanja ni kwamba nyumba itatamkwa kwamba mimi nimeuza nyumba yangu shilingi milioni 30, lakini gharama ya kuijenga ni milioni kadha ambazo hatazidisha ya ile ambayo ana uhakika atapewa nafuu ya ile shilingi milioni 15. Kwa hiyo, yeye atasema ameuza nyumba yake kwa shilingi milioni 20 ili asilipe wakati yeye ameuza juu. *(Makofi)*

Sasa hii utamdhibiti vipi? Mimi nafikiri tungekuwa na utaratibu labda tupate maelezo kwa Waziri. Mimi nilifikiria katika hili mwananchi angeruhusiwa kuuza nyumba yake na pengine tungesema sijui ilitajwa asubuhi sasa sijui imeelezwa wapi, lakini mimi ningeshauri kwamba ingefaa mtu katika kuuza nyumba aruhusiwe kuuza nyumba moja bila kulipa kodi. Sasa akishajulikana anauza nyumba nyingine na kwa sababu ana *TIN* wata-*identify* tu kwa sababu ana *TIN* kwamba amekwishauza nyumba moja. Sasa hii nyumba nyingine anauza ni lazima alipe kodi kutokana na kiwango kile kinachoanzia faida yake hata ikiwa shilingi moja ailipie kodi kuliko ukisema tu ameuza nyumba tano kwa sababu kiwango cha faida yake haizidi shilingi milioni 15, hakuna mtu atakayetangaza shilingi milioni 15 atakuambia nimeuza nyumba hii nilijenga kwa milioni hizi kwa hiyo, haikuzidi shilingi milioni 15 kwa hiyo, huwezi ukaishika kodi kama sijazidi shilingi milioni 15.

Mimi ndiyo nina wasiwasi katika hili nipate maelezo vizuri, pengine tungekubaliana kwamba mtu anaruhusiwa katika Jamhuri anauza nyumba yake moja halipi, akishauza nyumba ya pili sasa ni lazima alipe kodi hii itawasaidia hata wananchi walio na kipato kidogo. Mtu ameuza nyumba ajenge nyumba, leo unamuuliza umeuza shilingi ngapi? Sasa thamani ya nyumbani inabadilika, nyumba ulioijenga miaka minne iliyopita, miaka 20 iliyopita kwa shilingi milioni moja leo inaweza ikakupa shilingi milioni 20 lakini huwezi ukaijenga nyumba hiyo leo.

Kwa hiyo, pengine tumpe nafasi kwamba nyumba hii ya kwanza ambayo wewe umeuza basi ikuwezesha kujenga nyumba nyingine. Hizi nyingine tunajua ni mapato ya ziada lazima uyalipe. Haya ni mawazo yangu Serikali iangalie itakavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kifupi kwa sababu kengele ilishalia tuangalie suala la *double taxation* lilizungumzwa asubuhi, hebu tuangalie tusiwa-*tax* watu mara mbili. Kwa mfano, mfanyakazi analipa kodi ya mwenye nyumba, hiyo kodi nayo inashikwa kodi, sasa utakuta mfanyakazi umemnyonya kule asilimia 25 na huku mwenye nyumba tena analipia ni vitu ambavyo tunaviangalia tu *technically* kwa sababu sheria inabadilika tutaendelea kushauriana tufanye nini. *(Makofi)*

Suala la elimu kwa kweli mimi mwenyewe kwa bahati nzuri nimekuwa kwenye mashirika kwa miaka 25 nikiwa Meneja, ukiniuliza utaratibu wa kodi naweza kukushangaa, lakini baada ya kuondoka nimeanza biashara, leo ukiniambia hata kuzijaza

zile fomu wakati kuwa ngumu. Naomba utaratibu wa fomu zile lugha ya *taxation* ibadilike iwe laini sana. Hapa nimesoma katika Muswada huu kwamba sasa utakuja ule utaratibu mteja anataja kodi anayotaka kulipa, tukifanikiwa katika hii ya *self assessment* hilo ndiyo linalotakiwa, wewe anakuja ana-*assess,* sasa anakudanganya *investigators* waende wakaangalie anakudanganya nini, haya mambo ya kumwambia jazi, sijui *TIN* sijui mwaka jana mapato yako, *turn over* haya mambo bwana inafika mahali mpaka fomu ile ukiletewa unatoka jasho kwanza ya nini, wewe unataka cha Kaizari pokea haya mambo ya kumwuliza maswali mengi unataka kumwuliza nini? Bwana tutaogopana hapa. Naomba mliangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la uwezeshaji nimekwisha zungumzia. Mimi nimpongeze Waziri na kushukuru kwa Muswada huu mzuri na ninamtakia heri Waziri na ni Waziri mzuri, jitahidi sasa, tunategemea *bill* nzuri ya mwaka huu ya msamaha wa kodi na nina uhakika wananchi wanasubiri kile utakachokuja kuwastua kama ulivyostua mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Muswada huu wa Kodi ya Mapato.

Kwanza mimi ningependa nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil Mramba, pamoja na Manaibu wake, Katibu Mkuu wake na watendaji wake wote kwa kuweza kukaa chini na kufikiria kwamba wakati umefika wa kubadili ile sheria ya zamani ya kodi ya mapato na wakaweza kutengeneza Muswada ambao nafikiri kama wananchi watauelewa vizuri, basi tutaweza kupanua uwigo wa kodi na mapato ya Serikali katika nchi hii.

Pili ningependa nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watalaam wake kwa sababu wao nafikiri ndiyo ambao wanakaa chini wakishauriana na watalaam wa Wizara ya Fedha, kutengeneza Muswada huu. Nisiwasahau pia Wanakamati waliochambua Muswada huu ambao kwangu mimi kama Mbunge wa kawaida tu ambaye sikusoma haya mambo nimeona kwamba wamefanya kazi nzuri sana. Naomba kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamechangia vizuri, Muswada umetengenezwa vizuri. Kwa hiyo, nimeona kwamba sitazungumza mengi ila nitazungumza machache kwa nia ya kuboresha tu. Sasa tunapozungumza juu ya kupanua wigo wa kodi nia yetu inaweza ikafanikiwa tu kama wale walengwa wataelewa kwamba wao wanakuja wapi katika huu Muswada wa Kodi.

Hivyo basi, ningependa nimshauri Waziri na Wizara yake, iangalie namna ambavyo wanaweza wakatengeneza mikakati ya kutoa elimu kwa umma kuhusu huu Muswada na hii sheria itakapopitishwa. Kwanza ningependa nimshauri kwamba ni vizuri vikatengenezwa vijitabu vidogo vidogo ambavyo vinatoa *extract* kwenye hii sheria ambavyo vitamwezesha yule mlipa kodi wa kawaida wa nchi hii ambaye ni mfanyakazi pamoja na wafanyabiashara wadogo wadogo. Wale wakubwa nafikiri wana *layers* wao

*they can afford* ku- *hire a tax consultant* wanaweza waka-*afford* ku-*hire a layer* kuweza kuwafanyia kazi yao. Lakini wale wafanyabiashara wadogo wadogo ambao ndiyo Watanzania wanaojitokeza sasa hivi wengi hata ukiwapa hiki kitabu wasome wataona kana kwamba unawatukana kwa sababu kwanza hiyo lugha inayotumika hawailewi na pia huo muda wa kusoma kwa sababu ya ushindani mkubwa wa biashara hawana. Lakini kama utamtengenezea kijarida kidogo tu ambacho kitamwonyesha *section* yake anayohusika nayo akasoma na akaielewa nafikiri atasoma na atakuwa tayari kulipa kodi.

Tunapozungumzia pia kupanua wigo wa kodi, ningependa kusema kwamba Watanzania wengi hawaelewi umuhimu wa kupata risiti na ninaomba kusema kwamba pamoja na kujulisha mamlaka inayohusika kwamba wafanyabiashara wengi wanajitahidi sana kuwashawishi wanunuzi wasichukue risiti wakiwaambia kwamba ukichukua risiti utalipia *VAT* na ukilipia *VAT* utalipa fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kujiuliza ukiingia kwenye maduka hukuti *list* ya bei za bidhaa zilizomo mle zikiwa bila *VAT* kusudi hata yule mwananchi wa kawaida ambaye haielewi *VAT* ni nini ajue kwamba sasa kama amelipa, amelipa bei ambayo ni halali lakini *unfortunately* hawa wafanyabiashara wanawauzia kwa bei ile ile ambayo ina *VAT* lakini hawawapi risiti. Kwa hiyo, wanaibia Serikali yetu. Naomba mamlaka inayohusika ijaribu kufuatilia sana mambo hayo. *(Makofi)*

Pili, tunasema kwamba tuangalie kupanua wigo wa kodi, lakini unakwenda kwenye duka kwa mfano kwenye duka la *wholesale* unakuta yule mwenye duka la *wholesale,* yuko pale na mtoto wake na mke wake na mjomba wake sijui na nani, hawa watu wanaambiwa kwamba wanafanya kazi bila mshahara, anayelipwa mshahara ni yule Mwafrika anayebeba mizigo na yeye sijui kama analipwa mshahara ambao unaweza ukatozwa kodi.

Kwa hiyo, mtu huyu kodi anayolipa ni ile kodi ya mwisho wa mwaka ya *income tax* kwa ajili ya biashara yake anayofanya. Sasa pamoja na hayo ningeomba sasa mamlaka zinazohusika ziangalie namna ambavyo itawaingia hawa watu iwaulize kama wao wanafanya kazi hapa kwani mwisho wa mwezi hela zote zinawekwa *bank* kwa jina la *enterprise* yao au la kila mmojawapo pamoja na mjomba wao wanalipwa mshahara? Kama wanalipwa mshahara, wanalipwa shilingi ngapi ili aweze kulipa kodi? Nafikiri nchi zingine wanaangalia hayo. Lakini ni hapa kwetu Tanzania tu unakuta kwamba mtu kajaza watu wengi dukani, ndugu zake na wengine. Lakini hawa watu hawalipi kodi kwa sababu wanasingizia kwamba hawalipwi mshahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ningependa kuzungumzia juu ya *charitable organizations* hiyo ni ibara ya 74 inayozungumzia kwamba *charitable organization* ita-*declare* mapato yake na italipa kodi. Sasa naanza kujiuliza hizi *charitable organization* zinafanya kazi gani ambayo ni ya faida? Zinafanya kazi ya kuwahudumia walengwa ambao ni watu wasiojiweza katika taifa letu. Hawa *charitable organizations* mapato yao yanatoka kwenye biashara au ama yanatoka *from charities and from charities* maana yake inawezekana ikatoka kwa wale wanachama wa hilo shirika au kutoka kwa wafadhili.

Sasa huyo mfadhili ambaye utamwomba fedha umwambie kwamba sasa hizi fedha zako unazoniletea mimi nizitazi-*declare* na nilipie kodi kwa Serikali yangu, nafikiri wengi wataanza kujiuliza wewe unataka kulipa kodi kwa hela ambayo mimi nimeipata kwa mlipa kodi wangu na nikasema naileta kwako wewe uweze kumsaidia Mtanzania ambaye hajiwezi?

Mimi ningeomba kifungu hiki Wizara husika ikatoa ufafanuzi wanataka kumaanisha nini? *Otherwise* itakuwa ni matatizo kwamba wengi hawataelewa vizuri, hata mimi mwenyewe naomba kusema kwamba sikukielewa vizuri sasa naomba Wizara itoe ufafanuzi maana yake ni nini *charitable organizations* pamoja na ku-*declare assets and income* kwa ajili ya madhumuni ya kuweza kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ningependa kuzungumza pale ambapo wanasema kwamba mwajiri atapunguziwa kodi kama atawasomesha wafanyakazi wake. Mimi naomba kuwapongeza sana kwa sababu itawasaidia sana wafanyakazi wanaofanya kazi katika *private enterprises* kuweza kupatiwa elimu. *(Makofi)*

Lakini suala lingine ambalo najiuliza, je, kutakuwepo na *mechanism* ya kuweza kuwashinikiza hawa ambao wanataka jasho la Mtanzania na siyo kumwendeleza waweze kutoa fedha zao kumsomesha huyu mtu?

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kweli kusiwepo na *abuse* ya kusema kwamba tumesomesha watu kadhaa kumbe hawajawasomesha ilimradi anamwambia kwamba wewe sema kwamba nimekupeleka shule ya kompyuta *for so many hours or for so many weeks* nikakulipia ili nikuongeze mshahara wako kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kusema kwamba pale ambapo waajiri sasa watakuwa wanapunguziwa kodi kwa ajili ya kuwasomesha wafanyakazi wao, naomba basi yawepo masharti mawili makubwa.

La kwanza ni kwamba wanapowaelimisha wale wafanyakazi naomba na uwiano wa kijinsia utazamwe pia kwa ndani kwa sababu kuna masharika mengine ambayo mwanamke kwao ni mwanamke tu hatapata mtu wa kumuelimisha kwamba wanapoleta rekodi zao waambiwe kwamba tunataka kuona mchanganuo wa kijinsia kwamba mmesomesha wanawake wangapi na wanaume wangapi katika shirika lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kusema kwamba kama inawezekana basi kuwepo na *mechanism* ya kuweza kuwafuatilia sasa hawa kwamba hii *privilege* ambayo imetoka wahimizwe na wafuatiliwe kwamba kila mwaka katika mipango yao ya mashirika yao au kampuni zao wana mipango gani ya kuwaelimisha wale wanaofanya kazi kwao na hawa wanaoelimishwa basi wawe ni Watanzania siyo wale ndugu zao ambao wamewaleta na kuwaingiza nchini ndiyo ambao wataambiwa kwamba nimerudisha Uingereza kwenda kusoma kumbe kapelekwa kwenye likizo. Naomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huyu mnyama anaitwa *tax holiday,* huyu namwita mnyama kwa sababu inawapa wawekezaji wengi *loophole* ya kuliibia Taifa hili. Unamkuta mtu anaanzisha kiwanda anapewa *tax holiday,* kile kiwanda kinafanya kazi wee! Ikifika mwaka wa nne na nusu kile kiwanda kimeshafilisika kimeanza kiwanda kingine kwa jina lingine na ukiangalia mwekezaji ni yule yule anahama anaacha majengo pale maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba huyu mtu ni mtu mbinafsi hivyo kwamba anaona kwamba jasho lake halifai kupewa Watanzania kwa njia ya kodi, sasa huyu ningependa tumwone kwamba ni adui. *(Makofi)*

La pili hawa wawekezaji wanakuja anawekeza hapa, wanaamua kukaa kuuza ile biashara yake akiwa nje ya nchi ili asiwe kulipa *capital gain* hapa, asiweze kulipa *stamp duty* hapa Tanzania na baada ya kuuza huku nyuma tunabakiwa sisi tuna matatizo kuanza kukimbizana na hawa ambao wamenunua hizo kampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa Serikali itutamkie hapa Bungeni kwamba hawa wawekezaji ambao wanauziwa mashiriki au wanaanza shughuli zao humu nchini wanawekeza wanapewa masharti gani ya kuwadhibiti ili wasiwe wanakimbia wanapoona kwamba ule muda wa *tax holiday* unapita wakaenda kuwauzia wenzao hayo mashirika *and for that matter* mtu unaanza kujifikiria kama una akili nzuri kwamba huyu bwana kwa nini leo anaitwa *snake,* anasema amekwenda kumuuzia *Lizard* biashara yake, inawezekana huyu *Mr. Snake* ndiyo amekuwa *Mr. Lizard* lakini ametaka kutufunga tu ilimradi aweze kukwepa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kwamba hapo ni lazima tuwe waangalifu kwa sababu Serikali inapoteza mapato yake yaliyo mengi.

Mwisho kabisa ningependa kumzungumzia Mtanzania ambaye analipa kodi kwa kupitia yeye kwamba ni mwajiriwa wa Serikali au Shirika la Umma, huyu mwajiriwa huyu anakatwa kodi yake moja kwa moja inatoka, huyu akitoka kwenda kununua chochote dukani analipia pia *VAT,* huyu akisafiri ananunua tiketi anaambiwa lipia *VAT* huyu unakuta kwamba anafika mahali anaona kwamba mbona ni mimi tu ninalipa kodi nyingi katika nchi hii? Sasa ndiyo sababu nilikuwa nasema kwamba wale wengine ambao wapo wanafanya kazi na hawajalipa kodi basi na wao iangaliwe namna ambavyo wanaweza wakawajibishwa kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuchukua nafasi hii kuwapongeza watu wa *TRA* hususan Wafanyakazi wa *TRA* wa Mkoa wa Morogoro. Mimi ningependa kusema kwamba pamoja na matatizo mengi ya utendaji wanajitahidi kufanya kazi yao vizuri. Lakini ningependa waongeze bidii kuwadhibiti hawa wafanyabiashara ambao wanatoa elimu kwa wanunuzi kwamba msi-*demand* risiti kusudi msilipe *VAT.* Akikamatwa mtu wa namna hiyo, mimi naomba achukuliwe hatua za kisheria kama mhujumu wa uchumi katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango huo, ningependa kusema kwamba Wizara imefanya kazi nzuri pamoja na Mamlaka ya *TRA* na ningependa kusema kwamba ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika Muswada ulioko mbele yetu. Nianze kabisa kwa kuungana na Wabunge wenzangu kwa kuwapongeza wale wote ambao walichaguliwa kushika nyadhifa katika Taasisi za Kimataifa, ambao ni Mama Getrude Mongella, kwa kuwa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani na Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, kwa kuwa Rais wa Mawaziri wa Elimu ya Juu Barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwapongeze Waziri wa Fedha, Manaibu wake, pamoja na Watalaam wote wa Hazina na *TRA* kwa kazi nzuri walioifanya ya kuandaa Muswada huu ambao mimi nimeuona ni mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema ni mzuri kwanza kwa sababu Wizara imeonyesha kupokea mawazo kwa kiwango cha hali ya juu sana kwa sababu katika vifungu 145, vifungu 40 ambavyo ni sawa sawa na asilimia 30, vimefanyiwa marekebisho na hii ni karibu asilimia 30 ya vifungu vyote. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa usikivu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwapongeza walioandaa Muswada huu, naomba niende moja kwa moja katika Muswada wenyewe, kifungu namba 15 kimenipendeza sana, kifungu hiki kinaonyesha kwamba kabla ya kuandaa kodi gharama zile za kuanzishwa kama ni shamba, gharama za kuimarisha mazingira kuzuia mmomonyoko, gharama za utafiti na maendeleo, kuboresha huduma au kuboresha bidhaa zitaondolewa. Hii mimi naona kwamba inatoa changamoto sana kwa kuimarisha uwekezaji, kupanua ajira na kuboresha bidhaa ikiwa ni pamoja na kupanua wigo wa kodi na kwa hiyo Pato la Taifa. Kwa hiyo, kifungu hiki ni muhimu sana kwa sababu kinaimarisha sekta ambazo ni muhimu sana katika kuwezesha mapato kupatikana kwa njia ya kodi.

Ushauri wangu hapa ni uwezeshaji kwamba ili haya yaweze kupatikana lazima Serikali, ichukue jukumu la uwezeshaji kwa wale ambao wanapaswa waingize mitaji katika uzalishaji, katika kilimo, katika uvuvi. Nilifuatilia vizuri Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, alipokuwa anasisitiza suala la wakulima wadogo wadogo, wavuvi wadogo wadogo, wafugaji. Ukiangalia ukanda kwa mfano wa Ziwa Tanganyika, tunahitaji sana uwezeshaji kwa njia ya mikopo. Lakini ili hili liwezekane wito wangu kwa Waziri wa Fedha, ni kutoa maelekezo mazuri kwa Benki Kuu kwa sababu Benki Kuu ina nafasi kwa mujibu wa majukumu yake kuzielekeza Benki za Biashara na taasisi zingine za fedha kutenga mafungu kwa ajili ya kuwawezesha wananchi hasa wale wa kipato kidogo kuweza kupata mitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu zipo nchi duniani ambazo zina Benki zao Kuu zimetoa maelekezo makusudi kwenye Benki za Biashara, kwenye Taasisi za Fedha, kutenga mafungu maalum kwa ajili ya kuwakopesha hawa ambao wako katika sekta hasa ambazo siyo rasmi. Tusipochukua hatua hiyo, bado benki yetu itakuwa haijatenda jukumu kubwa na naamini Waziri kwa kuonyesha umahiri katika kuandaa

sheria hii ya kodi basi hilo litakuwa ni jambo la kuzingatia ili Benki Kuu nayo iweze kurekebisha sera zake kuzielekeza Benki za Biashara pamoja na Taasisi za Fedha kuliangalia hilo kama jukumu lao kubwa kuwawezesha wananchi kuwekeza hasa wakulima katika maeneo mbalimbali.

Mimi ukiacha eneo hilo la uvuvi katika Jimbo langu kwenye maeneo ya Bonde la Mto Malagarasi kule uwezekano ni mkubwa sana wa kuimarisha kilimo katika bonde lile. Vijiji vilivyo katika ukanda ule vya Uvinza, Nguluka, na kadhalika. Kwa hiyo, ni wito wangu kwamba hilo liangaliwe kwamba Benki Kuu itoe mwelekeo wa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kingine ambacho napenda nikizungumzie ni kifungu namba 58, kifungu hiki ambacho ni sehemu ya tano ya Muswada, inasema ni *special industries*. Katika kifungu hiki au sehemu hii ya Muswada *industries* ambazo zimetamkwa kwamba ni *special* ni pamoja na Bima, Akiba ya Uzeeni na Vyama vya Hiari, Vilabu na Vyama vya Kibiashara.

Ningependa katika sehemu hiyo nishauri kwamba Waziri na timu yake waangalie nadhani kuna *industry* nyingine ambayo ni *special* ambayo ingeweza kuwa nzuri pale na hii ni *shipping*. *Shipping* au shughuli zinazohusiana uchukuzi kwa njia ya bahari ni *special industry* na kwa Tanzania kama mojawapo ya nchi ambazo zina bandari nne katika ukanda huu wa Afrika Mashariki, labda wanaotuzidi ni Afrika Kusini tu. Lakini sisi Tanzania kwa kuwa na bandari hizo nilizosema nne ambazo ni Dar es Salaam, Mtwara Tanga na Zanzibar ukiacha hizi bandari ndogo ndogo, lakini pia kuna bandari kwenye maziwa yetu. Sasa *shipping* ni *special industry* na ni *special* katika manaa kuna kodi nyingi ambazo zinaweza kupanua uwigo mkubwa katika kulipatia Taifa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitazamia kwamba Muswada kama huu kwa sababu unaandaliwa na utakuwa kwa kipindi kirefu. Kwa sababu huu unaandaliwa baada ya ule wa mwaka 1973 kwa hiyo, karibu miaka 31. Kwa hiyo, natazamia kwamba kurekebisha tena hiyo itachukua miaka mingine ya namna hiyo. Kwa hiyo, ni wakati mzuri katika kuandaa chombo kama hicho kuweka vile vianzo vyote ambavyo vitapanua wigo wa mapato ya Taifa letu.

Kwa hiyo, *shipping* nadhani hii iangaliwe vizuri na wapo wataalam ambao kwa kweli *TRA* ni miongoni mwao lakini Mamlaka ya Bandari, haya makampuni ya uwakala wote hawa wanaweza kuchangia vizuri sana katika kuainisha, kuainisha aina mbalimbali za kodi ambazo nyingine kwa kweli inaonekana zimefichika na nakumbuka kuna kifungu fulani ambacho nimewahi kukisoma kinasema, *historically shipping* imekuwa ni *very trick* katika utoaji wa mapato au kodi kwa Serikali na hasa baada ya mabadiliko haya ya sasa ambapo wenye meli wamepewa fursa tu ya kuwa mawakala.

Sasa ni jinsi gani utakavyoweza kutoa taarifa kamili za kodi. Kwa hiyo, mimi ningependa kwamba hili liangaliwe na niungane labda kwa kipengele hiki labda niungane na mchangiaji Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, aliposema kwamba labda maeneo fulani wangeweza kupewa mkataba wale wajuzi katika eneo hilo wakasimamia

ukusanyaji wa kodi za namna hiyo. Sasa ningedhani hilo likiangaliwa linaweza kutuongezea wigo wa mapato.

Kwa mfano, wako waliokuwa wafanyakazi zamani wa *NASACO*. Nilisoma kwenye gazeti wakiomba wapewe fursa ya kuanzisha *MECCO*. Wapo wenzetu waliokuwa *TCFB,* wako waliokuwa hata bandarini *TACOSHILI*. Kwa kweli tuna *resource* za watu ambao wanaweza wakiungana pamoja wakawa ni wakala wazuri wa kukusanya hizo kodi kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo lingine ambalo nilidhani ni vizuri kuliangalia nalo ni kwa Serikali kuhamasisha uwekezaji. Uwekezaji ambao nauzungumzia ni ule ambao wapo Watanzania ambao wako nje, nje ya nchi ambao huko wanawekeza na pengine wangependa kuja. Nina mfano mmoja wa mwekezaji mmoja ambaye yuko Marekani ni Mtanzania yeye amebobea katika *designing* hizi mashine za ku-*process* vyakula.

Mwaka 2001 alikuwa *interviewed,* akasema alikuja hapa nchini, ana matarajio kweli ya kupenda kuwekeza hapa. Lakini mawasiliano hana na kule ana kiwanda kizuri sana. Ni *designer* nzuri wa mitambo ya namna hiyo na ame-*win* soko karibu na New York. Sasa wa namna ile nadhani ni vyema tukaendelea kuwavutia waje kuwekeza hapa nchini na wakiungana na hawa wenzao walio ndani ya nchi ambao nao wanaomba kuwekeza hapa nchini.

Mwisho Mheshimiwa Naibu Spika, ni kifungu kile cha 145. Kifungu hicho naomba nikinukuu. Kinasema: *"Where expenditure or a purchase price falls to be treated under the second schedule of the Income Tax Act, 1973, that schedule shall apply instead of Section 7, sub-division (d) of division one part three and the third schedule of this Act as the case requires."*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani huu ni Muswada au Sheria itakayokuwa mpya, sioni ni vema kwamba kifungu hicho kibaki kama kilivyo kikielekeza kwamba mtu aangalie kilivyo katika Sheria ya mwaka 1973 ambayo itakuwa imekwishafutwa. Nadhani hicho kifungu kingekuwa *reproduced* hapa hapa ili kutompa taabu huyo mtu anayetaka kutumia Sheria hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba niunge mkono mia kwa mia nikiwapongeza Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Waziri na timu yake ya *TRA* kwa kazi nzuri waliyofanya na naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutumia nafasi hii kutoa mchango wangu kuhusiana na Muswada huu uliowakilishwa mbele yetu.

Napenda nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, kwa kazi nzuri aliyoifanya katika suala zima la maandalizi ya Muswada huu akishirikiana na timu yote, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na

watumishi wengine wa Wizara hii ambao wameshiriki kwa namna moja au nyingine katika maandalizi mazima ya Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli Muswada huu umekuja wakati muafaka. Tukiangalia mazingira ilipotungwa Sheria hii hapo awali na mazingira ya sasa hivi kuna mabadiliko makubwa mno. Kwa hiyo, kutokana na mabadiliko hayo ni wazi kwamba ni Muswada ambao kwa kweli tulikuwa tunautegemea ili uweze kwenda sambamba na mazingira ya sasa hivi. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi pamoja na timu yake yote, Wajumbe wa Kamati hii kwa namna walivyouchambua Muswada huu kwa kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mchango huo umetufikisha mahali sisi Wabunge kazi yetu kuwa nyepesi. Kwa sababu sehemu kubwa ya mambo ya msingi wameyazungumza na habati nzuri Mheshimiwa Waziri amekuwa msikivu akayazingatia na kuyafanyia mabadiliko nawashukuruni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijachangia maoni yangu kutokana na Muswada huu, ninapenda nipongeze katika maeneo yafuatayo:-

Ninaamini kabisa Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakubaliana nami kwamba katika vikao mbalimbali vya Bunge vilivyopita tumekuwa tukizungumzia kwa nguvu sana kuhusu kuiomba Serikali kuwafikiria upya wastaafu ambao walipata fedha kwa mkupuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi sana siku hiyo nilikuwa nasikia kwenye redio kwamba Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha anatoa matangazo akiwaarifu wastaafu hao ili waende kujiorodhesha ili Serikali iweze kufanya taratibu za kuanza kuwalipa. Mimi nashukuru sana katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa dhati ya moyo wangu nimpongeze kwa dhati Kamishna Mkuu wa *TRA,* Ndugu Kitilya. Yeye pamoja na wale wote wanaomsaidia wamefanya kazi nzuri na kubwa ya kukusanya mapato ambayo yamefikia *average* ya bilioni ya 109 mpaka bilioni 11 kwa mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki ni kiwango kikubwa, lakini nimefurahi sana kwamba hawa wenzetu wa *TRA* katika mwezi wa Desemba peke yake waliweza kukusanya shilingi bilioni 136.5. Wanastahili pongezi kubwa sana hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha wamejiwekea lengo la kukusanya fedha shilingi trilioni 1.4. Kwa hiyo, tunawatakia kila la kheri katika kuhakikisha kwamba kiwango hiki kinafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia Muswada huu ambao umewakilishwa mbele yetu. Mimi nategemea kwamba Muswada huu utaleta mabadiliko ya kodi ambayo yatachochea kukua na kupanua kwa uchumi.

Aidha, Muswada huu utasaidia kwa kiasi kikubwa kuhakikisha kwamba sehemu kubwa ya mapato yatakuwa yanapatikana kutoka kwa mwananchi basi ile akiba atakayokuwa anabakiwa nayo mwananchi itamwezesha kuwekeza. Sasa katika mazingira hayo mimi nilikuwa na mapendekezo kadhaa, ingawa mengine yameshazungumzwa na wenzangu waliotangulia lakini mimi nitaongea tu kwa kifupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza nilikuwa napenda nipendekeze kwa kuiomba Serikali ifanye mkakati wa makusudi ya kuwasaidia wafanyabiashara ndogo ndogo nchi kwa kuwakopesha kwa masharti nafuu. *(Makofi)*

Kwa kuwapa ujuzi kwa njia ya mafunzo na kuwasaidia kuwatafutia masoko, hili limezungumzwa. Wote tunaelewa kwamba karibu katika maeneo yote tunayotoka, wako wafanyabiashara ndogo ndogo na wafanyabiashara. Lakini wanashindwa kupanua mitaji yao kutokana na masharti makubwa yaliyopo katika vyombo vyetu vya fedha.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba hili niiombe Serikali iweze kuona ni namna gani itakavyoweza kuwajengea mazingira mazuri wafanya biashara hawa ili waweze kupewa mikopo kwa masharti nafuu ambayo itawawezesha kuimarisha miradi yao hatimaye waweze kuwa walipa kodi wazuri ambapo watakuwa wamechangia kwa kiasi kikubwa katika pato letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la hili limeshazungumzwa kwamba Serikali ihakikishe kwamba suala la misamaha ya kodi haitolewi bila kuwepo na sababu za msingi. Hili limeshazungumzwa sipendi kuliendeleza zaidi. Lakini tatu, Serikali iwasaidie wawekezaji wa ndani katika kukuza sekta ya viwanda hasa wazalendo wapewe kila aina ya msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili nilikuwa naomba kwa kweli ufanyike mkakati wa makusudi. Tumekuwa tukishuhudia baadhi ya bidhaa zingine ambazo kwa kweli hata hapa hapa nchini zinaweza zikapatikana. Unashangaa unaona mpaka kuku wanaagizwa kutoka *South Africa,* wakati kuna wafanyabiashara wetu wadogo wadogo wanafanya hiyo biashara ya kuku. Unakuta mpaka matunda, nyanya, *cabbage,* viazi na kadhalika vyote vinatoka nje. Mimi nilikuwa nafikiri kwamba kuna haja Serikali kuweka mkakati wa makusudi wa kuhakikisha kwamba ili kuweza kulinda bidhaa hizi za ndani ikiwa ni pamoja na hawa wafanyabiashara ndogo ndogo waweze kuangaliwa ni namna gani wanavyoweza kusaidiwa katika suala zima la hizi bidhaa zao wanazozizalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba Serikali kwa makusudi isaidie sekta ya kilimo ili iweze kusaidia katika ukuaji wa uchumi. Maana uchumi wa mtu mmoja mmoja ukipanuka hata maeneo ya kutoza kodi pia yataongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili nilikuwa napenda Serikali iweke utaratibu nzuri wa kuwapa kila aina ya msaada wale wawekezaji ambao wanaonyesha nia ya kuweza kuwekeza katika sekta hii ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nilikuwa naomba nitoe ombi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na uongozi mzima wa *TRA* ni kwamba hawa wakadiriaji

wa kodi tunawaomba wahakikishe kwamba wanatenda haki kwa mlipa kodi. Maana wakadiriaji wana madaraka makubwa. Kwa hiyo, wakiyatumia vibaya wananchi wataumia na katika mazingira hayo, wananchi hao pia watatafuta mbinu mbalimbali za kukwepa kulipa kodi na katika mazingira hayo hayo yanajenga mazingira ya ushawishi wa rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hili ningependa nimwombe Mheshimiwa Waziri pamoja na viongozi wa *TRA* kuhakikisha kwamba wanalifuatilia kwa karibu sana ili wale watumishi wachache watakaokuja kubainika kwamba wanaenda kinyume na maadili ya kazi yao basi waweze kuchukuliwa hatua kali ili iweze kuwa ni fundisho kwao na kwa wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hili nilikuwa naomba tu nimwombe Mheshimiwa Waziri wakati atakapokuwa ana-*summarize,* basi asaidie kutupa, kama ana idadi yaani takwimu yoyote ya wale watendaji wa *TRA* ambao wamekuwa wakikiuka maadali ya kazi yao ambao wamekwishachuliwa hatua basi tuweze kuwafahamu na walipa kodi nao waweze kuwafahamu ili tuweze kuwa na uhakika kwamba kwa kweli Serikali imekuwa ikilifuatilia suala hili kwa karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mawazo yangu kwenye Muswada huu.

Kwanza ningeanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Naibu Waziri wa Fedha na Watendaji wa Wizara kwa kuleta mawazo mapya kwa sababu sasa hali ndiyo hiyo kwamba lazima tuendane na dunia ya sasa. Tufanye mapya, mapya ambayo yatatusaidia kwenda mbele siyo kurudi nyuma.

Pili, ningependa niwape pongezi wote waliochaguliwa kwenye Bunge letu hili akiwemo Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, akiwemo Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, katika nafasi mbalimbali walizozipata. Lakini kikubwa ningependa sana sana nitoe pole kwa Rais kwa haya matatizo aliyoyapata ya kuunguliwa makazi yake. Nina imani kwamba sasa anaanza kuzoea na atajiweka sawa lakini pia akijua kwamba tunamtakia kheri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilipoupata Muswada huu na baada ya kwenda nauangalia pole pole nilipata mawazo mazuri kwamba sasa naona mabadiliko yatakuja huko mbele. Kuna matatizo makubwa ambayo tunayajadili katika hali yetu ya kukusanya kodi katika nchi nzima na namna mlipa kodi anavyopaswa kutendewa. Tuna kodi mbalimbali ambazo ni nyingi ambazo zinamlenga mlipa kodi mmoja. Kodi ambazo tumekuwa tukizijadili mara nyingi tukitafuta ufumbuzi kwamba hizi kodi zipunguzeni kwa mlipa kodi mmoja.

Sasa mimi ningeiomba Wizara ianze kuangalia kwa makini kuna nyingine zinaweza zikaunganishwa kwa karibu karibu ikawa kodi moja ili kwamba mlipa kodi

huyu mmoja asiwe na ule utitiri wa kutoka hapa anahamia hapa, anatoka hapa anahamia hapa. Anapata kitu kimoja ambacho anakijadili kwa pamoja kama *package* na akimaliza kufanya hivyo basi anajua amemaliza *phase* yake ya kodi na pia ikiwezekana ndiyo mawazo ambayo najaribu kuyaona yanaanza kutoa mwelekeo kutokana na Muswada huu kwamba huko mbele ningefurahi sana kama tungeweza tukapata mtoza kodi mmoja badala ya wote ambao tulio nao. Serikali Kuu inatoza, Halmashauri zetu za Miji zinatoza. Anayetozwa ni yule mtu mmoja. Sasa anakaa anahangaika, anarudi huku na huku ambalo ni tatizo kubwa.

Lakini moja ambalo ningependa niliseme tu kabla sijajiingiza kwenye maelekezo yangu ambayo nimejielekeza kwenye Muswada huu ni suala hili zima na kupanua wigo wa kodi. Tarehe 16 niliuliza swali Bungeni nikajaribu tu kuangalia kwamba kodi zetu zinatoka sehemu gani na ilibainika kwamba Dar es Salaam wanalipa zaidi ya asilimia 80 ya kodi zote, mapato yote wanatoa watu wa Dar es Salaam, ambao hawa ni kama asilimia 10 tu ya wakazi wote nchini. Lakini lengo langu lilikuwa ni kuifungua Serikali macho, ijaribu kuangalia kwamba tupange namna gani uzalishaji huu ili kwamba wote waingie kiuchumi wafanye shughuli za kiuchumi ili mtandao wa kodi upanuke na *base* ya kodi ipanuke.

Kuna hoja nyingine zimetolewa humu ambazo kuzijibu inakuwa ni vigumu kama hali ya uchumi na bado tuliyonayo hivi sasa. Hoja za wazi kwamba katika Bajeti yetu nzima sisi ndani ya nchi tunachangia kama asilimia 55 hivi. Tunakusanya asilimia 12 kutoka kwenye Pato zima la Taifa na mambo mengine ya aina hiyo yanayolingana na kiasi gani tunatumia kwa mtu mmoja kwenye elimu na kwa mtu mmoja kwenye matibabu ya afya. Yako mengi unaweza ukayaainisha.

Lakini inakuwa vigumu kuzijibu hizi hoja kama hali ya kahawa bado inazorota namna hiyo. Hali ya pamba inasua, inakuwa vigumu sana sana kuzijibu hizi hoja. Hali ya pareto ndiyo hiyo sijui imezimika kabisa, sijui kama bado kuna pareto. Sasa hizi hoja tutazijibu namna gani. Niliuliza haya maswali makusudi Serikali iangalie, ione kwamba jukumu letu sasa liwe namna gani katika kujitosheleza kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, benki zetu ambazo hasa ni jukumu la Waziri wa Fedha, kuzifanya zifanye kazi zake katika kuhudumia sekta ya kilimo nyingi hazifanyi kazi hiyo na mimi katika kuchunguza haraka haraka nimekuta kuna vitu ambavyo vinaziletelezaa benki hizi zinazorota kufanya kazi. Kwa mfano, zinatoza *fees* nyingi kwa wateja wake. *Fees* ambazo Serikali ingeweza ikazikataza benki kutoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanapotoza hizo *fees* nyingi, wanapata pesa ambazo zinatosha kuendesha shughuli zao. Kwa mfano, kuna *fees* ya *Accounting Maintenance* ambayo inatozwa kwa wateja walio na *Current Accounts.* *Fees* ambayo inaanzia 5,000 na kwenda juu kufuatana na mteja yule. Kuna *Ledger Bank Fees* kitu kama hicho ambacho ni *fees* tu wanachukua *fees* kutoka kwa watu, *infact* ukweli ni kwamba watu wanakwenda kule kwa sababu ni lazima watunze pesa zao kwenye benki. Lakini wangetunza nyumbani wangeacha kupeleka kule na kuna *fees* nyingine ambazo kwa mfano unapoandika *cheque* kule inapolipwa *cheque* lazima kuwe na *service charge.*

Sasa unakuta kwamba riba yao wanaibakiza pale pale, kwa sababu inaonekana kana kwamba hawana shida ya kufanya biashara hawa. Lakini hizi namwomba Waziri wa Fedha kwa kweli achukue hatua hizi, pamoja na *BOT* waone haya mambo wayadhibiti namna gani. *Infact* yafutwe ili waweze hawa kwenda nje wakatafute wateja ili kwamba wawakopeshe na wale watakapowakopesha na wao wapate mapato yao. Kwa kufanya hivyo watasaidia sana sekta yetu ya kilimo.

Baada ya kusema hayo ningeomba nijielekeze kwenye suala zima la Muswada. Naomba nianzie na taratibu za namna gani Muswada umetoa nafasi ya kupokea au kusikiliza gharama za uanzishaji wa biashara. Nimeangalia kwenye Muswada hapa sikuziona. Unapoanzisha biashara kuna gharama nyingi unazipata. Unakwenda eneo jipya hujafika kule hata mara. Unafika pale unakaa hotelini unapiga simu wakati mwingine unaweza hata kununua vifaa, unajua kwamba biashara yako inaweza kuanza pale, ukajikuta haiwezekani, labda uhamie sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi gharama zinaachana, ziko za kawaida na ziko za kudumu. Sasa kwenye Muswada sioni namna gani anayeanzisha biashara asaidiwe au apokelewe ili aweze kuzifuta hizo gharama zake atakapokuwa ameanzisha biashara. Hili jambo ni jambo la msingi na la kitaalam na ningeomba tuone, tupate majibu kwamba litakwenda namna gani. Kwa sababu hizi gharama zinaachana na iwepo *provision* labda katika kifungu cha 11(2) labda kiongezwe 2(a) namna ya kufuta hizi gharama za uanzishaji wa biashara ni kitu ambacho kinaonekana ni cha lazima, sisi tunafanya shughuli kisasa na watu watakuja kuanzisha biashara hapa na hili jambo sijui wanalitekeleza namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, katika hilo hilo ni suala la sera. Sera zinapojitokeza zinagharamu sana wafanya biashara. Kuna wengine wanatoka kabisa kwenye biashara. Sasa hizi zinapojitokeza wana-*survive* kutokana na maamuzi ya sera hiyo, hawakupewa nafasi wajiweke namna gani sawa katika Muswada huu. Hili jambo ni la msingi sana kwa sababu tuna mifano ambayo iko hai. Kwa mfano, Bodi ya Pamba, imepata matatizo makubwa kutokana na mabadiliko ya sera.

Sasa hivi tuna sera ya soko huria, sera ambayo imewagusa wafanyabiashara kwa undani kabisa. Sasa katika sera hizi je, hawa watu wanapewa nafasi gani katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ningeomba tu tujielekeze kwenye kifungu cha 16(2) ambako Muswada umetoa nafasi ya kumpunguzia mtu katika gharama zake za *donations* anazozifanya. Lakini asilimia 2 naiona kwa sasa kufuatana na *willingness* ya watu kujitolea na kutaka kusaidia inakuwa ni ndogo. Kwa mfano, kwa wastani mfanyabiashara wa mapato ya jumla ya milioni 50, asilimia mbili kwake ni milioni moja tu. Lakini watu wapo tayari kutoa zaidi ya milioni 1 kama tutawapatia motisha hapa. Mimi ningeomba hiki kifungu kipande kutoka asilimia 2 kiwe asilimia 5 kitasaidia sana kuwatia sana kuwatia hamasa hawa watu waweze kuja kutuchangia katika shughuli zingine za maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho kiko katika Muswada huu ningependa tu nijielekeze katika sehemu ya 10, *administration* kwa ujumla suala ambalo limejadiliwa na kuzungumzwa kwa kirefu na Waheshimiwa Wabunge hapa ndani jambo ambalo najaribu kuangalia. Ndiyo lengo zima la Muswada, ndiyo lengo zima la Waziri kwamba mtoza kodi na mlipa kodi wawe marafiki, waweze kuwasiliana kwa usawa fulani. Hii tabia ya ukiritimba na umangimeza na ukubwa itoke na hili ni jambo ambalo ningemwambia Waziri moja kwa moja kwamba ajitahidi kila mahali ambayo utawala, utaratibu na *powers* kama zilivyoelezwa hapa, azipange kwa namna ambayo zitakuwa hazitishi mtu. Mlipa kodi awe huru kwenda kumtafuta mtoza kodi *freely* ili kwamba shughuli hizi na mambo yote yaende kwenye picha hiyo ambayo tunajaribu kuiangalia sasa kwamba tuwe na ukaribu, umoja na urafiki ndani ya kutoza kodi kwa sababu itakuwa vigumu kutekeleza kifungu Na. 91 ambako mtu anapashwa aseme mwenyewe ataweza kulipa kodi kiasi gani, kama mwenzake ana madaraka makubwa na anamtisha, itakuwa siyo rahisi.

Kwa hiyo, atakwenda kule atashindwa hata kujieleza. Kwa hiyo, hiki kifungu 91 mpaka 92 ambayo tumepewa nafasi kwa ajili ya watu wenyewe waende kuji-*assess* na kusema mimi naweza kulipa kodi kiasi fulani watashindwa kufanya kwa sababu ya hali ya madaraka na ukubwa ambao unatolewa na hii sehemu ya *administration.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba tu niunge hoja mkono na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na ubunifu huu aendelee nao na nadhani na mizimu hii iendelee ili kwamba katika Bajeti ijayo tuweze kupata mabadiliko mengine katika ujumla wake huu kwa sababu nina imani atakapokuja na mawazo, anaweza kuja na mapya kwa mfano tulivyoanza kwenye *Local Government* tuli-*privatize* sehemu ya shughuli na mapato yakaongezeka. Labda sasa tunafumba macho na *TRA* kwamba tukifanya privatization kule tunaweza kufanya zaidi na hali ikawa bora zaidi kuliko ambavyo tunafanya sasa.

Kwa hiyo, mimi namwomba sana Mheshimiwa Waziri aendelee na utaratibu wake pia wa kutuomba maoni, mawazo na kuzunguka kupata maoni ya wananchi kwa jumla kama alivyokuja Mwanza juzi tukaita wafanya biashara, tukapata maoni. Hii nina imani tutaboresha sana. Tunataka katika Bajeti ijayo au *also at least* tusiishie asilimia 13 ya Pato la Taifa. Labda tufike asilimia 16 au 17. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa ambao wameteuliwa kusimamia Mabaraza haya muhimu ya *Environment* na Vyuo Vikuu. Kweli Watanzania wenzetu hawa wameonyesha wazi kwamba wanao uwezo wa kuwafanya hivyo ndio maana wenzao wamewapa imani hiyo na wapo Watanzania wengi tu wenye uwezo huo

kwa hiyo, nadhani kila tunapoenda tutaendelea kuwajenga wengi zaidi ili kuweza kuchangia katika ulimwengu huu wa utandawazi. *(Makofi)*

Katika Muswada huu ninayo machache tu ya kuchangia. Kwanza, mimi kama Mwalimu wa zamani nadhani hili suala la kodi linahitaji elimu, kujenga maana ya kulipa kodi miongoni mwa Watanzania na nadhani tuanzie mashuleni. Enzi hizo sisi tuliposoma kulikuwa na somo la uraia ambalo linakufundisha namna ya kuwa raia mwema. Somo hilo lilikuwa linakusaidia usivunje sheria na uwe na majukumu katika jamii yako. Nadhani halikuwa na tofauti na kile ambacho tunakifahamu katika mila na desturi ya kwamba kama wewe ni wa kabila fulani kuna mila na desturi zake. Hili mimi nadhani linakosekana, watu wengi hatuoni kwamba kulipa kodi ni uraia mwema na kwamba ukitaka kuwa raia mwema unachangia maendeleo ya Taifa lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sio kosa la mtu mmoja mmoja ni namna mfumo wetu wa uchumi ulivyo. Mtu wa kawaida anajikuta kama kile anachokifanya haoni uhusiano wake na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Matokeo yake ni kwamba unapokuwa umepata pesa zako halafu mtu anakugongea uchukue pesa zako umpe, hiyo nadhani dhana ya kwamba mtu anagonga kuomba pesa zako na maelezo hayapo kwa nini umpe pesa zako. Kwa hiyo, Serikali inaonekana kama inanyang'anya kutoka kwa mtu ambaye ametokwa jasho na amepata kipato hicho na mtu anataka kukichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi iliyopo pia baada ya Muswada huu kupita ni namna tutakavyohusisha kila mtu katika ngazi zote kutoa elimu ya maana ya kodi katika jamii katika njia ambayo siyo ya nguvu. Watu wamezoea kodi ni mpaka tushikane, tusukumane badala ya kusema wewe umeanzisha duka, wakati anachukua leseni, wajibu mmojawapo ni kwamba katika kufanya biashara hii unapaswa urudishe kiasi fulani ili kuweza kuendeleza nchi kwa sababu bila nchi kuendeleza kwa mfano mawasiliano, usafiri na nchi kuwekwa katika hali ya amani huwezi kufanya biashara. Wafanyabiashara wengi wanaipenda Tanzania kwa sababu ya amani ambayo sisi tunailipia sana na haijaonyesha kiasi gani tunalipia hawa watu kukaa katika nchi yetu wakatengeneza pesa kwa gharama za walipa kodi wa Tanzania. Kwa hiyo, nadhani suala hili tulifafanue vizuri tusichoke.

Lingine ambalo naliona ni la muhimu ni kujenga uwezo wa Mtanzania kulipa kodi. Tunasema zaidi ya 50% ya Watanzania wanaishi kwa dola moja kwa siku yaani shilingi 1,000 huyu unapomlipisha kodi maana yake umechukua hata ile dola moja kwa sababu hujamjengea ule uwezo wa kuweza kulipa kodi hiyo au anapofanya biashara anafanya biashara ambayo ni ndogo kiasi kwamba kutoa kodi anajisikia kama anaumia sana.

Katika sheria hii mpya nafikiria kwamba tutajitahidi kuiboresha kila wakati kwa sababu sheria haiwezi kutungwa kama Biblia lakini tukiendelea kuiboresha kama walivyofanya safari hii Wizara inayohusika ambapo napenda nimpongeze Mheshimiwa Basil Mramba na Naibu Waziri, nadhani tukiendelea kuboresha hivi na huu usiwe mwisho tunaweza kufika mahali kwa kweli tukaendelea sasa kupeleka kile kinachokipata katika kodi katika kuboresha na kujenga uwezo wa Watanzania kulipa kodi. Unapokuwa

una kidogo mno unapata shida kuona kwamba kulipa kodi ni kitu cha heshima na kitu ambacho kinajenga uzalendo wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika walipa kodi kuna wengine ambao wako katika kundi lingine sio Watanzania ni wawekezaji na wale ndio wanaowekeza katika maeneo yanayozalisha zaidi. Kuna wakati nilipata kuzungumza na mtu mmoja wa Benki nikamwuliza kwa nini dola huwa ina-*change.* Akasema inaenda kwa vipindi, vipindi ambapo dola za pamba zinaingia shilingi inapanda thamani wakati zinaingia dola za korosho kwa sababu umevuna shilingi inapata nguvu. Sasa mimi nikauliza, je, inapoingia pesa ya dhahabu? Akasema kwa kweli sina uhakika sijawahi kuiona ikileta mshtuo katika uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda Waziri atanisaidia hapa hawa wawekezaji wakubwa wanapaswa kutoa mshtuko katika uchumi wetu kiasi tukaona kwamba kuna manufaa ya wao kuja katika kuwekeza katika uchumi wetu. Kama pamba inaweza kutoa mshtuko, korosho ikatoa mshtuko na mazao mengine yakato mshtuko madini je, yanatoa mshtuko kiasi gani katika uchumi wetu? Kama isipoonekana yanatoa msukumo kwa nini tuyachimbe, kwa nini tuharibu nchi yetu kwa kutoa dhahabu halafu isilete mshtuo? Hatuwatozi kodi ya kutosha na kama hatuwatozi kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona Waheshimiwa wenzangu tunalalamika juu ya *tricks* za watu katika kukusanya kodi, kulipa kodi, tunafika mahali kama vile sisi wote tumebweteka wanaotuongoza sasa ni wale wanaolipa kodi na hasa walipa kodi wakubwa ya kwamba wao ndio wana-*set the price* halafu sisi tunafuata nyuma.

Napendekeza tuwe na orodha ya wazi, orodha ya walipa kodi wakubwa wote hata sisi tuwajue na kila mwaka tuwe tunaonyeshwa hawa wamelipa kiasi hiki, hawa wamelipa kiasi hiki na wale wamelipa kiasi hiki na katika eneo la pamba kodi iliyoingia ni hii, eneo la korosho kodi iliyoingia ni ile ili tuweze kuona kwenye Bajeti ile najua inakuwa *reflected.* Lakini si ingekuwa vizuri tu tukaonyeshwa kama *appendix* fulani ya kupata nani kaingiza nini na hapo watu wangejisikia kama ni mlipa kodi akajiona kwenye orodha mwaka jana alilipa kidogo lakini mwaka huu amelipa zaidi tungemheshimu na hata wenzake wangeona aibu wanaojaribu kutubabaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua uwezo alionao Mheshimiwa Basil Mramba, hao wanaobabaisha kodi akiwadhibiti anaweza akawamudu kwa sababu nchi hii haiwezi kuendelea bila malipo ya kodi. Tuna mfano mzuri tu wa kutumia MMEM. MMEM hatukupewa bure ni pesa zitakazolipwa na walipa kodi wa Tanzania lakini ina mstuo katika maeneo tunakotoka. Mtu ukimweleza kwamba hii inatokana na kodi yako ambayo sasa inarudia kwako, Serikali inakuja kuunga mkono juhudi zako za kujenga madarasa, mwananchi sasa anaona aahaa kumbe hii ndio ile pesa niliyopeleka pale. Kwa hiyo, hiyo *list* ninayoiomba hata mifano mizuri hii ni vizuri wananchi wakaifahamu kwa sababu wakati mwingine inakuja *in isolation* haionyeshwi moja kwa moja kwamba matokeo ya kodi yako hili limefanyika. Hilo nalo ni moja ambalo nilitaka nilizungumzie.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujenga uwezo wa walipa kodi, nadhani maeneo yangetizamwa, wapi ambapo ukitoa msukumo kidogo umejenga uwezo wa watu hawa kulipa kodi, umejenga uwezo wao wa kulipia hospitali, unajenga uwezo wao wa kulipia shule, unajenga uwezo wao kujilisha wenyewe. Nadhani hilo nalo tungeweza kuliangalia katika kujaribu kuweka uwezo wa wananchi mmoja mmoja au kwa makundi kuweza kuchangia au kujenga uwezo wa kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina tatizo moja ambalo naomba niliulize hapa nalo ni tatizo la mafuta kama vile dizeli, petroli, katika uchumi kuna vitu ambavyo vinakuwa injini ya maendeleo ikipanda kidogo ina-*impact* kwenye uchumi wetu. Mimi natoka Kanda ya Ziwa, kwa kuangalia kidogo tu naanza kuona kama kuna matatizo, sekta hii hatujaidhibiti vizuri kwa hiyo wale walio na uhalali wa kuingiza mafuta wanaathirika kwa kutowadhibiti wale ambao wanapita njia za panya. Wanaopita njia za panya wakishakuwa wameharibu utaratibu na mtiririko mzima basi matokeo yake itajionyesha katika kilimo cha pamba, uvuvi na katika sekta zote kwa sababu injini hii ambayo ndio inaendesha uchumi wa nchi inakuwa imeingiliwa na watu ambao hawana nia njema na maendeleo ya nchi hii na nadhani tunawajua. Sidhani kama sisi Watanzania tu wapumbazi kiasi kwamba hatujui nani anakoroga nini, nadhani tunawajua. Kama hiyo, ndiyo kwamba hatuwajui, tusimame hapa tulielie, hivi ni nani atakayekuja kusema hii haiwezekani katika nchi yetu huwezi kuja kufanya chochote kile unachotaka kwa sababu unatokorogea uchumi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba hilo la mafuta ulizingatie na mtiririko mzima na mzunguko hasa katika Ukanda wa Ziwa ni nini kinachovuruga utaratibu mzuri wa kulipa kodi kutokana na mafuta?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa wale wote walionipongeza kwa kupata nafasi hii ya kusimamia Bunge la Afrika na napenda niwahakikishie kwamba nitahitaji msaada wa kila mmoja wenu. Nafasi hii nimeipata kwa niaba yenu nyie ambao mlinituma huko kwenda kuwawakilisha kwa hiyo, nitakuwa tayari kabisa kushirikiana nanyi na mijadala kama hii ndio itatuwezesha sisi watano ambao tunatoka hapa tuweze kushiriki kwa kikamilifu hasa yakizungumzwa masuala ndani ya Bunge hili yanayohusu Bara zima la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono Muswada huu na nimhakikishie Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwamba *they are on the right truck,* ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge, Balozi Getrude Mongella, ndiye alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho. Nimepokea taarifa kwamba Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, angependa kutumia haki yake ambayo iko kwenye Kanuni ya 21(6) ya Kanuni zetu za Bunge atumie hiyo nafasi ya kuahirisha Bunge ili atoe maelezo yake. Sasa namwita Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili atoe hoja ya kuahirisha Bunge kwa kadri ya Kifungu cha 21(6) ili tuweze kumsikiliza Mheshimiwa Thomas Ngawaiya.

## KUAHIRISHA BUNGE KABLA YA WAKATI WAKE

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe takriban saa moja kabla ya wakati wake hadi kesho saa tatu asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

## HOJA BINAFSI

## UCHAGUZI KATIKA SERIKALI ZA MITAA NA NAMNA MATOKEO YA CHAGUZI HIZO YANAVYOFUTWA

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya mwisho leo niweze kutoa hoja kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii ni kama naikumbushia Serikali kuhusu hoja niliyokuwa nimeitoa tarehe 8 Aprili, 2003 kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa na namna Kamati za Malalamiko zinavyofuta matokeo kinyume na maagizo au hukumu ya Mahakama Kuu ambayo ilikaa mwaka 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuja hapa Bungeni, sitaki niseme mambo mengi kwa sababu sitaki niwachoshe Wabunge...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, naomba ukae kwanza. Naomba nitoe maelekezo kwa taratibu ya Kifungu hicho ambacho unataka kukitumia, Kanuni ya 21(6) kinasema: “Endapo Spika atakuwa amepokea taarifa ya Mbunge yeyote anayetaka kutoa maelezo yake chini ya fasili ya (9) ya Kanuni hii, basi badala ya yeye kuahirisha Bunge, Spika atamwita Waziri anayetoa hoja ya kuahirisha Bunge ili kutoa nafasi kwa Mbunge huyo aweze kuchangia hoja hiyo kwa kutoa maelezo yake lakini itabidi maelezo hayo yawe yameandikwa na kuwasilishwa kwa Spika angalau siku moja kabla ya kutolewa, na Mbunge anayehusika atayasoma kama yalivyoandikwa.” Kwa hiyo, utayasoma kadri ulivyoandika. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi niko hivyo ila labda nilikuwa najaribu kutaka kufupisha lakini kama utataka nisome, nitasoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwezi wa saba, Serikali ilinijibu kupitia hoja hii lakini bado ikaelekeza kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye ndiye alitakiwa kujibu. Kama nilivyoandika hapa nimeleta malalamiko ndani ya Bunge hili kuishtaki

Wizara ya Sheria na mambo ya Katiba kwa Mheshimiwa Spika, sasa naisoma, ili kujibu Hoja Binafsi niliyowasilisha kwenye Bunge tarehe 8 Aprili, 2003 kuhusu hukumu ya Jaji Kyando juu ya kufuta matokeo ya chaguzi za Serikali za Mitaa. Mimi ninaamini kwamba Bunge ni chombo cha juu sana katika Serikali yoyote ndio maana kunakuwa na nafasi ya pekee ya kuhoji Serikali kuhusu mwenendo wake pamoja na kuishauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilileta Hoja Binafsi mbele ya Bunge lako Tukufu ikihusu baadhi ya chaguzi zilizokuwa zinafanywa katika maeneo mbalimbali na kufutwa na *WEO* na *VEO* kinyume na maagizo ya Mahakama Kuu kutoruhusu kufutwa kwa matokeo ya chaguzi za Serikali za Mitaa na mtu yeyote zaidi ya Mahakama ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu waliofutiwa matokeo ya chaguzi kinyume na hukumu hiyo ya Jaji wa Mahakama Kuu ni wengi na hasa wale wa Vyama vya Upinzani. Nilipojaribu kuuliza, niliambiwa eti nikitaka niende Mahakamani. Je, ni Mahakama ipi tena wakati Mahakama Kuu ikishaamua juu ya jambo fulani ni agizo kwa Mahakama zote pamoja na umma mzima?

Mimi binafsi pamoja na waathirika wote katika chaguzi hizo, tumesikitishwa sana jinsi Waziri alivyochukua muda mrefu katika kujibu hoja hiyo na alipokuja kujibu hakuweza kutoa jibu sahihi kwani hoja ilielekezwa kwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba na wala sio Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambaye ni *interested party.* Hata hivyo, ukiangalia majibu yake bado yeye mwenyewe anakiri na kuelekeza kwenye Wizara ya Sheria kama nilivyoomba mimi mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii danadana inaonyesha jinsi Mawaziri wanavyodharau Bunge lako na wasivyojali hoja za Wabunge.

Mwisho naomba nipate majibu mapema ili niwajulishe wenzangu kwa maana ubabe sio jambo zuri mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, hapa naambatanisha majibu ya Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kama nilivyosema umesoma vizuri, imeeleweka na hukupoteza muda sasa upande wa Serikali kuna mtu anaweza kujibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa!

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFIS YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba nitoe maelezo ya Serikali kuhusiana na maelezo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyatoa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 8 Aprili, 2003, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini, aliwasilisha kwenye Bunge hili Hoja Binafsi iliyohusu Sheria za Uchaguzi zinazogongana ngazi ya Kitongoji, Kijiji na Mtaa. Katika hoja hiyo, pia Mheshimiwa Thomas Ngawaiya alirejea hukumu ya Mahakama Kuu ya

Mheshimiwa Jaji Kyando kuhusu uwezo wa Kamati za Malalamiko na Kamati za Rufaa kufuta matokeo ya chaguzi za Serikali za Mitaa, ngazi za vijiji, Vitongoji na Mitaa.

Mwaka huu katika kikao hiki cha Bunge, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, ameleta tena hoja hiyo akitaka kupata majibu ya hoja yake ya mwaka jana kuhusu uamuzi wa Mahakama Kuu kwamba Kamati za Malalamiko na Kamati za Rufaa hazina uwezo wa kubatilisha matokeo ya uchaguzi wa Wenyeviti na viongozi wengine wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa.

Kamati za Malalamiko na Kamati za Rufaa zilizotajwa katika hoja hizi ni zile ambazo zimeundwa chini ya taratibu za uchaguzi wa viongozi wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa kupitia matangazo ya Serikali Na. 253, 254, 255 na 256 ya tarehe 20 Agosti, 1999.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama Kuu katika Kesi ya Madai Na.72 ya mwaka 2000 iliyohusu uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa wa Rangitatu, Wilayani Temeke ilitoa uamuzi kuhusiana na madaraka na uwezo wa Kamati za Malalamiko na Kamati za Rufaa kwamba kisheria Kamati hizo hazina uwezo wa kubatilisha matokeo ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa na kwamba Mahakama ya Hakimu Mkazi ndio yenye madaraka hayo. Aidha, Mahakama Kuu hiyo iliamua kwamba Bwana Iddi Mkambaku kuwa alikuwa mshindi halali katika uchaguzi huo wa Mwenyekiti wa Mtaa wa Rangitatu, Wilayani Temeke na kwamba ndiye anastahili kuwa Mwenyekiti.

Katika maelezo yangu niliyoyatoa hapa Bungeni tarehe 25 Julai, 2003, nilieleza bayana na kwa kirefu madaraka ya Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa kutunga taratibu za uchaguzi katika ngazi za Vijiji, Vitongoji na Mitaa hivyo nisingependa kurudia tena maelezo hayo. Aidha, katika maelezo yangu ya tarehe 25 Julai, 2003, nililijulisha Bunge lako Tukufu kwamba suala hili nililiwasilisha kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata mwongozo wake. Hatua ya kuliwasilisha suala hili kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali sio danadana na wala sio hatua iliyokusudia kulidharau Bunge lako au kutojali hoja za Wabunge. Napenda ieleweke kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiye Mshauri Mkuu wa Serikali kuhusu masuala yote yanayohusu sheria. Hivyo hatua ya kuwasilisha suala hili kwake ni katika kuzingatia umuhimu wa nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufanyika mawasiliano kati ya Ofisi yangu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kama ifuatavyo:-

(i) Maamuzi ya Mahakama Kuu katika kesi ya Madai Na.72 ya mwaka 2000 inayohusu uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa wa Rangitatu, Wilayani Temeke ni halali na yenye nguvu za kisheria na Serikali itatekeleza maamuzi hayo kikamilifu. *(Makofi)*

(ii) Kwa kuwa Serikali imezingatia maagizo ya Mahakama Kuu katika Shauri Na.72 ya mwaka 2000 inayohusu uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa wa Rangitatu, Wilayani Temeke, Ofisi yangu itafanya uchambuzi katika Halmashauri zote ili kubaini Wenyeviti ambao matokeo yao yalibatilishwa na Kamati za Rufaa na mara baada ya

kupata maelezo hayo, Ofisi yangu itawaagiza wasimamizi wa uchaguzi huo ambao ni Wakurugenzi wa Halmashauri kuwarudisha Wenyeviti hao kwenye nafasi zao. *(Makofi)*

(iii) Kwa vile kumejitokeza mkanganyiko katika Sheria ya Uchaguzi wa Madiwani Na.4 ya mwaka 1979 na Sheria ya Serikali za Mitaa Na.7 na 8 za mwaka 1982 pamoja na taratibu za uchaguzi wa viongozi wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa kupitia matangazo ya Serikali 253, 254, 255 na 256 ya mwaka 1999, Serikali inalifanyia kazi suala hili na katika wakati muafaka, Serikali itawasilisha Bungeni mapendekezo ya kurekebisha vifungu vya Sheria za Serikali za Mitaa Na.7 na 8 za mwaka 1982 ili ziendane na Sheria ya Uchaguzi wa Madiwani Na.4 ya mwaka 1979 kama ilivyobainishwa na Mahakama Kuu katika hukumu tajwa hapo juu. Aidha, Serikali itazirekebisha taratibu za uchaguzi wa viongozi wa Vitongoji na Mitaa ili ziweze kuzingatia maamuzi haya ya Mahakama Kuu ya Tanzania.

Mwisho napenda kumalizia maelezo yangu kwa kumshukuru Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijiji, kwa kuwasilisha hoja yake hii ambayo ni ufuatiliaji wa Kauli ya Serikali niliyoitoa katika Bunge lako Tukufu tarehe 25 Aprili, 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, sasa nitawahoji juu ya hoja ya kuahirisha Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 12.58 Jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa*
*Tarehe 23 Aprili, 2004 Saa 3.00 Asubuhi)*